SUPA JACKPOT
TZS.1,044,303,118
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



UKURASA 4

**RIPOTI MAALUM**
Watelekeza familia kisa ukosefu wa samaki bwawani




UKURASA 13

Nipashe
MWANGA WA JAMII
Jumamosi Oktoba 29, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0581113
www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

# UKATILI WA WENZA

**WATAKA** sheria ya dharura uovu majumbani... *Endelea ukurasa 9*




Mchuuzi wa mahindi ya kuchoma akionyesha kukaidi na kuendelea na shughuli zake, licha ya kuwepo kwa bango la zuio la kufanya biashara lililowekwa na Wakala wa Barabara nchini (TANROADS), kando ya Barabara ya Bagamoyo, eneo la Mbezi Tangi Bovu, Manispaa ya Kinondoni, mkoani Dar es Salaam jana. **PICHA: SABATO KASIKA**

UKURASA WA 2

## ACT WAJENGA MAKAO MAKUU

CHAMA cha ACT-Wazalendo kinatarajia kuzindua ofisi yake mpya kesho waliyojenga Magomeni mkoani Dar es Salaam, itakayokuwa makao makuu...

UKURASA WA 3

## OFISA MTENDAJI KUKATWA MSHAHARA KWA MIAKA MITATU

HALMASHAURI ya Wilaya ya Wanging'ombe mkoani humo imeagiza kukatwa mshahara asilimia 15 kila mwezi kwa muda wa miaka mitatu...

UKURASA WA 8

## WATAKA MIKOPO ELIMU YA JUU INUFAISHE WENGI

KAMATI ya Makamu Wakuu wa Vyuo Vikuu nchini (CVCPT) imeishauri serikali kupanua wigo wa kutoa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu ili kuwezesha wanafunzi wengi wanaohitaji kujiunga na vyuo vikuu kupata nafasi...

# 45 waugua kwa kunywa pombe

**WAMO** watoto, mtengenezaji wake afa... *Endelea uk. 2*

## Mwanafunzi wa darasa la tano adaiwa kujinyonga

UKURASA 3

**MICHEZO** MGUNDA: UCHOVU ULIIMALIZA SIMBA UK. 32

**KATUNI** UK. 6

# 45 waugua kwa kunywa pombe, wamo watoto

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

MFANYABIASHARA wa pombe za kienyeji, mkazi wa Kijiji cha Nambala, Wilaya ya Mbozi mkoani Songwe Kenneth Nzunda (58), amefariki dunia huku wengine 45 wakiwamo watoto, wakilazwa hospitalini baada ya kunywa pombe ya kienyeji.

Kamanda wa Polisi mkoani hapa, Alex Mukama amethibitisha kutokea tukio hilo na kubainisha kuwa uchunguzi zaidi unaendelea.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Serikali wilayani Mbozi (Vwawa), Dk. Kenneth Lesilwa alisema waliowapokea walikuwa wakilalamika kusumbuliwa na tatizo la kuharisha, kutapika na tumbo kuuma na kati yao, wagonjwa watano walitibiwa na kuruhusiwa.

Alisema walipokea mwili wa Nzunda ambaye inadaiwa kuwa ndiye aliyekuwa akiuza pombe hiyo.

"Kati ya wagonjwa hao kulikuwa na watoto wawili, mmoja ana umri wa mwaka mmoja na miezi tisa na mwingine ana umri wa miaka miwili na mwezi mmoja, ambao nao wanadaiwa kunywa pombe iliyopikwa nyumbani kwao," Dk. Lesilwe alisema.

Alibainisha kuwa kati ya waliougua, wanawake ni 36 na wanaume ni wanne na kwamba wagonjwa wengine watano wanadaiwa kupelekwa hospitali binafsi za Ilasi na Kituo cha Afya Sifika.

"Licha ya kwamba hakuna dalili ya kipindupindu, sampuli za wagonjwa wote zimechukuliwa ili kufanyiwa vipimo zaidi kwa kuhofia kuwa unaweza kuwa ugonjwa wa kipindupindu ambao umeingia nchini Malawi," alisema.

Dk. Lesilwe alisema wanatarajia kuwaruhusu wagonjwa 36 kutoka hospitalini baada ya hali zao kiafya kuimarika.

Juliana Tuya, mmoja wa waliolazwa hospitalini huko, alisema tukio hilo lilitokea Jumanne baada ya kutoka msibani na kupita katika kilabu cha pombe za kienyeji.

Alisema kuwa baada ya kunywa pombe hiyo, muda mfupi walianza kusikia maumivu makali ya tumbo na kuanza kutapika na kuhara.

Mke wa marehemu, Wema Mwampashe (40) ambaye amekuwa akishirikiana na mume wake katika kazi hiyo, alisema amekuwa akiendesha maisha yake kwa kupika pombe za kienyeji na kushangaa kwa nini hiyo imeleta madhara kwa familia yake.

"Huwa ninapika pombe na mume wangu ambaye anaendesha kilabu cha pombe ndiye mteja wangu, huniuzia na kuniletea fedha, lakini siku hiyo nilipoanza kuumwa nilimpigia simu kumweleza hali yangu na watoto wawili akiwamo na mama yangu lakini nilishangaa baadaye hakunitafuta tena hadi tulipoletwa hospitalini nimeambiwa kafariki dunia," alisimulia.



Ofisa Programu Mkuu wa Asasi ya AGENDA inayojihusisha na utunzaji wa mazingira na maendeleo wajibifu, Silvani Mng'anya, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam juzi, wakati wa kuadhimisha siku ya kimataifa ya kuzuia madhara ya madini ya risasi yanayopatikana kwenye rangi. Kulia ni Ofisa Programu Mwandamizi wa asasi hiyo, Dorah Swai. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# ACT-Wazalendo wajenga makao makuu

**Na Romana Mallya**

CHAMA cha ACT-Wazalendo kinatarajia kuzindua ofisi yake mpya kesho waliyojenga Magomeni mkoani Dar es Salaam, itakayokuwa makao makuu.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Naibu Katibu wa Habari, Uenezi na Uhusiano na Umma wa chama hicho, Janeth Rithe, uzinduzi huo utafanyika kwa kuhudhuriwa na viongozi wa ndani na nje ya nchi.

Rithe alisema, mgeni rasmi katika uzinduzi huo atakuwa Kiongozi wa chama hicho, Zitto Kabwe, akibainisha kuwa jengo hilo lina ofisi za kisasa, kumbi za mikutano, studio, ofisi za viongozi na maktaba.

"Mbali na viongozi na wanachama wa ACT-Wazalendo, wengine watakaohudhuria ni watu mbalimbali wakiwamo viongozi wa dini, wawakilishi wa serikali na wanasiasa kutoka ndani na nje ya nchi," alisema.

Rithe alisema baadhi ya vyama vya nje ya nchi vitakavyotuma wawakilishi ni pamoja na chama tawala cha Zambia (UPND) ambacho kinatarajia kuwakilishwa na Katibu Mkuu wake, Imenda Batuke na Mkurugenzi wa Mambo ya Nje ya chama, Rose Sikala.

Pia alisema, chama kikuu cha upinzani Zimbabwe (CCC) kinatarajiwa kuwakilishwa na Katibu Mkuu wake, Chalton Kwende na Mkurugenzi wa Mambo ya Nje wa chama, Grady Hlatywayo.

Chama cha ACT-Wazalendo kilipata usajili wa kudumu mnamo Mei 2014. Chama hicho kwa kiasi kikubwa kilitokana na makundi mawili; la kwanza likiwa la waanzilishi wa chama waliotoka Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) waliokuwa wanamuunga mkono Zitto katika mapambano yake ndani ya CHADEMA na la pili ni waliokuwa viongozi wa ADC ambao nao wengi wao chimbuko lao la asili ni waliokuwa wafuasi wa Hamad Rashid ndani ya Chama Cha Wananchi (CUF).

# Kamati Kuu ya CCM yampongeza Samia

**Na Mwandishi Wetu**

KAMATI Kuu ya Halmashauri Kuu ya Taifa (CC-NEC) ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) imempongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa kupokea ripoti ya kikosi kazi alichokiunda kuratibu maoni na mapendekezo ya wadau mbalimbali juu ya mchakato wa mustakabali wa taifa katika uendeshaji wa siasa .

Pongezi hizo zilitolewa jana katika kikao cha Kamati Kuu ya CCM kilichofanyika jana jijini Dodoma chini ya Mwenyekiti wake, Rais Samia.

Taarifa iliyotolewa jana na Katibu wa NEC, Itikadi na Uenezi, Shaka Hamdu Shaka, ilisema hatua hiyo aliyochukua Rais ni kubwa na ya kupigiwa mfano.

Shaka katika taarifa hiyo alisema tangu alipoingia madarakani, Rais Samia amekuwa mstari wa mbele katika kusimamia utekelezaji wa ilani ya uchaguzi ya CCM 2020-2025, kuimarisha demokrasia ya vyama vingi vya siasa na ujenzi wa maridhiano ili kuliwezesha taifa kuendelea kuwa na utulivu wa kisiasa, umoja na amani kwa maendeleo endelevu.

Pia alisema Kamati Kuu imempongeza Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, kwa kuendelea kuimarisha uhusiano wa kisiasa visiwani Zanzibar kwa kuunda kikosi kazi cha kuratibu maoni kwa upande wa mambo maalum yanayohusu Zanzibar.

Shaka alisema kikosi kazi hicho kinaendelea vyema na majukumu yake hatua ambayo itaimarisha demokrasia, umoja na mshikamano.

Katika hatua nyingine, Shaka alisema Kamati Kuu imepokea taarifa ya awali ya maandalizi ya Mkutano Mkuu wa Taifa wa 10 wa CCM unaotarajiwa kufanyika Desemba, mwaka huu.

Alisema Kamati Kuu imeridhishwa na hatua mbalimbali za maandalizi ya mkutano mkuu huo wa kawaida utakaofanyika kwa mujibu wa Katiba ya CCM ya mwaka 1977 toleo la mwaka 2022 Ibara ya 99(3),

"Mkutano Mkuu wa CCM wa Taifa utafanya mikutano yake ya kawaida mara tatu katika kipindi cha miaka mitano. Mikutano miwili kati ya hiyo itakuwa ya uchaguzi na mmoja utakuwa wa kazi.

"Kalenda ya vikao vya chama itaonyesha ni lini mikutano mitatu hiyo itafanyika lakini mkutano usiokuwa wa kawaida unaweza kufanyika wakati wowote ukiitishwa na Mwenyekiti wa CCM au ukiombwa na theluthi mbili ya wajumbe wote wa Halmashauri Kuu ya Taifa," alisema.




Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi isiyo ya kiserikali inayojihusisha na kusaidia vijana kuwajengea uwezo wa kujitegemea ya Tanzanite Support Organization (TSO), Bahati Chando (wa pili kulia), akikabidhi cheti cha kuhitimu mafunzo awamu ya kwanza ya kuwajengea uwezo wa kujiajiri katika sekta mbalimbali, kwa Assanath Abass, kutoka kituo cha kulelea watoto yatima cha Ijango, katika hafla iliyofanyika mkoani Dar es Salaam jana. Kulia ni Mtengeneza Maudhui wa Taasisi ya Mind Garden, Shannon Abdulrahaman. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mwanafunzi darasa la tano adaiwa kujinyonga

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MWANAFUNZI Brayton Daniel (11) wa darasa la tano katika Shule ya Msingi Ndala 'A' Manispaa ya Shinyanga mkoani hapa, anadaiwa kujinyonga kwa kutumia kamba aliyoitundika nyuma ya mlango nyumbani kwao Mtaa wa Mwabundu, Kata ya Ndala.

Mama mkubwa wa mwanafunzi huyo, Joyce Kalulu alisema jana kuwa tukio hilo lilitokea Jumatano asubuhi na kwamba mtoto huyo hakuwa na tatizo lolote.

Alisema siku ya tukio, baada ya kunywa chai alitoka na kuelekea kwenye shughuli zake na aliporejea, alikuta mlango umefungwa.

"Wakati ninaondoka nilimwacha akiwa na bibi yake, baada ya kurejea nyumbani saa nane mchana, nikaukuta mlango umefungwa kwa ndani. Nilijaribu kumwita ili afungue bila mafanikio, tulipovunja mlango tukakuta kijana wetu amejinyonga," alidai.

Kalulu alisema kuwa kabla ya kuvunja mlango, walimwita Mwenyekiti wa Mtaa huo, Pili Masanja ambaye alifanikiwa kutoboa nyavu za dirisha na kumwona Brayton akining'inia mlangoni.

Mwenyekiti Masanja alisema taarifa za tukio hilo alipokea saa tisa alasiri na baada ya kufika eneo la tukio, walitoboa wavu wa dirisha na kumwona mwanafunzi huyo akiwa amejinyonga nyuma ya mlango kwa kutumia kamba ya rangi nyeusi, ndipo walipotoa taarifa polisi.

Kamanda wa Polisi Mkoa Shinyanga, Janeth Magomi alithibitisha kutokea kwa tukio hilo na kubainisha kuwa walikuwa wanaendelea na uchunguzi zaidi wa tukio hilo.

# Wanafunzi watumia maji pamoja na mifugo

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

UHABA wa maji umesababisha wanafunzi wa Shule ya Sekondari Wanging'ombe, Halmashauri ya Wanging'ombe mkoani Njombe kutumia maji pamoja na mifugo.

Diwani wa Wanging'ombe, Geofrey Nyagawa alibainisha hayo juzi wakati akichangia hoja kwenye kikao cha Baraza la Madiwani la Halmashauri hiyo.

Nyagawa alisema, hali hiyo inatokana na shida katika upatikanaji wa maji, akitamka: "Tumejaribu kuongea na WANGIWASA (Mamlaka ya Maji Wanging'ombe) na RUWASA (Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini), ili waone wanatatuaje changamoto hii lakini kwa sasa wanafunzi wanazagaa.

"Pale kuna bwawa jirani ambalo mifugo wanatumia na wanafunzi nao wanakwenda wanatumia hilo bwawa kwa sababu ndipo pekee panapopatikana maji."

Nyagawa alisema kuwa pamoja na kwamba mpaka sasa hakujatokea mlipuko wa magonjwa, hatua za haraka zinapaswa kuchukuliwa.

Alisema RUWASA wamechimba kisima ambacho hakijajengwa ili kutoa maji.

Meneja RUWASA Wilaya ya Wanging'ombe, Charles Mengo alisema wameshatia saini mkataba wa kusambaza maji, wakitarajia kuingiza maji shuleni huko wakati wakiendelea na ujenzi wa tangi kubwa la lita 150,000 kwenye mnara wa mita sita.

"Mwenyekiti tunatambua tatizo lililopo pale na ndiyo maana tukaweka bajeti ili kusaidia eneo hilo. Kwa hiyo, kwa maelezo hayo nimhakikishie mheshimiwa diwani kwamba kuanzia sasa tutaanza huo ujenzi," alisema.

# Ofisa mtendaji kukatwa mshahara miaka mitatu

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

HALMASHAURI ya Wilaya ya Wanging'ombe mkoani humo imeagiza kukatwa mshahara asilimia 15 kila mwezi kwa muda wa miaka mitatu, Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Masage, Kata ya Kidugala, Zuru Nyato baada ya kubainika kughushi nyaraka za serikali na kusababisha hasara.

Akizungumza baada ya kikao cha uamuzi wa baraza, Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Agnetha Mpangile alisema kosa hilo ni kinyume cha kanuni 42 Jedwali la 1 sehemu A(1) ya Kanuni ya Utumishi wa Umma ya Mwaka 2003, ikisomwa pamoja na kanuni D.12 na Kanuni F27(1)(a) ya Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma toleo la mwaka 2009.

Mpangile alisema, watumishi wengine watatu waliokuwa na masuala ya kinidhamu, baraza limeagiza wapewe adhabu ya karipio kali la maandishi.

Alisema watumishi wanapaswa kuwa na maadili ya kazi na kufuata mwongozo na nidhamu pamoja na taratibu za kiutumishi.

"Kufanya udanganyifu kwenye mambo ya fedha sio uadilifu na wala sio utumishi, hivyo ninawaasa watumishi wote, hawa ni mfano lakini kama kuna tabia ambazo zipo katikati ya watumishi wetu, basi wanatakiwa waache mara moja na kufanya kazi kwa uadilifu, vinginevyo hawa tungewachukulia hatua kubwa. Kwanza wamemdanganya mwajiri wao na halmashauri," alionya.

Diwani wa Itulaumba, Thobias Mkane alisema watumishi wa umma wanapaswa kushirikiana kulinda fedha za serikali na michango ili kuleta tija kwa wananchi Inaelezwa kuwa nyaraka zilizoghushiwa ni za michango ya wananchi kwa ajili ya ujenzi wa zahanati ya kijiji baada ya mtendaji huyo kutakiwa kurejesha kwenye akaunti fedha hizo.

RIPOTI MAALUM

# HALI MBAYA MTERA

## ■Mabadiliko tabianchi chanzo bwawa kukosa samaki
## ■Wanawake watelekezewa familia, DED afunguka

**Na Augusta Njoji, aliyekuwa**
MPWAPWA



Wauzaji wa samaki geti la Mtera wakinadi bidhaa zao kwa wateja kwenye barabara ya Iringa-Dodoma. Samaki wanaouzwa katika eneo hilo kwa sasa wanatoka Tabora kutokana na uhaba wa samaki kwenye Bwawa la Mtera. **PICHA: AUGUSTA NJOJI**

"HALI ya kimaisha hapa kwetu ni ngumu. Nina familia ya watu tisa, nikimpigia simu mume wangu huko aliko nako anasema 'hali ni ngumu, mnachopata mridhike nacho'," Happy Sanga, mkazi wa Kijiji cha Chungu, Kata ya Mtera wilayani Mpwapwa anasimulia kinachojiri katika makazi yao.

Happy anayeishi na watoto wake sita na wajukuu wawili kijijini huko, anasema kinachowasibu ni matokeo ya mabadiliko ya tabianchi yaliyoathiri Bwawa la Mtera lililokuwa tegemeo kwa wakazi wa eneo hilo katika upatikanaji wa samaki.

"Mume wangu aliondoka hapa (kijijini Chungu) miaka miwili iliyopita, aliniaga anakwenda kwenye shughuli za uvuvi Singida. Upatikanaji wa huduma hapa nyumbani umekuwa mgumu, hata tukimpigia simu anasema hali ngumu.

"Kwa sasa hatuna msaada wa aina yeyote. Hata ukisema ukate kuni, hakuna mnunuzi, hadi mume akufikirie huko aliko baada ya mwezi mzima au wiki tatu anakutumia Sh. 10,000," Happy anasimulia kinachowasibu.

Ni madhila ambayo pia yanamkabili mchuuzi wa samaki, Agatha Mawanja anayebainisha kuwa wanaume wengi wanaojishughulisha na uvuvi ambayo ndio shughuli kuu kwa wakazi wa eneo hilo, wamelikimbia Bwawa la Mtera kutokana na kukosa samaki.

Anasema uamuzi huo wa wanaume umesababisha wanawake wengi kuchukua majukumu ya wakuu wa kaya, wakifanya anachokiita kuhangaika huku na kule kuhakikisha wanalea familia.

Agatha anabainisha kuwa huu ni mwaka wa nne mfululizo bwawa hilo limekumbwa na ukosefu wa samaki uliochangiwa na athari za mabadiliko ya tabianchi, wavuvi wakilazimika kutelekeza familia zao kwenda kwenye maeneo mengine ya mbali yenye samaki.

Nipashe imetembelea maeneo ya kambi za wavuvi za Mapera Mengi, Chadumbwi, Chungu wilayani Mpwapwa na kushuhudia makazi ya wavuvi na wachuuzi wa samaki yakitawaliwa na jinsia ya kike na watoto.

Mchuuzi wa samaki Agatha anasema ukosefu wa samaki kwenye bwawa hilo umeathiri uchumi wao, baadhi ya wazazi wakilazimika kuwaacha watoto wakajilee na kusababisha mahudhurio hafifu shuleni.

"Waume zetu ambao kwa asilimia kubwa ni wavuvi, wametukimbia na mitaji yetu kwa sasa imeyumba, hatuna fedha ya kumudu biashara ya samaki wanaoletwa hapa Mpwapwa kutoka Tabora.

"Tunaishi kwa kukopa samaki kwa wafanyabiashara wanaotuletea samaki hapa. Tunachokifanya tukichukua samaki, tukishauza tunapeleka kulipa. Kama hujapata soko la samaki, hawezi kukupa samaki tena maana huna mtaji," Agatha anafafanua.

Anabainisha kuwa wako wanawake 98 katika eneo hilo wanaojishugulisha na uuzaji wa samaki lakini kwa sasa hawana mitaji na ndio sababu ya kugeukia maisha mapya ya kukopa samaki kwa wafanyabiashara.

"Ukiwa na mtaji una uhakika wa kufanya biashara badala ya kutegemea mkopo, yaani nikiwa na mtaji wa kilo 20 za samaki, ninaweza kujiendesha badala ya kukopakopa kwa mtu," Agatha anasema.

Elizabeth Nyauringo, mkazi wa Mtera anayehudumia familia ya watoto 10, anawasilisha kilio chake kwamba huu ni mwaka wa nne mumewe hajarejea nyumbani na wakimpigia simu, mrejesho wake ni hali ngumu kimaisha inayomkabili katika shughuli zake za uvuvi.

"Tumekuwa tukihangaika kutafuta vibarua kwa matajiri wa ng'ombe ili kupata chakula cha familia. Kwa sasa hapa kwangu tunakula mlo mmoja kwa siku, tunaomba serikali itafute ufumbuzi, hili bwawa limekosa samaki, limesababisha waume zetu kutelekeza familia," Elizabeth anasema.

Halima Punyee, mama wa watoto saba na mkazi wa Mtera, anakiri mume wake anafanya anachokiita kutangatanga kwenye mabwawa pasi na kutoa huduma stahiki kwa familia.

"Hapa nina watoto wanasoma sekondari, mmoja ambaye anasoma shule ya bweni amerudishwa kutokana na kutolipa fedha.

"Kuna wakati ninalazimika kukata kuni na kuuza maji mtaani ili nipate Sh. 70,000 kwa ajili ya malipo ya kila mwezi ya watoto wangu wawili wa shule hiyo ya bweni, hapo bado matumizi yao mengine shuleni.

"Hali inapokuwa ngumu zaidi ninalazimika kuuza vitu vya ndani ya nyumba ili kupata fedha za kuhudumia watoto," Halima anasimulia kinachojiri.

Mwenyekiti wa Wauza Samaki Mtera, Selina Ndahani, anarejea historia yao kibiashara, akibainisha kuwa awali walikuwa wanapata samaki kwa Sh. 3,500 kwa kilo katika bwawa hilo lakini sasa kilo moja ya samaki wanaotoka mkoani Tabora inauzwa kwa Sh. 7,500, ikiwa ni zaidi ya mara mbili ya bei ya samaki waliokuwa wanapatikana Mtera.

"Hata mitaji ya kufanya hiyo biashara hakuna, kinachofanyika sasa wenye mitaji wanakwenda kufuata huko samaki waliko na kutuletea kutukopesha. Ukipima kilo 10 pamoja na mafuta inafika gharama Sh. 83,000, ukiuza unapata Sh. 90,000, watoto wanapata kula hiyo faida ya Sh. 7,000.

"Awali maisha yetu yalikuwa nafuu, tulipoanza kukosa samaki kwenye Bwawa la Mtera, hali ikawa mbaya kama unavyoona hapa.

"Uchumi kwa ujumla ni mbovu, tumelima lakini hatujafanikiwa kuvuna, mvua ilikuwa ndogo, samaki nao hakuna, kinamama wametoka majumbani kuhangaika kupata chochote," Selina anasema.

Rai yake kwa serikali ni kuinusuru jamii ya Mtera kwa kuiwezesha mikopo kwa wajasiriamali wanaojishughulisha na biashara ya samaki, ili kumudu kufanya biashara hiyo.

"Sisi Mtera hatujawahi kupata mikopo ya wanawake, hatujawahi kufikiwa na mikopo hiyo hata mara moja. Wafanyabishara wakubwa wa samaki ndiyo wanatukopesha samaki.

"Kwa sasa ninapata faida ya wastani wa Sh. 5,000 hadi 6,000. Inabidi kuchangiana na wenzangu tuna michezo ya upatu unatoa Sh. 1,000 kwa siku ili mtu apate kiroba cha unga wa ugali, familia zipate chakula," anasema.

Selina anabainisha kuwa kwa sasa wafanyabiashara wenye mitaji kwenye eneo lao ni watatu ambao huleta samaki kutoka maeneo wanakopatikana na kuwakopesha wanawake hao wachuuzi.

**WANAUME WAKIRI**

Mkazi wa Mtera na mfanyabiashara wa samaki, Amon Kodi anakiri wanaume wavuvi kutelekeza familia zao kutokana na hali mbaya kiuchumi baada ya Bwawa la Mtera kukosa samaki.

Anasema hali ya upatikanaji wa samaki ni mbaya, akibainisha kuwa huu ni mwaka wa tano bwawa hilo halina samaki wengi na mwaka huu hali imezidi kuwa mbaya zaidi.

"Upatikanaji wa samaki kwa sasa ni shida, hata ungekuwa na nyavu 1,000 ukazitega unaweza usitoke hata na samaki mmoja, yaani ni kama umetega nchi kavu, wataalamu hawajatuambia kiini cha tatizo.

"Hali ya uchumi hapa Mtera ni mbaya hasa kwa watu wanaotegemea uvuvi. Hadi sasa wavuvi wa Bwawa la Mtera kwa kiwango kikubwa hawapo, hata ukipita kambini utakuta wanawake na watoto tu.

"Wavuvi wengi wamehamia Tabora, Manyara na Bahi, ndiko wengi wamekwenda kusaka samaki huko, hawa samaki wanaopatikana hapa kwa sasa wanatoka kwenye maeneo hayo," Kodi anabainisha na kuwashauri wavuvi wakumbuke familia zao na kuzipa huduma stahiki hata kama wako mbali.

Mvuvi Richard Nkondola anarejea uzoefu wake kazini, akikiri upatikanaji wa samaki kwenye bwawa hilo kwa sasa umekuwa mgumu kulinganishwa na miaka ya nyuma.

"Unajua awali mtumbwi kama huu mdogo ulikuwa unaweza kuleta kilo 30 hadi 40 lakini kwa sasa ukibahatika sana ni kilo tatu na wakati mwingine hakuna kabisa.

"Hapa Chungu wavuvi wengi wameondoka, waliobaki hawazidi 10, wavuvi wasiojiweza wamebaki kambini, kazi yao sasa ni kuchota na kuuza maji," Ndokola anasema.

●ITAENDELEA KESHO

# Mtoto adaiwa kunyongwa akiwa machungani

**Na Neema Hussein,**
MPANDA

MTOTO aliyefahamika kwa jina la Ntemi Ndamo (10) anadaiwa kunyongwa hadi kufa na watu wasiojulikana akiwa anachunga ng'ombe.

Katika tukio hilo lililotokea Oktoba 25, mwaka huu, katika kijiji cha kasekese wilayani Mpanda mkoani Katavi, watu waliohusika na tukio hilo, baada ya kukamilisha kitendo hicho, waliondoka na mifugo aliyokuwa akichunga mtoto huyo.

Nipashe ilifika katika familia iliyokumbwa na mkasa huo na kuzungumza na baba mkubwa wa marehemu, Shefa Luhende, ambaye alisema mtoto huyo aliondoka nyumbani asubuhi akiwa na ng'ombe 11, majike yakiwa sita na maksai watano kwenda malishoni.

Alisema baada ya kuona muda umeenda na mtoto harudi nyumbani, ndipo walipochukua jukumu la kutoa taarifa kwa uongozi wa serikali za mtaa na ndugu, jamaa na marafiki.

"Tulimtafuta mtoto hadi saa 4:00 usiku bila mafanikio. Baada ya muda kidogo yale majike ya ng'ombe yakarudi nyumbani bila mchungaji. Tulisikia wanalia sababu walikuwa wananyonyesha. Ilipofika asubuhi tulikuwa tumepiga simu vijiji jirani kutoa taarifa ya kuibiwa ng'ombe.

"Tulipigiwa simu kuwa kuna ng'ombe wamekamatwa getini wakivushwa kupelekwa kijiji jirani huku anayewaswaga hana kibali, tukaambiwa tukawaangalie kama ni ng'ombe wetu tukakuta ni wenyewe.

"Ikabidi turudi na huyo aliyekuwa akiwaswaga na uongozi wa kijiji akiwamo mwenyekiti pamoja na polisi baada ya yule kuhojiwa akasema walikuwa watatu. Tulipomuuliza kuhusu mchungaji akasema twende atupeleke tulipofika tukakuta mwili wakiwa tayari wamemuua," alisema Luhende.

Baadhi ya majirani, akiwamo Elizabeth Aloyce, walisema wameshtushwa na tukio hilo, hivyo wameiomba serikali kukamilisha haraka ujenzi wa kituo cha polisi katika kijiji hicho na kuongezewa polisi kwa ajili ya usalama wao na mali zao.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Kasekese, Simon Sungwa, alisema wahalifu hao kwa sasa wamebuni njia nyingine ya kuiba mifugo tofauti na mwanzo walipokuwa wakiiba mifugo usiku ikiwa kwenye zizi.

Alisema kifo cha mtoto huo kimewashtua huku akiwataka wazazi kuacha tabia ya kutuma watoto kupeleka mifugo malishoni ambao hawana uwezo wa kupambana na wahalifu.

"Yaani inasikitisha sana yule mtoto kule tulikoenda kuonyeshwa yaani wamemuua wakamtupa kwenye shimo refu. Hata sisi wenyewe tumemtoa kwa kamba, sijui waliingia vipi kule wakaenda kumfunika na majani kwa juu hata hao wauaji wenyewe ni vijana tu. Angekuwa huyo mtoto ni mtu mzima, angepambana nao labda angefanikiwa kujiokoa," alisema.

Emmanuel Tinda, Ofisa Uhusiano wa Hospitali ya Rufani Mkoa wa Katavi, alikiri kuupokea mwili wa mtoto huyo kutoka Jeshi la polisi ukiwa na majeraha shingoni na baada ya kuufanyia uchunguzi, waligundua shingo ilikuwa imevunjika.

# Wanaume washauriwa kupima tezi dume

**Na Joseph Mwendapole**

WANAUME wenye umri wa kuanzia miaka 40 na kuendelea wameshauriwa kujenga utamaduni wa kupima saratani ya tezi dume mara kwa mara ili wanaobainika kuwa na matatizo wapate matibabu mapema.

Mkurugenzi wa Hospitali ya KAM Musika iliyoko Kimara Korogwe, Dar es Salaam, Dk. Kandore Musika, alisema hayo jana wakati hospitali hiyo ilipoandaa kambi ya upimaji bure wanaume dalili za tezi dume.

Alisema iwapo mtu atabainika mapema kuwa na dalili za saratani ya tezi dume, inakuwa rahisi kwake kupata matibabu na kupona kuliko kusubiri mpaka saratani ifikia hatua mbaya.

Dk. Musika alisema wameamua kuandaa kambi hiyo ya bure ya siku moja kuwapa fursa wananchi wa maeneo ya Kimara kupima saratani ya tezi dume na wale watakaobainika kuwa na tatizo hilo waanzishiwe matibabu mapema.

"Ugonjwa wa saratani ya tezi dume unawashambulia sana wanaume wenye miaka kuanzia 40 na kuendelea na hospitali ya KAM imeamua huduma hii bure kama shukrani kwa jamii inayotuzunguka," alisema Dk. Musika.

Alisema wanaume wengi hawana uelewa kuhusu saratani ya tezi dume, hivyo wamelazimika kuwaelimisha kuhusu dalili zake ili kuwahi hospitalini watakapoziona.

Mamia ya wanaume waliojitokeza kwenye kambi hiyo, alisema wamepewa somo la kutosha kuhusu dalili za ugonjwa huo na wameahidi kwenda kuelimisha wenzao.

"Mtu mwenye saratani ya tezi dume akichelewa akikaa nayo muda mrefu, matokeo yake inasambaa mwili mzima na kushambulia kila sehemu kwa hiyo kupima mara kwa mara si jambo la kupuuza kwa wanaume watu wazima," alisema.

Alisema wameanza kutoa huduma hiyo bure mwaka huu na wamepanga kuhakikisha huduma hiyo inatolewa kila mwaka ili kusaidia kubaini wanaume wenye shida kama hiyo.

Alisema saratani ya tezi dume inapimwa kwa njia tatu ikiwemo ya kutoa damu, 'utra sound' na njia ya kidole lakini wameamua kutumia njia ya damu ambayo wanaume wengi wanaipendelea. "Hatutaishia kupima saratani ya tezi dume tu tutafanya utaratibu wa kupima bure saratani ya matiti na saratani ya shingo ya kizazi kwa wanawake kama sehemu ya kutoa shukrani kwa jamii tunayoihudumia," alisema Dk. Musika.


TRA

TANZANIA REVENUE AUTHORITY

ISO 9001: 2015 CERTIFIED

CUSTOMS AND EXCISE DEPARTMENT

PUBLIC NOTICE

New Customs Agency Licenses for Year 2023

Notice of Extension of Time to Submit Applications

Notice is hereby given to the General Public that, Commissioner for Customs and Excise has extended the time for submission of applications for new Customs Agency Licenses for year 2023. The application window will be open from 31st October, 2022 to 07th November, 2022.

All applicants who wishes to apply for new Customs Agent's Licenses are advised to take advantage of the extended period to submit their applications.

"Together We Build Our Nation"

Said Athumani

Commissioner for Customs and Excise

017123501

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kila la kheri Simba Queens Ligi ya mabingwa Afrika

**MICHUANO** ya soka la Ligi ya mabingwa Afrika kwa Wanawake inatarajia kuanza kesho Jumapili jiji Rabat nchini Morocco.

Michuano hiyo inashirikisha klabu za soka za Wanawake ikiwa ni mara ya pili tangu kuanzishwa kwake. Mara ya kwanza ilifanyika nchini Misri mwaka jana na klabu ya Mamelodi Sundowns ya Afrika Kusini ndio iliibuka kuwa mabingwa.

Simba Queens imepangwa katika Kundi A na itafungua pazia la mashindano haya Jumapili kwa kuwavaa wenyeji ASFAR Queens mchezo utaanza majira ya saa 4:00 usiku kwa saa za Tanzania.

Kikosi cha Simba Queens kilitua salama jijini Rabat mapema wiki hii tayari kwa ajili ya kushiriki mashindano hayo na Meneja wa timu hiyo, Selemani Makanya, alisema wachezaji wote wako katika hali nzuri na wanasubiri kuanza kupeperusha vyema bendera ya klabu na Tanzania.

Kwa mujibu wa Makanya kikosi kilianza mazoezi juzi usiku na wanashukuru hali ya hewa kwa sasa jijini humo ni nzuri na inafanana na ile ya Dar es Salaam.

Meneja huyo aliongeza anafurahi kuona kila mchezaji aliyesafiri kwenda huko anashauku kubwa ya kutimiza kile ambacho mashabiki, wanachama na viongozi wa Simba wanachokisubiri.

Naye Ofisa Habari wa Simba, Ally Shatry 'Chicco' alisema kwa upande wa utawala maandalizi yote kuelekea mashindano haya yamekamilika na wamejipanga vizuri.

Tukiwa kama wadau wakubwa wa michezo hasa soka, tunachukua nafasi hii kuitakia kila la kheri Simba Queens katika mashindano hayo ambapo ni moja ya sehemu ya kuitangaza tanzania kupitia mchezo huo duniani kote.

Tuna imani na wachezaji hawa wanawake kwamba wanaweza kufanya vizuri na hata kulibeba taji la michuano na kutua nalo Tanzania kwa mara ya kwanza katika historia yake.

Wakati tukiwa na kumbukumbu nzuri ya timu ya nchini India, basi tuna matumaini makubwa kwa Simba Queens.

Ikumbukwe baadhi ya wachezaji hao wa Serengeti Girls wapo katika kikosi cha Simba Queen, tunaamini watatumia vizuri zaidi uzoefu walioupata kwenye michuano ya kombe la dunia kwa kushirikiana na wachezaji wenzao kufanya vizuri.

Serengeti Girls ilifanikiwa kufika robo fainali ya mashindano hayo, huku ikiwafunga wababe wa Dunia Ufaransa katika kinyang'aniro hicho.

Hivyo, Nipashe tunaamini kabisa kwamba, Simba Queens wanaweza kuiga mafanikio waliyoyapata Serengeti Girls na kufika mbali zaidi katika mashindano haya ya Klabu bingwa Afrika.

Wito wetu kwa benchi la ufundi ni kuhakikisha wanawapa mbinu za kutosha wachezaji hao ili kuhakikisha kwamba, wanafanya vizuri zaidi kama sio kulibeba taji hilo.


Kwa upande wa wachezaji, tunaamini watatumia vizuri maelekezo ya benchi la ufundi chini ya kocha mkuu kuhakikisha wanacheza kwa bidii na maarifa ili kuibuka na ushindi katika kila mchezo.

Kufanya vizuri kwa Simba Queens kwenye mashindano hayo tutaipa nafasi nzuri zaidi Tanzania kuendelea kutambulika kisoka duniani na pia kuwapa nafasi nzuri zaidi wachezaji kuonekana kusajiliwa na klabu mbalimbali kubwa duniani.

Taifa ya wanawake chini ya umri wa miaka 17, Serengeri Girls namna ilivyotubeba kwenye michuano ya kombe la Dunia

Tunawatakia kila la kheri Simba Queens.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Simba ilifungwa kabla ya kucheza na Azam

Na Adam Fungamwango

**PAMOJA** na kwamba mpira una matokeo matatu, ushindi, sare na kupoteza, kwenye mechi ya Ligi Kuu iliyochezwa juzi kati ya Azam FC na Simba, soka lingekuwa halitendi haki kama Wekundu wa Msimbazi wangeibuka na ushindi kwenye mechi hiyo.

Simba iliyokuwa na wachezaji waliochezea Azam FC tangu mwaka 2008, leo hii iwaje kucheza dhidi ya timu yao ya zamani miaka 14 baadaye wapate ushindi?

Ukweli ni kwamba makocha wa Simba, Juma Mgunda na Selemani Matola walitengeneza wenyewe mazingira ya kufungwa na hili hawawezi kukwepa lawama kwa wanachama na mashabiki wa timu yao ambao wameonekana kulalamika sana baada ya mechi hiyo.

Haikuingia akilini makocha kumpanga Erasto Nyoni kucheza kama beki wa pembeni dhidi ya mawinga wa Azam wenye kasi na wajanja.

Kama makocha wa Simba wangeangalia mechi ya Azam dhidi ya Yanga jinsi mawinga wa Azam walivyowachachafya mabeki wa pembeni wa timu hiyo, sidhani kama wangethubutu kufanya hivyo.

Kama mabeki wa pembeni wa Yanga kina Kibwana Shomari, Farid Mussa, na Djuma Shaaban ambao kwa sasa ni bora sana kwenye Ligi Kuu ya Tanzania walipata taabu na 'kulala na viatu' dhidi ya kina Kipre Junior, Ayoub Lyanga, unawezaje kumweka Nyoni kukabiliana na mawinga hao? Hapa ndipo nasema kuwa Simba ilifungwa kabla hata mechi hiyo kuanza.

Kwanza kabisa, picha inaanza. Haikuwa na viungo wao ambao wamekuwa tegemeo kwa sasa, Mzamiru Yassin na Sadio Kanoute na hilo likawa pengo kubwa kwenye mechi hiyo. Inakuwaje tena kuwapa mzigo mwingine wachezaji kuwaongeza mtu ambaye kwa sasa umri umekwenda na hawafai tena kwenye mechi ya ushindani kama ile?

Ilikuwa kama kuchezea shilingi kwenye choo. Kwa timu yoyote ambayo inasaka ubingwa, sifa ya kwanza ni kupata pointi tatu au moja kwa timu ambazo inagombania nazo ubingwa.

Makocha wanaojua hivyo, sidhani kama wangecheza mchezo wa hatari kama huo kumuweka Nyoni ambaye pamoja na umri, amekuwa hana tena kasi, wala uamuzi sahihi mbele ya winga hatari kama Kipre. Kama amekuwa wa haaminiki hata kwenye mechi dhidi ya Ihefu, inakuwaje kwenye mechi dhidi ya Azam?

Watetezi wanaweza kusema mabeki wa kulia wote ni majeruhi ambao ni Shomari Kapombe ambaye ingawa amerejea bado hana utimamu wa mwili na mwingine ni Israel Mwenda. Lakini kama makocha wangekuwa makini, wangeweza kumchezesha Keneddy Juma kati na Henock Inonga angeachwa kucheza namba mbili.

Ukiangalia kwenye mechi ya juzi ni kwamba Inonga alikuwa akicheza zaidi kulia akimsaidia Nyoni kuliko kwenye namba yake ya asili. Sasa unajiuliza kwa nini kati pale asingekaa Kennedy kwa sababu hata huyo Nyoni mwenyewe hakuonekana kama anacheza beki wa kulia licha ya kuonekana yupo. Hakuweza kuzuia, wala kupandisha mashambulizi mbele. Na cha ajabu alicheza dakika zote 90.

Nilichogundua kwenye mechi hiyo pia kuwa Simba inatakiwa kusajili kiungo mkabaji mwenye kiwango cha juu cha kimataifa kama kweli inataka kupambana kwenye Ligi Mabingwa Afrika.

Hata hawa kina Mzamiru na Kanoute ni msimu huu tu ambao wamekuwa kwenye kiwango kizuri, lakini msimu uliopita nao pia walikuwa wanapigiwa kelele.

Kwa viongozi wa Simba itoshe tu kusema wafanye uamuzi mgumu kwani wakiendelea kuwa na kina Nyoni, Bocco na viungo wakabaji ambao hawafanyi kazi ipasavyo wanakuwa wanajipiga kisu mgongoni.

Wachezaji hawa wameifanyia makubwa kwa kuipa ubingwa mara nne mfululizo, lakini kwa walipofikia inatosha na viongozi wasitake kuwafanya mpaka wachezaji hao wanazomewa ndiyo wawaondoe.

Kwa timu kubwa kama Simba inayotaka mafanikio kwenye michuano ya kimataifa, haina kikosi kipana kwenye viwango vya kimataifa, badala yake wachezaji wawili tu wakiwa majeruhi basi wanaoingia ni wale waliocheza Ligi Kuu tangu katikati ya miaka ya 2000.

# Kelele za wahudumu zasimamisha kwa muda usikilizwaji kesi mauaji

**Na Grace Gurisha**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, juzi ilisimama kwa muda kuendelea na usikilizwaji wa kesi ya mauaji katika chumba cha wazi baada ya kutokea ugomvi wa wahudumu wa mgahawa wa chakula na kusababisha kelele.

Hali hiyo ilitokea juzi saa 9:00 alasiri mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu Joseph Luambano wakati Daktari wa Hospitali ya Vijibweni, Kigamboni, Dk Said Mkwachu, akitoa ushahidi dhidi ya John Magembe na Mussa Titto wanaotuhumiwa kumuua Julius Kazoshi.

Mkwachu alikuwa akiulizwa maswali na mawakili wa utetezi, Francis Munuo na Khard Muhidini, lakini kutokana na kelele kuzidi kuingia ndani ya chumba hicho, Hakimu Lwambano alimwagiza askari akawalete wahudumu hao ambao walikuwa wakipigana.

Askari huyo aliwaleta wahudumu hao wa chakula ambao walikuwa wadada na Hakimu aliwauliza kama wao ni watumishi wa werikali, wakamjibu ndiyo

Lwambano aliwauliza tena kama wanazifahamu sheria za mahakama na wakamjibu wanazifahamu. Pia aliwauliza kuwa walivyofika walielekezwa utaratibu wa mahakama? Wakamjibu ndiyo.

Hakimu aliwauliza mawakili wa pande zote kama anawaonea na wakamjibu kwamba hawaonei. Pia akawauliza sheria inasemaje na wakamjibu wakipatikana na hatia ni kifungo cha miezi sita jela.

"Mtu yeyote akipiga kilele wakati kesi inaendelea naye anashtakiwa kuwa anapiga kelele. Watu wa aina hiyo wanajieleza kidogo halafu wanahukumiwa," alisema Lwambano.

Hakimu huyo aliwauliza sababu ya wao kupigana na wakashindwa kumjibu chochote lakini wakaomba awasamehe na hawatarudia tena. Msamaha wao ulikubaliwa na wakaamuriwa kutoka mahakamani.

Awali, Dk. Mkwachu alidai kuwa wakati akifanya uchunguzi wa mwili wa marehemu, aliona jeraha upande wa kushoto wa kifua chake na akafanya uchunguzi zaidi akakuta moyo umejeruhiwa.

Alidai marehemu aliuwawa kutokana na umwagikaji wa damu nyingi baada ya kuchomwa na kitu chenye ncha kali. Aliomba mahakama ipokee ripoti ya uchunguzi kama kielelezo kwenye kesi hiyo na mahakama ilipokea.

Washtakiwa wanadaiwa kumuua Julius Septemba 14, 2017 eneo la Vijibweni ndani ya wilaya ya Kigamboni, Dar es Salaam.



Mkurugenzi wa Bodi ya Sukari Tanzania Kenneth Bengesi (wa pili kushoto), akimkaribisha Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Fatma Mwasa (kushoto) katika banda la Kampuni ya Sukari ya Kilombero kwenye (KSC), katika maonesho ya Wakulima wa Miwa Kilombero katika kijiji cha Ruaha wilayani Kilosa, mkoani Morogoro mapema wiki hii. Wengine ni viongozi wa kampuni hiyo, Mkuu wa Kitengo cha Wakulima wa Nje, Pierre Redinger (kulia), Mkuu wa Idara ya Mahusiano, Ephraim Mafuru (wa pili kulia) na (wa tatu kulia) ni Mkurugenzi Mtendaji Guy Williams. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Waziri ataka maeneo ya hifadhi yanayomegwa yapatiwe hatimiliki

**Na Munir Shemweta,** NJOMBE

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, ametaka maeneo yanayomegwa kwa ajili ya kupatiwa wananchi waliovamia hifadhi yapangiwe mpango wa matumizi ya ardhi na kutolewa hati kwa wamiliki.

Dk. Mabula alitoa agizo hilo juzi katika kijiji cha Mpanga, Wanging'ombe Njombe wakati timu ya mawaziri wanane wa wizara za kisekta inayoshughulikia migogoro ya matumizi ya ardhi katika vijiji 975 ilipotembelea mkoa wa Njombe ikiwa ni mfululizo wa ziara zake kwenye mikoa ya Tanzania Bara.

Mpanga ni moja ya vijiji 11 vilivyoko wilaya za Wanging'ombe na Makete mkoani Njombe ambavyo vimemegewa eneo kutoka hifadhi ya Pori la Akiba la Mpanga Kipengele.

Dk. Mabula alisema, serikali imeridhia baadhi ya vijiji kwenye mkoa wa Njombe kubaki maeneo ya hifadhi za mapori ya akiba ingawa wananchi wake waliingia bila ridhaa ya serikali.

Kwa mujibu wa Dk. Mabula, ili kuondokana na migogoro ya ardhi, vijiji vilivyomegewa maeneo vitapimwa na kumilikishwa ili wamiliki kujua mipaka sambamba na kutumia hati kukopa fedha benki na fedha kutumika kuboresha shamba au mifugo.


"Kinachofanyika hapa si tu kutoa maeneo. Eneo linatolewa lakini liwekewe mpango mzuri na endelevu ili kuona jinsi gani mnaweza kutumia ardhi mliyopewa kwa faida na kwa sababu tunaongezeka, basi mpango uwe mzuri na endelevu," alisema Dk. Mabula.

Alibainisha kuwa ni lazima maeneo yanayopangwa yaanishwe matumizi yake kama vile maeneo ya akiba, hifadhi, makazi na uwekezaji na kutaka wakati wa utekelezaji wataalamu wazingatie mpango wa matumizi katika maeneo hayo.

Timu ya Mawaziri Wanane wa Wizara za Kisekta ambayo inashughulikia migogoro ya matumizi ya ardhi kwenye vijiji 975 imemaliza ziara yake katika mkoa wa Njombe ukiwa ni mkoa wa 22 kati ya 26 ya Tanzania Bara na inaendelea na ziara yake katika mkoa wa Ruvuma.

## KABWELA

**Fadhili Mohamed**



# Wataka mikopo elimu ya juu inufaishe wengi

**Na Joseph Mwendapole**

KAMATI ya Makamu Wakuu wa Vyuo Vikuu nchini (CVCPT) imeishauri serikali kupanua wigo wa kutoa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu ili kuwezesha wanafunzi wengi wanaohitaji kujiunga na vyuo vikuu kupata nafasi.

Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Prof. Yohana Mashalla, alitoa rai hiyo jana wakati wa mkutano wa 30 wa kamati hiyo uliofanyika jijini Dar es Salaam.

Alisema idadi ya wanafunzi wanaohitimu sekondari imekuwa kubwa, hivyo kusababisha wanafunzi wengi kushindwa kujiunga na vyuo vikuu kutokana na hali ya umaskini kwenye familia zao.

Alisema miaka ya hivi karibuni serikali iliongeza idadi kubwa ya shule za msingi na sekondari na kutoa elimu bila malipo, hali inayosababisha ongezeko la wanafunzi wengi wanaomaliza shule ya msingi na sekondari na kuhitaji kujiunga na vyuo vikuu mbalimbali nchini.

"Vyuo vikuu navyo vitapata shida ya upungufu wa miundombinu, hivyo kulazimika kuongeza idadi ya madarasa, maabara na maktaba ili kukidhi mahitaji ya idadi ya wanafunzi. Kwa hiyo, Bodi ya Mikopo ipendekeze kwa serikali namna nzuri ya kuongeza wigo wa utoaji wa mikopo," alisema Prof. Yohana.

Prof. Mashalla pia aliishauri serikali kuvisaidia kifedha vyuo vikuu nchini kupata uwezo wa kuweka miundombinu ya kuchukua idadi kubwa ya wanafunzi, hali itakayosaidia kuongeza idadi ya wanafunzi wanaodahiliwa kwenye vyuo vikuu mbalimbali nchini.

Prof. Costa Mahalu, Makamu Mkuu wa Chuo cha Mtakatifu Augustine, alisema vyuo vikuu binafsi vina vinakabiliwa na vikwazo vingi kulinganisha na vyuo vya umma kwa kuwa vinategemea kujiendesha kwa kukusanya ada kutoka kwa wanafunzi.

Alisema idadi ya wanafunzi wanaopata mikopo ya elimu ya juu ni ndogo na kwa wale wanaobahatika kupata wanapata asilimia ndogo, hali inayovifanya vyuo hivyo kuishi maisha magumu kwani vinategemea zaidi ada katika kujiendesha kwake.

"Wanafunzi wanaopata mikopo wakiwa wachache sana inatusumbua sisi kwa kuwa inakuwa shida namna ya kuendesha vyuo, wanafunzi wetu wengi wanatoka kwenye familia ambazo haziko vizuri kifedha, zinategemea zaidi mikopo ya bodi. "Tusipopata wanafunzi wengi sisi wa vyuo binafsi huwa tunaathirika sana kwa sababu hata mishahara ya kuwalipa watumishi inakuwa shida kubwa kwetu lakini wenzetu wa vyuo vya serikali hawana shida kwa sababu mishahara yao yote inatoka serikalini," alisema Prof. Mahalu.

Aliongeza kuwa kamati yao inahusisha vyuo binafsi na vya umma na lengo lao ni kuishauri serikali namna bora ya kuinua ubora wa elimu ya vyuo vikuu nchini.

Prof. William Anangisye kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), alisema lengo la vyuo vikuu ni kutoa wahitimu ambao watatatua shida mbalimbali kwenye jamii.

Alisema UDSM imekuwa ikipitia mitaala yake kila baada ya miaka mitano kuhakikisha chuo kinakuwa na mitaala bora ili kusaidia chuo hicho kupata wahitimu wenye ubora unaotakiwa na ambao watakidhi mahitaji ya soko.

"Mfano, mwaka huu UDSM inapitia mitaala kwenye vitengo vyake vyote, upitiaji wa mitaala ni muhimu na haukwepeki kwa sababu mabadiliko katika jamii yetu yapo na kila jamii inabadilika kila siku, sasa ni lazima uwe na mitaala inayokwenda sanjari na mahitaji ya wakati huo," alisema Prof. Anangisye.




Mkaguzi Mkuu wa Ndani Benki ya NMB, Benedicto Baragomwa akiwalisha mada kwenye Kongamano la sita la TEHAMA, jijini Zanzibar mapema wiki hii na kuzinduliwa na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ajitolea kupeleka VETA vijana 100

**Na Gurian Adolf,** NKASI

MBUNGE wa Nkasi Kaskazini, Aida Khenan, amejitolea kuwalipia gharama za masomo kwenye Chuo cha Mafunzo ya Ufundi (VETA) wilayani humo vijana 100, ili wapate utaalamu utakaowasaidia kutekeleza miradi ya maendeleo.

Alibainisha hayo juzi wakati wa mkutano wa hadhara uliofanyika mjini Namanyere kwa lengo la kujibu na kuzipatia ufumbuzi kero mbalimbali, ikiwamo ukosefu wa maji ambayo inawakabili wananchi wa jimbo hilo.

Alisema kumekuwa na kasi ndogo katika kukamilisha miradi inayotekelezwa kwa utaratibu wa nguvu kazi ya ndani (force Acoount) kutokana na kutokuwa na mafundi wenye ujuzi katika fani mbalimbali.

Mbunge huyo alisema kwa kuanzia amejitolea kuwalipia vijana 100 ambao ni wahitimu wa darasa la saba na kidato cha nne, ambao watakuwa wako tayari kusoma katika Chuo cha VETA kilichoko wilayani hapo ili mafundi wapatikane wa kutosha.

"Nipo tayari kuwalipia vijana hao gharama zote kwa ajili ya kusoma VETA, ili vijana wajifunze ufundi selemala, ufundi uashi, ufundi bomba pamoja na ufundi wa aina nyingine ili wakatumike kwenye miradi inayotekelezwa wilayani kwetu," alisema.

Kuhusu kero ya maji inayolalamikiwa na wananchi wa Jimbo la Nkasi Kaskazini, mbunge huyo alisema serikali imetoa fedha za dharula Sh. milioni 200 zitakazochimba visima vya majisafi, ili kupunguza kero ya uhaba wa maji wilayani hapo.

Katika mkutano huo, mkazi wa Kitongoji cha Kipundu Kala, Mzee Shilingi alimwomba mbunge huyo kuiwasilisha bungeni kero hiyo, ili serikali iitatue kwa kuwa imekuwa ya muda mrefu tangu kuanzishwa kwa wilaya hiyo.

## REAT yawataka wastaafu kuungana kujenga umoja

**Na Faustine Feliciane**

CHAMA cha Wastaafu Tanzania (REAT) kimewataka wastaafu nchini kuungana kwa ajili ya kuongeza nguvu katika kutatua kero zinazowakabili.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Rais wa chama hicho, Dauda Bilikesi alisema Tanzania ina vyama vingi vya wastaafu vya taasisi na mashirika ya serikali pamoja na sekta binafsi huku akishauri waungane kuimarisha chama hicho ili kutatua kero zilizoko.

"Wastaafu tuna changamoto nyingi, REAT tunatoa wito kwa vyama hivyo vingine kuja kuungana kwenye chama hiki na kuunda shirikisho ambalo litatua changamoto zetu zinazotukabili badala ya sasa kila taasisi kuwa na chama chake cha wastaafu.

"Kwa mfano, Chama cha Wastaafu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (WACHUDA), kipo kile cha Walimu cha (UWAWA) na vipo vingine vya wafanyakazi kama wa Magereza, TANESCO na mashirika mengine, tunatoa wito wote sisi tuungane ili kutetea maslahi yetu," alisema.

Aliongeza kuwa mpaka sasa REAT imefanikiwa kuwa na wanachama 317 na lengo lao kufikisha wanachama 1,300 nchi nzima ifikapo Desemba mwaka huu.

"REAT tuna msemo wetu mkubwa ambao tunahamasishana kutatua changamoto zetu kwa lugha ya kigeni, tunasema "Yes were retired but not tired" kwa tafsiri tunasema 'ndio sisi ni wastaafu lakini hatujachoka', niwaombe wastaafu wenzangu kujiunga na chama hiki ili tuunde shirikisho letu," alisema Bilikesi.

Mwenyekiti wa Bodi ya wadhamini wa chama hicho, Mwalimu Gratian Mukoba, alisema wastaafu kutoka katika vyama vya mashirika wakiujiunga na REAT haitawaondolea haki na uhuru wao wa kuendelea kuwa wanachama wa vyama vyao vya mashirika au taasisi walizokuwa wanazifanyia kazi.

"Ndege wenye rangi moja huruka pamoja, wastaafu wenzangu tuje tuungane tuendelee na harakati zetu za kutetea haki zetu kama wastaafu," alisema Mukoba.

Aliongeza kuwa katika lengo walilojiwekea la kutafuta wanachama, wanataka kuona kila mkoa unakuwa na wanachama angalau 50 (vyama vya taasisi, mashirika au kampuni).

## LATRA yatishia kufuta leseni daladala zinazokatisha safari

**Na Oscar Assenga,** TANGA

MAMLAKA ya Udhibiti wa Usafiri wa Ardhini (LATRA) imewaonya wasafirishaji wa mabasi madogo ya abiria katika Mkoa wa Tanga kuhusu kukatisha safari kwa kuwa kufanya hivyo ni kuwahujumu abiria na kukiuka masharti ya leseni.

Kutokana na kukithiri kwa tatizo hilo, LATRA imetishia kuyafungia leseni mabasi hayo kuanzia sasa ili kukomesha tabia hiyo.

Ofisa Mfawidhi wa LATRA Mkoa wa Tanga, Shedrack Malale alitoa onyo hilo jana wakati alipozungumza na Nipashe kuhusu namna walivyojipanga kudhibiti vitendo hivyo.

"Madereva ni lazima watii sheria za usafirishaji kama ilivyoainishwa wakati wakiomba leseni ili kuwaepusha na malalamiko.

"Katika Jiji la Tanga hivi sasa kumekuwa na vitendo vya ukatishaji wa ruti (safari), hasa kwa mabasi madogo yanayofanya safari zake pembezoni mwa jiji," alisema.

Mabasi madogo yanayolalamikiwa ni yale yanayofanya safari zake katikati ya jiji na pembezoni kupitia Raskazone.

Alisema kitendo cha ukatishaji wa ruti ni makosa na watakaobainika watachukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria zilizopo ili kuwa fundisho kwa wengine wenye tabia za namna hiyo.

"Ndugu zangu madereva niwaase mnapokuwa safarini, acheni ukatishaji ruti kwani kufanya hivyo ni makosa kisheria, hivyo fuateni sheria za usafirishaji mnapokuwa barabarani," alisema Ofisa Mfawidhi wa Latra Mkoa wa Tanga.

Akizungumza kuhusu operesheni ambazo wamekuwa wakifanya katika mkoa huo, Malale alisema kwa sasa wameanza operesheni katika eneo la Segera, Wilaya ya Handeni kwa kufanya ukaguzi wa magari yanayopita ili kudhibiti ajali.

# Auawa akituhumiwa mwizi wa bodaboda

**Na Mary Mosha,** MOSHI

MTU anayedaiwa kuwa jambazi, ameuawa kwa kushambuliwa kwa mawe na wakazi wa Kata ya Mabungo, Wilaya ya Moshi mkoani Kilimanjaro baada ya kutuhumiwa kujaribu kupora pikipiki 'bodaboda', Sh. 30,000 na simu.

Akizungumzia mauaji hayo jana, Kamanda wa Polisi mkoani hapa, Kamishna Msaidizi Simon Maigwa alisema mtuhumiwa huyo aliyeuawa, anadaiwa kufanya tukio hilo Oktoba 26 mwaka huu akitumia silaha aina ya bastola. "Huyu aliyeuawa hajajulikana jina lake lakini alitekeleza tukio hilo akiwa karibu na eneo la Mto Mabungo. Alipouawa na kukaguliwa alikutwa akiwa akiwa na bastola na sime.

"Hilo tukio lilitokea Oktoba 26, majira ya saa moja jioni huko Mabungo, ambako mwendesha pikipiki (hakumtaja jina), alikuwa ametoka shambani kubeba maembe, alipofika kwenye Bonde la Mto huo, alilazimika kushuka na kusukuma mzigo huo, ndipo jambazi aliyeuawa alipomvamia.

"Baada ya kuona ana silaha, mwendesha pikipiki alijisalimisha na kutoa baadhi ya vitu alivyokuwa navyo zikiwamo fedha, simu na pikipiki. Alipomkabidhi vitu hivyo, alifanikiwa kutoroka na kupiga kelele na wananchi walifika na kuanza kumshambulia mtuhumiwa.

"Wakati wananchi wakimshambulia, polisi waliokuwa doria walifika eneo la tukio na kumwokoa mtuhumiwa huyo, lakini wakati anakimbizwa hospitalini, alipoteza maisha akiwa njiani," alisimulia.

Kwa mujibu wa Kamanda Maigwa, uchunguzi wa polisi katika tukio hilo unaonyesha kuwa mtuhumiwa huyo alikuwa na bastola yenye namba A 920580 ikiwa na risasi tisa.

Alisema silaha hiyo ilikuwa ikitafutwa na polisi baada ya kuibwa kwa mfanyabiashara mmoja wa Babati mkoani Manyara Machi mwaka huu.

Mwili wa mtuhumiwa huyo umehifadhiwa katika Hospitali ya Rufani ya Kanda KCMC, ukisubiri uchunguzi wa kitabibu na taratibu zingine za mazishi.




Ofisa Sheria wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Amani Mkwama (kulia), akitoa ushauri wa kisheria kwa mmoja wa wananchi waliofika katika soko la Mbauda kwenye Wiki ya Asasi za Kiraia (AZAKI), jijini Arusha jana. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# Asasi zataka sheria ya dharura ukatili wenza

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

ASASI za kiraia zimeiomba serikali kuchukulia matukio ya ukatili dhidi ya mwenza yanayoendelea hivi sasa, kama jambo la dharura na kutunga sheria ya ukatili majumbani ili kukomesha matukio hayo yanayoongezeka nchini.

Akizungumza jana Jijini Arusha wakati wa mjadala wa mada ya ukatili dhidi ya mwenza uliowahusisha wadau wa asasi za kiraia, viongozi wa dini, serikali na waathirika wa matukio hayo, Mkurugenzi wa Sera, Uchechemuzi na Maboresho wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Fulgence Masawe alisema wamekutana kutafuta ufumbuzi wa matukio hayo.

Alisema wameona kuna umuhimu wa kukabiliana matukio hayo na kushauri serikali namna bora ya kukomesha matukio hayo ambayo kila kukicha yanazalisha walemavu na vifo. "Katika Wiki hii ya Asasi za Kirai tumeweka mada hii ili tuje na mpango mkakati wa kushauri serikali jinsi ya kukabiliana na haya na tunaomba itunge sheria ya ukatili majumbani na kwa dharura kwa sababu wengi wanaokumbwa na matukio haya ni wenza na kufanyika kwenye nyumba zetu," alisema.

Fulgence alisema ongezeko la matukio ya kukatana mikono, mauaji na kuumizana maeneo mengine ya mwili kwa Tanzania ni hatari kwani yakiachwa yaendelee, yataharibu kizazi kijacho.

Alisema sababu kubwa ya ongezeko la matukio hayo ni wivu wa kimapenzi, ukatili wa kiuchumi na matatizo ya afya ya akili.


Mtafiti Mwandamizi wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Fundikila Wazambi, akiwasilisha ripoti ya ukatili dhidi ya mwenza, alibainisha kuwa takwimu za kimataifa zinaonyesha kati ya wanawake watatu, mmoja wao amefanyiwa ukatili wa kimwili au kingono.

Alisema ukatili huo hufanywa na wenza wao ambao ni mume, mke au rafiki wa kiume au wa kike kwenye nyumba zao.

"Inaonekana nyumbani kwa sasa ni sehemu hatari kwa kinamama kwa sababu mauaji na hata kusababishiwa ulemavu hufanyika nyumbani, hali hii lazima wadau tuungane kutafuta mbinu za kukomesha matukio haya," alisema.

Mmoja wa waathirika wa ukatili wa mwenza, Veronika Kidemi, Mwalimu wa Shule ya Sekondari Kiranyi wilayani Arumeru, alisema alikatwa na mume wake kiganja cha mkono wa kulia na sime Septemba 26, 2020 nyumbani kwake Kijijini Siwandeti.

"Sababu kubwa wivu wa mapenzi, mume wangu Alfanyo Ombeni, siku ya tukio alirudi Arusha kimyakimya na alipofika nyumbani hakunikuta, mimi nilikwenda kununua mahitaji ya ndani ili kujikimu na watoto wangu wawili, nilipofika nyumbani alianza kunirushia matusi na akachukua sime na kunitenganisha kiganja changu, ilikuwa ngumu kuhimili ile hali ila ninashukuru sasa nimezoea hali hii kwa msaada na ushauri niliopewa na wadau mbalimbali na maisha yanaendelea," alisema. Aliongeza kuwa kabla ya kukatwa kiganja chake, mwanzoni mwa ndoa yao kulikuwa na karaha kwa sababu ya matusi na vipigo, lakini ndugu walimsihi kuvumilia kwa kuwa ana watoto, hadi alipopata ulemavu huo na kila mmoja kuona "kumbe alikuwa na mwanamume katili".





# Kiwanda kilichofungwa kwa miaka 10 chaanza uzalishaji

**Na Oscar Assenga,** LUSHOTO

KIWANDA cha Chai Mponde kilichofungwa kwa zaidi ya miaka 10, kimeanza tena kuchakata majani mabichi ya chai.

Kiwanda hicho kilifungwa kutokana na mgogoro kati ya wakulima na viongozi wa Chama cha Wakulima wa Chai (UTEGA) na mshirika wake, Kampuni ya Chai Lushoto inayokuwa ikiendesha kiwanda hicho, wakulima wakidai kuchoshwa na kile walichokiita kunyonywa na mwekezaji hivyo wakaamua kuacha kupeleka majani mabichi ya chai kiwandani huko na kusababisha kiwanda kukosa malighafi.

Akizungumza na waandishi wa habari juzi wakati wa ziara ya Mkuu wa Wilaya ya Lushoto, Kalisti Lazaro, Meneja wa Kiwanda hicho, Saane Kwilabya alisema majaribio ya uzalishaji yalianza Septemba 2 mwaka huu na kwa sasa wameshazalisha tani 27 000 huku uzalishaji kwa siku ukiwa kati ya tani sita na saba.

Meneja huyo alisema kuwa licha ya kuanza majaribio ya uzalishaji lakini tayari wameshapata soko la uhakika Pakistan ambako sampuli iliyopelekwa kwa mnunuzi imekubalika kutokana na ubora.

"Tumepata soko Pakistan, hivyo kwa sasa tunaendelea kukusanya majani taratibu ili kwenda kuingia sokoni, vibali vyote kutoka OSHA na TBS tumeshapata," alisema meneja huyo.

Mkuu wa Wilaya hiyo, Lazaro, alisema kiwanda hicho kimefufuliwa na serikali kupitia mifuko ya hifadhi ya kijamii ya PSSSF na WCF.

Lazaro alisema serikali imetoa Sh. bilioni nne kwa ajili ya ufufuaji na ukarabati wa kiwanda hicho na hadi sasa fedha zilizotumika ni Sh. milioni 700 huku kiwanda kikiwa na mtaji wa Sh. bilioni tatu.

Alisisitiza fedha zilizobaki zitawasaidia katika matumizi mengine ikiwamo kununua vitendea kazi kama vile magari ya kubebea chai na kuni na kufufua shamba la miti linalomilikiwa na kiwanda hicho.

"Tunaishukuru serikali kwa kuamua kuwekeza Sh. bilioni nne kwa ajili ya ufufuaji na ukarabati wa kiwanda hiki kilichofungwa kwa zaidi ya miaka 10," alipongeza.

Alibainisha kuwa Halmashauri ya Bumbuli ina kata 18. Kati ya yake, 15 zinalima chai katika skimu tano zilizopo.

Richard Mbughuni mmoja wa wakulima na Diwani wa Mponde, alisema zaidi ya wananchi 6,000 wanalima chai na kati yao, 200 wameshapatiwa mikopo nafuu kwa ajili ya kufufua mashamba yao.

"Sisi wakulima tunaamini juhudi za Mbunge January Makamba zimefanya Rais wetu kutupatia fedha za kufufua kiwanda. Hivyo, tunawaahidi hatutawaangusha, tumeamua kurudi shambani ili tusikitie hasara kwa sababu bila kupeleka malighafi ni hasara," alisema.

Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Hozza Mandia alisema uchumi wa Bumbuli unategemea kwa kiasi kikubwa zao la chai hivyo anaamini uchumi wao utaimarika kutokana na kiwanda hicho kuanza tena uzalishaji.



Mkuu wa Wilaya ya Mkinga, mkoani Tanga, Kanali Maulid Surumbu (wa pili kulia), akikabidhi mpango wa dharura wa kukabiliana na ukame kwa Ofisa kilimo wa Mji wa Handeni, Aldegunda Matunda, wilayani humo juzi, unaozilenga Halmashauri tatu za Handeni Mjini, Handeni Wilayani na Mkinga, zinazokabiliwa na mabadiliko ya tabianchi. **PICHA: HAMIDA KAMCHALLA**

## 75 mbaroni kwa uhamiaji haramu

■ **Wahukumiwa kifungo gerezani**

**Na Oscar Assenga,** KOROGWE

JESHI la Polisi likishirikiana na Jeshi la Uhamiaji mkoani Tanga limewakamata watu 75 kutoka Ethiopia na Mtanzania mmoja kwa tuhuma za uhamiaji haramu.

Limesema kuwa watuhumiwa hao wamekamatwa wilayani Korogwe wakiwa wamejificha porini.

Akizungumza na Nipashe jana ofisini kwake, Ofisa Uhamiaji Mkoa wa Tanga, Kamisha Msaidizi wa Uhamiaji Kagimbo Hosea alisema watuhumiwa hao walikamatwa Oktoba 25 mwaka huu majira ya saa 7.30 mchana.

Alisema watuhumiwa hao walikamatwa katika Kijiji cha Mwakijungi-Mwembeni, Kata ya Hale wilayani Korogwe baada ya vyombo vya dola kupata taarifa kuhusu watu waliojificha mahali huko na kuweka mtego eneo la tukio.

"Tulibaini kuwa watu hao walikuwa wamefichwa katika pori, tukaanza kufuatilia nani anawapatia chakula. Wakati tunafuatilia, tulipata taarifa kwamba wameshushwa eneo hilo lakini lori ambalo lilikuwa limewabeba lilikuwa limekwishaondoka.

"Taarifa zinaeleza kwamba wahamiaji haramu hao raia wa Ethiopia walishushwa kwenye lori ambapo namba zake za usajili hazikujulikana, lakini mmoja wa mashuhuda aliyeshuhudia wakishushwa, alipewa fedha na maelekezo na mtu anayetumia namba ya simu 0789... (anataja namba za simu iliyosajiliwa kwa jina la... (anataja jina)," ofisa huyo alifafanua.

Alisema walimkamata Yahaya Msemwa anayetuhumiwa kupewa jukumu la kuwaangalia na alitumiwa fedha kwa ajili hiyo, akifikishwa kwenye ofisi ya Uhamiaji Mkoa wa Tanga kwa ajili ya mahojiano.

Watuhumiwa hao walifikishwa mahakamani Oktoba 27 mwaka huu na kuhukumiwa kifungo cha mwaka mmoja gerezani baada ya kushindwa kulipa faini ya Sh. 500,000 kila mmoja.

# Asilimia 70 ya wanafunzi hawajui wanachokisomea

**Na Mary Mosha,** MWANGA

ASILIMIA 70 ya wanafunzi wa shule za sekondari wilayani Mwanga mkoani Kilimanjaro hawajitambui wanataka kuwa nani na mwenye taaluma ipi baada ya kuhitimu masomo yao ngazi za sekondari au vyuo.

Ofisa Elimu Taaluma Sekondari wa Wilaya hiyo, Emmanuel Kipele amesema kuwa kutokana na hali hiyo, serikali inaona kuna haja kuanza kutolewa elimu ya kujitambua na kujiamini kwa wanafunzi wawapo shuleni pamoja na mafunzo ya stadi za kazi.

Kipele alikuwa akizungumza juzi na wanafunzi wa Shule za Sekondari Msangeni na Kifaru wakati wa hafla ya kutambua vipaji chini ya Mradi wa Glami.

"Wanafunzi wanaohitimu kushindwa kuwa na malengo au ndoto zao, kwamba wanataka kuwa nani, ni jambo ambalo linadimiza vipaji na kuathiri elimu kwa kuwa matokeo yasiyoridhisha katika mitihani ya taifa.

"Zamani tulikuwa tukifundishwa namna bora ya kufanya kazi za mikono, na hii ilikuwa inasaidia kuhakikisha mwanafunzi anajitambua na kufahamu kipaji alichonacho.

"Kipaji kinaweza kutumika kumpatia mtu huyu kipato baadaye, tumeona wachezaji mpira, washonaji na wasanii wa fani ya uchoraji," alisema.

Mkuu wa Shule ya Sekondari Kifaru, Abdallah Mwambuka alisema kuwa baada ya kuanza kupata elimu ya kujitambua kutoka shirika lisilo la kiserikali Glami, tatizo la mimba shuleni huko na utoro limetatuliwa.

Mratibu wa Malezi wa Shirika la Glami, Aikande Muro, alisema kwa Mkoa wa Kilimanjaro, wana miradi miwili ambayo ni ya Binti Shupavu na Kisa, ikisaidia wanafunzi kujitambua, kuwa wastahimilivu na kujiongoza hasa wa kike.

Mkoa wa Kilimanjaro katika Mradi wa Kisa, shirika hilo linazihusisha shule 15 na wanafunzi 700.



## RC awataka machinga kuondoka mara moja

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, ameagiza wafanyabiashara wadogo (machinga) wanaofanya shughuli zao mitaa ya Jiji la Dodoma kuhakikisha ifikapo Oktoba 30, wawe wamehamia kwenye soko la wazi la Machinga Complex.

Senyamule aliyasema hayo juzi alipokuwa akizungumza na machinga hao katika mkutano uliofanyika kwenye soko hilo.

Alisema machinga watakaokutwa mitaani wakiendelea kufanya biashara zao watakuwa wamekiuka agizo hilo, hivyo wasije wakainyoshea serikali kidole kwa hatua itakazochukua.

"Nipende kuwatangazia machinga wote wa jiji la Dodoma wanaofanya biashara zao kwenye mitaa mbalimbali wanatakiwa kuondoka. Kuanzia 28,29 na 30 mwezi huu wa 10 mwaka huu, muwe mmehamia kwenye soko lenu hili la wazi la Machinga Complex tayari kwa kufanya biashara zetu,"alisisitiza.

Mkuu huyo aliagiza kamati ambayo ilikuwa ikiratibu shughuli zote za kuwadahili machinga hao,kuhakikisha walengwa wanaotambuliwa ndiyo wanaotakiwa kuingia kwenye soko hilo na kufanya biashara na si vinginevyo.

"Niwatangazie pia wavamizi wote waliovamia wanaojifanya wao pia ni machinga,sehemu hii siyo yao na ninawataka waondoke wenyewe waachiwe walengwa wa soko hili limejengwa kwa ajili ya machinga na siyo watumishi maofisini," alisema.

Awali, Kaimu Mkuu wa Divisheni ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji, Abeid Msangi akitoa taarifa fupi kwa mkuu wa mkoa, alisema kuwa kwa asilimia kubwa soko hilo limekamilika na mifumo yote ya mawasiliano na ulinzi inafanya kazi.

Alisema kuwa kutokana na kukamilika kwa miundombinu ya soko hilo machinga sasa watahamia kufanya biashara zao.

Naye, mwakilishi wa machinga Jiji la Dodoma, Shaban Simba, aliipongeza serikali kwa kuwajengea soko hilo la kisasa ambalo sasa litawaondolea kero ya kufanya biashara zao kwenye maeneo yasiyo rasmi.

Alisema soko hilo kwa kuwa ni la kisasa machinga watahakikisha wanafanya biashara kwa malengo ya kuinua mitaji na kulitunza kwa kufanya usafi.

Simba aliomba Ofisi ya Jiji na kamati inayoratibu machinga hao kuwa tayari kwa kusikiliza kero na mapendekezo yao.

# Walimu 919 nchini wafukuzwa kazi

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

TUME ya Utumishi wa Walimu (TSC) imetoa uamuzi kwenye mashauri 1,642 ya walimu ya makosa mbalimbali ya kinidhamu huku walimu 919 sawa na asilimia 56 wakifukuzwa kazi katika kipindi cha Machi 2021 hadi Septemba 2022.

Katibu wa Tume hiyo, Paulina Nkwama, aliyasema hayo juzi jijini hapa alipokuwa akizungumza kuhusu utekelezaji wa majukumu ya taasisi na vipaumbele vyake kwa mwaka 2022/23.

"Katika mashauri 1,642 yaliyoamuliwa, walimu 919 sawa na asilimia 56 ya adhabu zilizotolewa walifukuzwa kazi, walimu 234 sawa na asilimia 14.3 hawakupatikana na hatia, 115 sawa na asilimia saba ya adhabu zilizotolewa walishushwa vyeo, walimu 89 sawa na asilimia 5.4 walikatwa mshahara asilimia 15 kwa muda wa miaka mitatu.

"Walimu 143 sawa na asilimia 8.7 walipewa adhabu ya karipio, 59 sawa na asilimia 3.6 walipewa adhabu ya onyo na walimu 77 sawa na asilimia 4.7 walipewa adhabu ya kufidia hasara," alisema.

Hata hivyo, alisema mashauri 310 yapo katika hatua mbalimbali za kuyahitimisha (92 uchunguzi na vikao 218).

Awali, alisema kwa kipindi hicho walimu 1,952 walifunguliwa mashauri ya kinidhamu ambapo 1,362 sawa na asilimia 69.8 ya mashauri yote yalihusu utoro.

"Mashauri 260 sawa na asilimia 13.3 ya mashauri yote yalihusu kughushi vyeti, mashauri 119 sawa na asilimia 6.1 yalihusu mahusiano ya kimapenzi na wanafunzi, mashauri 98 sawa na asilimia 5 yalihusu ukaidi, mashauri 66 sawa na asilimia 3.4 yalihusu ulevi, Mashauri 16 sawa na asilimia 0.8 yalihusu ubadhirifu na mashauri 31 sawa na asilimia 1.6 yalihusu makosa mengineyo,"alisema.

"Mahusiano (uhusiano) ya (wa) kimapenzi kati ya walimu bila ndoa hairuhusiwi kwenye utumishi, taratibu ni zile zile za kuwawajibisha," alisisitiza.

Pia alisema sheria ya tume hiyo inatoa haki kwa mwalimu kukata rufani pale ambapo hakubaliani na uamuzi uliotolewa na Mamlaka yake ya nidhamu au mamlaka yake ya rufani.

Akizungumzia kuhusu vipaumbele vya 2022/23, alisema ni kusimamia utumishi na maendeleo ya walimu kwa kudumisha maadili na nidhamu kwa Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari.

Pia alisema wataendelea kuhakikisha kwamba walimu wenye sifa ya kupandishwa vyeo na kubadilishiwa kazi wanapata huduma hiyo kwa wakati baada ya kibali kutolewa na Mamlaka husika.




Mstahiki Meya wa Jiji la Dodoma, Prof. Davis Mwamfupe (wa pili kushoto), akizungumza katika kikao cha Baraza la madiwani, jijini humo jana. Wengine ni Mkurugenzi wa Jiji hilo, Joseph Mafuru (kushoto), Mwenyekiti wa CCM wilaya ya Dodoma, Charles Mamba (kulia) na Naibu Meya, Jamal Ngalya. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Wahamasishwa kushiriki tuzo ubora TBS

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

SERIKALI imetoa wito kwa wazalishaji wa bidhaa na watoa huduma kushiriki mashindano ya tuzo za ubora za mwaka 2022/23 zinazoratibiwa na Shirika la Viwango Tanzania (TBS) kwa kushirikiana na taasisi mbalimbali.

Rai hiyo ilitolewa jana jijini hapa na Kaimu Katibu Mkuu wa Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Aristides Mbwasi alipokuwa akizindua tuzo za tatu za ubora kitaifa kwa taasisi na watu binafsi wanaofanya vizuri kwenye masuala ya ubora.

Alisema miundombinu ya ubora ni eneo muhimu linalohitajika kuchangia ukuaji na maendeleo ya sekta ya viwanda na biashara.

"Matumizi ya viwango, udhibiti wa ubora, ithibati pamoja na ugenzi husaidia kulinda soko la bidhaa na huduma ndani ya nchi yetu na huboresha nafasi ya bidhaa na huduma zetu katika ushindani kwenye masoko ya kimataifa,"alisema.

Alifafanua kuwa tuzo hizo zilianzishwa ikiwa ni makubaliano baina ya wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo kwa nchi za kusini mwa Afrika(SADC) ili kutambua na kukuza sekta ya biashara kupitia ubora wa bidhaa.

"Tuzo hizi ni sehemu ya mipango ya serikali katika kuboresha huduma na bidhaa zinazotengenezwa nchini kupitia matumizi ya viwango na kanuni za ubora kwa taasisi za umma na binafsi,"alisema.

Alieleza kuwa tuzo hizo zimegawanyika kwenye vipengele vitano ambavyo ni tuzo kwa kampuni bora, tuzo kwa bidhaa, tuzo kwa huduma, tuzo kwa muuzaji bora kwa bidhaa nje ya nchi na mtu mmoja aliyefanya vizuri kwenye masuala ya ubora.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mkuu wa TBS, Dk.Yusuf Ngenya, alisema ili bidhaa za Tanzania ziuzike nje ya nchi ni lazima kuwa na bidhaa na huduma bora.

Alisema wazalishaji na watoa huduma za ubora wanatakiwa kujenga ushindani.

"Mwaka 2020/21 walijitokeza kushindana tisa tu, lakini 2021/22 walifika 23 na tunategemea mwaka huu kupata washindani zaidi ya 100,"alisema.

## Watakiwa kuzalisha zaidi miche ya minazi

**Na Mwandishi Wetu**

WATAALAMU wa kilimo wametakiwa kuongeza uzalishaji wa miche ya minazi na kuwafikishia wananchi ili kukabiliana na uhaba wa nazi Zanzibar.

Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo, Shamata Shaame Khamis, aliyasema hayo jana alipotembelea kituo kinachozalisha miche ya miti mbalimbali ikiwemo minazi, Selem, wilaya ya Magharibi A Unguja.

Alisema uhaba wa nazi Zanzibar unaweza kukabiliwa iwapo wananchi wataacha kukata minazi na kupanda mipya, hivyo kuna haja ya kuwa na vitalu vinavyozalisha miche bora na ya kutosha.

Pia alisema, lengo la ziara hiyo ni kutaka kujua changamoto zinazokikabili kituo hicho zinazosababisha kuwapo kwa upungufu wa miche ya minazi.

"Wataalamu wetu lazima mjitahidi sio kuzalisha miche ya kutosha pekee ila lazima muhakikishe kuwa miche hiyo inakua bora na inayohimili changamoto za hali ya hewa ya sasa tuondokane na kadhia ya kuagiza nazi kutoka nje ya Zanzibar," alisema Shamata.

Hata hivyo, alisema serikali itafanya jitihada ya kuhakikisha tatizo hilo linapungua na kuelekeza kuoteshwa kwa wingi miche ya minazi ya madafu ili kuzuia biashara hiyo isiathiri uzalishaji wa nazi.

Mkuu wa kituo hicho, Asaa Ali Suleiman, alisema tatizo la uhaba wa nazi linatokana na kuzeeka kwa baadhi ya minazi na kushindwa kutoa nazi za kutosha.

Alimweleza Waziri Shamata kwamba wameamua kuatika miche 450 ya minazi imechukua nafasi ya minazi iliyozeeka kusaidia kupunguza uhaba wa miche ya minazi.

Alisema wanakabiliwa na wizi katika eneo hilo unaochangia kupunguza upatikanaji wa miche na uzalishaji wa nazi zinazotumika kuzalisha miche hiyo.

# Zanzibar mwenyeji mkutano wanasheria mabunge Afrika

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

BARAZA la Wawakilishi Zanzibar linatarajiwa kuwa mwenyeji wa mkutano wa sita wa Chama cha Wanasheria wa Mabunge ya Afrika unaotarajiwa kufanyika siku tatu kuanzia Novemba Mosi, mwaka huu.

Akizungumza jana na waandishi wa habari katika ofisi za Baraza la Wawakilishi, Chukwani, Katibu wa Baraza hilo, Raya Issa Mselem, alisema mkutano huo unatarajiwa kuhudhuriwa na wanasheria 150 wanaohudumia mabunge mbalimbali ya Afrika ikiwa ni pamoja na mabunge ya kitaifa na mabunge ya majimbo.

Aliyataja mabunge hayo kuwa ni Baraza la Wawakilishi, mabunge ya Tanzania, Zambia, Gambia, Ghana, Msumbiji, Jumuiya ya Kiuchumi ya Nchi za Afrika Magharibi (ECOWAS) na Kenya na kaunti zake.

Mabunge mengine ni Sierra Leone, Botswana, Malawi, Zimbwabwe, Nigeria, Shelisheli, Uganda, Afrika Kusini na Eswatini.

Alisema mkutano huo unatarajiwa kufunguliwa na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, na mada mbalimbali zitawasilishwa na wataalamu wabobezi wa sheria wa ndani na nje ya nchi. "Tunatarajia kuwa mkutano huo utaongeza utaalamu wa wanasheria wa mabunge katika kuwahudumia wajumbe wa mabunge yao," alisema.

Katibu huyo alisema kufanyika kwa mkutano huo visiwani hapa kutatoa mchango mkubwa wa juhudi za serikali za kuimarisha utalii hasa utalii wa mikutano ambao unaimarisha kwa kasi kubwa uchumi wa nchi.

Pia alisema mkutano huo pia utaleta manufaa mengi ya pande zote kwa taasisi za serikali ya Zanzibar.

Alisema chama cha wanasheria wa mabunge ya Afrika ni chama kinachowakusanya wanasheria wa mabunge ya nchi za Afrika na kiliasisiwa mwaka 2011 Nairobi, Kenya kikiwa na malengo mbalimbali ikiwamo kujenga uhusiano wa karibu na kubadilishana taarifa, uzoefu na ujuzi baina ya wanasheria wanaouhudumia mabunge.

Lengo lingine, Alisema ni kuzifanyia uchunguzi na kuimarisha kazi na majukumu ya wanasheria wanaohudumu katika mabunge ya Afrika kujenga uwezo wa wanasheria barani Afrika.

Naye, Rais wa chama hicho, Mussa Kombo, alisema wageni hao pia watapata fursa ya kutembelea vivutio mbalimbali vya kitalii vilivyopo Zanzibar.



Rais wa chama cha wanasheria wa mabunge ya Afrika, Mussa Kombo (kushoto), akizungumza na waandishi wa habari, Chukwani Zanzibar jana, kuhusu mkutano wa chama hicho, unaotarajiwa kufanyika Novemba moja mwaka huu. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# SMZ yaomba China wataalamu habari

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WIZARA ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, imeiomba serikali ya China, kuendeleza ushirikiano na wizara hiyo ili kuongeza wataalamu katika sekta za habari na utamaduni.

Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Fatma Hamad Rajab, aliyasema hayo jana katika kikao cha tathmini ya mkutano wa 20 wa chama tawala cha China (CPC) kilichochofanyika katika ubalozi mdogo wa nchi Mazizini Zanzibar.

Katibu mkuu huyo alisema hatua hiyo pia ililenga kukuza lugha ya Kiswahili kwa kuwa nchi hiyo ina magazeti yanayoandikwa kwa lugha hiyo.

"Niwapongeze sana kwa kukuza lugha ya Kiswahili lakini niwaombe mwendelee kuipa nguvu sekta ya habari na mawasiliano hasa katika nyanya za wataalamu," alisema Fatma.

Naye Naibu Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Khamis Abdullah Said, alisema serikali inaupongeza ubalozi huo kwa kuendeleza ushirikiano uliopo katika sekta hiyo na nchi hiyo inavyoendelea kupiga hatua nzuri ya kiuchumi jambo ambalo linaipa nguvu Zanzibar.

Alisema, mchango wa Rais wa Kwanza wa Tanzania, Mwalimu Julius Nyerere na Mwenyekiti wa Chama cha CPC, Mao Zedong, umekuza uhusiano unaoendelezwa na Rais wa sasa wa chama na nchi hiyo Xi Jinping.

"Rais Jinping ameonesha uongozi bora kwa nchi yake kwani licha ya kuwa na idadi kubwa ya watu katika taifa hilo, lakini ameweza kupambana na tatizo la umaskini," alisema Said.

Balozi mdogo wa China, Zhang Zhisheng, aliipongeza Serikali ya Zanzibar kwa kuendeleza ushirikiano na taifa hilo na namna wanavyojali kuendeleza udugu ulioanzishwa na viongozi wakuu wa taifa hilo.

Alisema CPC imefanya mengi ya maendeleo kwa kushirikiana na mataifa ya Afrika, ambayo uchumi wake unaendelea kupiga hatua kila siku, jambo ambalo linaipa faraja China kuendelea kushirikiana na Tanzania kuinua uchumi wa nchi.

Alisema ubalozi huo utaendelea kushirikiana na Zanzibar kukuza sekta ya habari na wakati wote wako tayari kutoa taarifa wanazozihitaji ili kuepuka upotoshaji wa habari.

"Hivi karibuni kulitokea upotoshaji kwamba China imefungua vituo vya polisi nchini Tanzania, jambo ambalo si la kweli kwa kuwa nchi yetu haiwezi kuingilia mamlaka ya utendaji wa sera za ndani ya nchi," alisema.



## HARMONIZE
UKURASA 16

Nipashe
MWANGA WA JAMII
BT
BURUDANI TELE
JUMAMOSI OKTOBA 29, 2022




# ANJELLA

UKURASA WA 15

YUKO WAPI ?

# Salum Abdallah-3

## Mtunzi wa kibao 'Mkono wa Idd', Aliiba pesa kuunda bendi yake





**Na Adam Fungamwango**

WIKI iliyopita tuliona jinsi mwanamuziki Salum Abdallah Yazidu (SAY) alipokutana na zengwe wa marafiki wa baba yake kumkwamisha kwenye maendeleo ya kipaji chake cha muziki kiasi cha kuamua kutoroka nchini kutaka kwenda Cuba kwa ajili ya kujifunza zaidi muziki.

Aliondoka nchini kwa kuzamia meli.

Hata hivyo, kutokana na hali ya kisiasa wakati huo duniani kutokana na mgogoro wa Vita Kuu ya Pili ya Dunia, meli aliyozamia, ilishindwa kwenda Cuba na kuishia Mombasa nchini Kenya, ikisikilizia usalama kwanza.

Ilibidi Salum akae Mombasa kwa muda mrefu na pesa za kujikimu zilipokwisha, ilibidi aanze kazi ya kuuza mishikaki mitaani.

Siku moja akiwa kwenye matembezi alikuta sherehe za Maulidi kwenye nyumba moja na vijana walikuwa wakipiga dufu na kughani.

Alipendezwa mno, hivyo naye alijiunga nao. Naye alianza kughani kwa sauti ambayo ilimshtua kila mtu, kiasi kwamba kila mmoja alitaka kumfahamu yeye ni nani na anaishi wapi.

Ingawa hakutaka kujitambulisha sana, lakini baadhi ya Waarabu wafanyabiashara kati ya Mombasa, Dar es Salaam na Morogoro walimtambua kuwa ni Salum, mtoto wa mzee Abdallah Yazid wa Morogoro.

Na pia, baadhi alikuwa ameshapata taarifa za kupotea kwa kijana wa mzee Yazid mjini Morogoro na hajulikani alipo.

Vyama vya kusaidiana vilikuwapo tangu zamani, hivyo wanachama wa Chama cha Waarabu Afrika Mashariki ambacho pia mzee Abdallah Yazid ni mwanachama wake, walichanga pesa na kuamua kumsafirisha kutoka Mombasa hadi Morogoro.

Hivyo ndivyo Salum Abdallah alivyokosa safari ya kwenda Cuba, alivyohangaika mjini Mombasa na kurejea tena mikononi mwa baba na familia yake.

Kupotea kwa Salum kulimliza mno mzee Abdallah Yazid, kwani aliona amepoteza kijana wake mwenye akili nyingi wa kusimamia mali zake, na tayari alikuwa ameshaanza kuziendeleza, mwenye uono wa kisasa zaidi, pia mrithi wake.

Hivyo aliporejea, aliachana na mambo ya kusikiliza maneno ya pembeni, hivyo alimuachia kijana wake afanye anachokitaka.

**La Paloma yawa Cuban Marimba**

Baada ya kuachiwa huru ni kama vile 'kichaa alikuwa amepewa rungu' Salum Abdallah, aliamua kuchukua pesa kwenye biashara zao na kununua vyombo vya kisasa vya muziki vinavyotumia umeme wakati huo ndiyo kwanza vinaingia nchini.

Akaibadilisha kabisa bendi yake ya awali La Paloma iliyokuwa imesimama baada ya yeye kutoroka na kuiita Cuban Marimba.

Uhuru huo sasa ulimpa fursa Salum kuonyesha kipaji chake na kila mmoja sasa alikubali kuwa kijana huyo alizaliwa kwa ajili ya muziki na si vinginevyo.

**Kutoka kuhangaika na kuwa staa**

Baada ya kurekodi nyimbo kadhaa, tayari Salum alianza kuwa staa na kila mmoja alishangazwa na kipaji chake cha ajabu cha kila mwaka, bendi yake ya yeye mwenyewe walizidi kuwika kiasi cha kumfanya kuwa maarufu Afrika Mashariki yote.

Ikumbukwe kuwa Salum, pamoja na kurekodi nyimbo nyingi nchini, lakini alikuwa ni mmoja wa wanamuziki wa kwanza Tanzania kwenda kurekodi nyimbo nchini Kenya, na kwa bahati nzuri alikuwa ameshakuwa mwenyeji kidogo hasa mjini Mombasa ambako alishawahi kuishi.

Nyimbo zilizompatia zaidi umaarufu ni "Ngoma Iko Huku', 'Shemeji Shemeji','Mkono wa Idd', 'Wanawake Tanzania', 'Sipati Majibu,' 'Naumia', 'Cuba Chacha' na 'Ewe Mola Wangu.'

'Ewe Mola Wangu' ni moja kati ya nyimbo za mwisho za mwanamuziki huyo kabla ya kufariki, na mashairi ya wimbo huo yalitafsiriwa na mashabiki wa muziki kuwa alikuwa anatabiri kifo chake.

**Itaendelea wiki ijayo**



# SAFARI HII ANJELLA

WASWAHILI wana msemo wao unaosema lisemwalo lipo, kama halipo basi linakuja! Hivi sasa kuna taarifa zinazosambaa mitandaoni kwamba ndani ya lebo ya Konde Gang, inayoongzwa na Mwanamuziki Harmonize, hali imekuwa si shwari.

Baada ya kufukuzwa kwa wasanii wawili waliokuwa chini ya lebo hiyo, Cheed na Killy, imeelezwa msanii wa kike pekee Anjella mguu nje, mguu ndani.

Inadaiwa wakati wowote Anjella anaweza kujitangaza kuwa huru baada ya uongozi wa lebo hiyo kumuonyesha mlango wa kutokea, licha ya hali hiyo kuwa siri.

Haijafahamika nini wameafikiana hadi sasa, lakini taarifa kutoka watu wa karibu zinaeleza Anjella amemalizana kila kitu na Harmonize.

Wadaku wamekwenda mbali zaidi kwa kueleza Anjella amejitenga na uongozi, kiasi ambacho hajaposti chohote kuhusu bosi wake. Posto yake ya mwisho kuhusu Harmonize aliiweka mwezi Mei mwaka huu.

Licha ya Harmonize kutangaza ujio wa Albam mpya, Anjella hajaposti chochote na kuongeza kasi ya uvumi huo kwamba hayuko tena Konde Gang.


Tetesi za anjella kumalizana na Konde Gang huenda zikawa za Msanii mwenzake Ibraah na watu wengine wa Konde Gang wameshiriki kuiweka katika kurasa zao za mitandao kava ya Album hiyo.

Kutokana na ukimya ulioko kila upande kuzungumzia suala hilo, watu wamebaki wakisubiri nini kitatokea.

## INSTA-TWITTER

Tuffolow/ Tu-tag

**@burudanitele**



**@kajalafrida**
Nyie nyie nimeimbiwa tena sasa bwana rajab @harmonize_tz hizi nyimbo zote si zangu inabidi nitoe EP yangu.

**@masanjamkandamizaj**
Baraka na Zawadi zote hizo zilifanyika kwa Wakati mmoja, Mungu hubariki wanao bariki wengine! Ninyi endeleeni na majungu





**@hamsaford**
Ogopa sana mwanamke wako akipata rafiki wa kiume harafu akampa muda wake na kuhakikisha ana furaha muda wote ..Bro ukiona hivyo kachunge mbuzi tu

**@dullvani**
Hata kama ndo kupenda umbea ila #mamachogo kazidisha ndo kumfuata mtu hadi kuzimu





**@whozu_**
Chi mama leo kaona kabla ya kurudi Dar amalizie bethidei yake kwa kutaka kunipaka 'make up' basi tu Nifanane nae Chibaba Hahah. Kafurahi mwenyewe..

BASI SAWA

## Ommy Dimpoz unawafanya watu wasilale



MASHABIKI wa muziki wa Bongo Fleva, wamekuwa na siku ngumu mtandaoni baada Staa Ommy Dimpoz, kutangaza kuachia Album yake mpya.

Album hiyo ambayo ni ya kwanza tangu aanze muziki, imepewa jina la Dedication, amewashirikisha wasanii mbali mbali akiwemo Nandy, Marioo, Black Diamond, Fally Ipupa, Muda Keys na wengine.

Katika mtandao wa kijamii, mashabiki wamekesha wakituma maoni yao tofauti kutokana na ujio wa Albam hiyo na kueleza Ommy Dimpoz amefanya kile ambacho wao walikuwa wakikitamani kila siku.

## Msikie Baraka The Prince anavyojigamba



Msanii wa BongoFleva, Barakah The Prince amesema kamwe hana kiburi kama anavyoelezwa na wasanii wenzake, bali jina lake limekuwa likiwahangaisha watu wengi.

Akizungumza na Planet Bongo, amesema hawezi kuondoka katika msimamo wake hata watu wakimzungumzia vibaya, anachoamini hata akikaa muda wa miaka 10 bila kutoa ngoma mpya, umaarufu wake bado utaendelea.

"Mimi siamini kama kuonekana katika vyombo vya habari kila siku ndio unalinda umaarufu, waache waniambie mimi nina kiburi ndio maana sionekani, ukweli nina uwezo mkubwa." Amesema.



## HARMONIZE UTAKIACHAJE KISWAHILI?

MKALI wa muziki wa Bongo Fleva, Harmonize, amewaambia mashabiki zake kwamba inaweza kuwa mara ya mwisho kuandaa albam kwa lugha ya Kiswahili.

Harmonize mwenye uwezo mkubwa wa kutunga nyimbo kuliko wasanii wengine, amesema albam mpya inayoitwa 'Made For Us' itakuwa ya mwisho kwake kuimba kwa Kiswahili, lakini hakubainisha lugha gani atatumia.

AlbUm ya kwanza inayoitwa Afroeast ilitoka mwaka 2020 na kufuatia ile ya pili High School iliyotoka mwaka jana.





## Rasco sasa unatafuta bifu

MWANAMUZIKI wa HipHop Rasco Sembo, ameamua kuwaponda wasanii wakongwe akisema yeye ndio rapa bora kwa sasa nchini na wanarukaruka.

Sembo amesema, kwa upande wake yupo tofauti kutokana na aina ya muziki anaoufanya na kwamba kimtazamo yupo juu tofauti na wengine.

"Wanaosema kuwa kuimba ukiwa nje ya nchi ndio alama ya mafanikio wanakosea kwa sababu mimi niko hapa Tanzania lakini naimba na kufanya vizuri huku nikifanya maendeleo kuliko wenzangu," amesema Rasco Sembo.

## MA-X WA WASANII WANAOLILIWA

**Na Adam Fungamwango**

KWENYE masuala ya mapenzi kuna mambo mengi sana yanayoonekana na yasiyoonekana. Kwenye mapenzi kuna muda wa kufurahi na kuhuzunika.

Ni muda ambao penzi limechujuka, kuisha na kuachana. Wakati mwingine wapenzi huachana kwa hasira tu, lakini moyoni inakuwa kinyume chake. Ndiyo maana baadaye utaona watu wanarudiana, halafu walimwengu wanashangaa kwa jinsi walivyoachana kwa maneno makali.

Kuna wengine wao wakishaondoka wameondoka. Kwao suala la kurudiana huwa walipo.

Sasa ukute mmoja anataka kurudiana na mwenzake, halafu mwingine hataki. Hayo maneno utaomba ardhi ipasuke uingie.

Wasanii mbalimbali wameshatunga ngoma kadhaa zinazohusiana na maudhui ya watu walioachana na wake, waume au wapenzi wao.

Kila mtu anazungumza kile anachojisikia kuhusu X wake. Wengine wakionekana kujutia, wengine hawana hata habari. Hivyo ndivyo mapenzi jinsi yalivyo.

**Mobeto ft Seneta-X Wangu**

Kwenye ngoma hii ambayo imeimbwa na Hamisa Mobeto pamoja na Seneta Kiraka, huyu bibie anashangaa ni nani ambaye kwa sasa anaishi na mpenzi wake wa zamani.

Anachoshangaa ni kwa nini hampi mapenzi motomoto kama yeye alivyokuwa anampa, kiasi kwamba kila siku anapiga simu kwake ili warudiane?

Ina maana huyu bibie hana kabisa mpango naye huyo jamaa. Anashangaa ni kwa nini huyo aliyenaye hamfanyi kumsahau yeye kwa sababu hawezi kurudiana naye, kwani naye ana wake ambaye kwa sasa wanapendana, hivyo kurudiana haiwezekani.

**Marioo-Dear X**

Msanii Marioo yeye ndiye akaamua kabisa kuweka bayana kuwa harudii matapishi. Ina maana kuwa hawezi kumrudia mpenzi ambaye ameshaachana naye.

Halafu kwenye ngoma yake hiyo anawauliza wenzake kuwa utamrudia X wangu au bora kufa? Hao jamaa nao wanaitikia 'bora kufa.' Wana maana ni afadhali kufa kuliko kurudiana na wapenzi wao wa zamani.

**Smile The Genius-X Wangu**

Msanii Smile The Genius, yeye naye akaja na ngoma yake ambayo haitofautiani na hizo mbili za juu.

Yeye anamwambia X wake kuwa asifikirie kama atarudi kwake kwa sababu penzi halipakwi rangi na ndiyo lishazama hivyo.

Akaenda mbali zaidi akidai hajutii kabisa kumpoteza mpenzi wake huyo kutokana na mambo aliyopitia wakati wakiwa wote.

"Najua dua unazoniombea ni njema, najua unavyoumia, nishajisahaulia, huna faida, nanawiri, huyu niliyenaye ndiyo anayesababisha." Hapo anapigilia msumari kabisa akionyesha kuwa hawezi kabisa kurudiana na X wake hata kwa bahati mbaya.

**D Voice- X Wangu**

Ngoma hii imepigwa kwenye mahadhi ya singeli ambapo msanii D Voice anampasha mpenzi wake ambao wanaonekana ni kama vile alimtaka warudiane.

"Si ulinidharau, ukaniona wa nini mama, na ukasahau kuwa vizuri vipo vingi, ukirudi umelewa, pole dear X mwenzako nipo salama, mambo ya stress nishasahau hizo zama, lako penzi feki kwangu limechina, kwangu sizeeki, nadekezwa kama mwana." Nadhani ukishambiwa hivyo kinachofuata ni kutafuta mpenzi mwingine tu.

**Lody Music-X wangu**

Katika ngoma zote nne, hii ya Lody Music iko tofauti. Huyu jamaa anajutia. Huyu anamkumbuka X wake. Kila anapogusa anaona hapana, yule wake wa zamani alikuwa bomba zaidi kuliko hawa wengine

"Nimekumbuka, sorry nimeona bora nikupigie, na kuna makelele toka nje tuongee, nimezunguka kote na nimeamua kukurudia.

Tangu nimekuachia mwenzako nimefubaa, naendekeza pombe mwenzako nalala na njaa, mapenzi yananifanya nilie, mwenzako nakonda vibaya." Du, hapa ndiyo utaona mapenzi kizungumkuti. Wakati yupo anayelia usiku na mchana hata kula hali kwa ajili ya kumbembeleza mpenzi wake wa zamani warudiane, lakini yupo anayesema kurudiana naye ni bora afe. Hiyo ndiyo dunia.

FILAMU

## Nyota ya Kifalme: Mungu akikupa haandiki barua

**Na Adam Fungamwango**

BAHATI ya mwenzako usiilalie mlango wazi na wala mwenye bahati habahatishi. Hii ni baadhi ya misemo ya Waswahili kuhusiana na neno lenyewe bahati.

Leo hii tunaiangalia filamu iitwayo 'Nyota ya Mfalme' inayoomlenga kijana mmoja aliyepata zali tu la kuwa mfalme kwa bahati nasibu.

Yeye mwenyewe hakupanga, na wala hakuona. Hakuzaliwa kwenye familia yoyote ya asili ya ufalme, lakini imewezekana. Amepitia changamoto kadhaa na kutishiwa kuuawa, lakini mwisho wa dhiki faraja.

Filamu hiyo imechezwa na Noel Msonga, Bahati Kindamba, Muruswad Sanane, Hanifa Siraju, Twaha Mbarale na wengine.

Filamu inaanza kwa kuwaonyesha watu watatu waliokuwa wakiishi pamoja. Kwenye adhi hiyo hakukuwa na mtu mwingine zaidi yao.

Watu hao ni Wanyika, Mbarale na Pecha. Pecha na Mbarale ni ndugu wa baba na mama mmoja, Wanyika akiwa ni ndugu yao mtoto wa shangazi.

Ni ardhi ambayo miaka mingi ya nyuma ilikuwa na watu wengi, lakini kulitokea vita iliyoua watu wengi.

Wenyewe hao watatu wakaamua kumtengeneza mfalme wao wa kuchonga, Pecha akawa ndiye upande wa pili wa adhi hiyo kulikuwa na mama mmoja aliyekuwa akiishi na binti mmoja tu.

Siku moja akamwita na kumwambia miaka yote waliyokuwa wakiishi hakuwahi kumwambia kuwa yeye si mama yake mzazi. Anamwambia nchi hiyo wanayoishi kulikuwa na vita iliyoua watu wengi ikiwemo mfalme na malkia. Akamfahamisha kuwa mfalme na malkia ndiyo walikuwa



wazazi wake. Na yeye alikuwa ni kijakazi wake. Akamkabidhi vitu ambayo alipewa na baba yake kabla hajafa ili ampe binti huyo. Akamwambia anaweza kuurudisha ufalme wa baba yake kama anaweza kumpata mume wa kumuoa.

Kijuti anaamua kumuacha binti mfalme Nyahale ili akamtafutie mwanaume, lakini akaingia mikononi mwa wale wanaume watatu, Wanyika, Mbarale na mfalme Pecha.

Kwa sababu hakukuwa na mwanamke eneo hilo, wote hao walimtaka Pecha kwa sababu yeye ni mfalme akamchukua yeye ili awe malkia, na akamtimua Wanyika. Mbarale alibaki tu kwa kuwa ni mdogo wake.

Wanyika alitoka na kwenda kujenga kibanda chake nje ya mji. Wakati huo Nyahale naye alikuwa akimsaka mama yake wa hiari ambaye hajamuona kwa siku tatu. Njiani naye anaangukia mikononi mwa Wanyika aliyejitengenezea kimji chake.

Ghafla walitokea kupendana na kwa mujibu wa taratibu zilizopo ni kwamba yoyote atakayekuwa mume wa Nyahale binti mfalme, ndiye awe mfalme. Ufalme wa mchongo ukatoka kwa Pecha na kwenda kwa Wanyika.

BARIZI LA PWANI

# SHAKIRA SAID-4

# Mwimbaji mkongwe wa taarab alitamba kwa sauti tamu ya kinanda



MWIMBAJI mkongwe wa taarabu nchini Tatu Said, maarufu kama 'Shakila Said' ni miongoni mwa wasanii waliojizolea sifa kutokana na mchango wake mkubwa kuinua muziki huo.

Katika mwendelezo wa maisha yake ya kisanii, wiki iliyopita tuliangazia namna alivyoshiriki katika siasa za nchi na kujiunga jeshini na kuunda bendi ya taarab.

Wiki hii tunaendelea na simulizi ya msanii huyo kwa kuangalia mambo aliyokumbana nayo ikiwa siku za mwisho wa maisha yake.

Shakila aliwahi kutamka kuwa yeye ni miongoni mwa wasanii ambao hawakunufaika na kazi zake kama ilivyo kwa wasanii wengi wa zamani kutokana na mfumo mbaya.

Sauti yake nyororo ilikuwa haitofautiani sana na mwimbaji kutoka Somalia aliyeweka makazi yake nchini Kenya, Aisha Abdul maarufu 'Malika' ambaye sasa anaishi nchini Marekani.

Shakira alistaafu muziki akiwa katika bendi ya Jeshi la Kujenga Taifa mwaka 2009.

Licha ya kustaafu, alikuwa akiitwa kwenda kuimba na kundi lake hilo la JKT ambapo alikuwa akilipwa ujira wa shilingi 3,000 wakati akifanya onyesho moja.

Tatu Said 'Shakila' alikuwa akilalamika kuwa baada ya kustaafu, hakuwa na pesa za kujikimu kimaisha kwa kuwa kiwango alichokuwa akipokea kilikuwa hakimtoshi.

Alilazimika kuishi kwa kupika na kuuza visheti na vitumbua.

Kabla ya kufariki, Shakira alikuwa mbioni kumalizia albamu yake ya 'Mama na Mwana' ambayo ingelikuwa na nyimbo nane na kati ya hizo, tano zilikuwa zimekamilika ukiwamo wa 'Mama na Mwana'

Shakila alibahatika kupata watoto 15, kati ya hao 12 bado wako hai.

Binti yake anayejulikana kwa jina la Mape, ndiye pekee aliyetajwa kama mrithi mikoba ya taarabu ya mama yake.

Msanii huyo alifariki ghafla baada ya kumaliza kuswali swala ya Magharibi.

Shakira alianguka ghafla na alipofikishwa hospitali alielezwa kuwa tayari amekwisha fariki. Aliizikwa Agosti 20, 2016 huko Mbagala Charambe jijini Dar es Salaam.



## BATA LA WIKI

Je una kiwanja cha burudani piga -0717336368

**Bogos Musica**
Bendi hii chini ya Nyoshi El-sadat, Jana ilikuwa katika ukumbi wa Kibozone, Mbezi Malamba Mawili, leo Jumamosi wapo katika ukumbi wa Nakomida Park Kimara Temboni na kesho wapo ndani ya Board Room Sinza Mori.

**Kimokimo Band**
Kundi hili ambalo linaongozwa na mwimbaji wa siku nyingi aliyepitia bendi mbalimbali, Khadija Kimobitel, kila Ijumaa linatoa burudani ya nguvu katika ukumbi wa Mariot uliopo eneo la Extertanal.

**FM Academia 'Wana Ngwasuma'**
Kama kawaida yao wakiwa chini ya Patcho Mwamba, kila Jumamosi wapo ndani ya ukumbi wa Mawasiliano Park Ubungo wakifanya vitu vyao.

**Waluguru Original**
Bendi hii yenye maskani yake mjini Morogoro, jana Ijumaa ndani ya ukumbi wa Kambarage SUA, Jumamosi wapo Terminal Pub Msamvu na Jumapili wapo eneo hilo, katika ukumbi wa F2 Florida.

**Twanga Pepeta**
Jana Ijumaa walikuwa ndani ya ukumbi wa Mawasiliano Park Ubungo, leo Jumamosi watafanya vitu vyao katika ukumbi wa Muungano Park, Kivule na kesho wapo Gwambina Lounge (zamani TTC Club Chang'ombe).

**Orchestra Sikinde Original**
Bendi hii mpya chini ya mwimbaji Abdalah Hemba, leo Jumamosi inafanya makamuzi katika ukumbi wa Shabaha Mbezi Becah, kesho Jumapili itamalizia wikiendi katika ukumbi wa Nefaland Manzese Argentina.

**Msondo Ngoma**
Leo Jumamosi bendi hii kongwe itatoa burudani katika ukumbi wa Kwetu Pazuri Mbezi kwa Msuguri, kesho Jumapili kama kawaida itamalizia wikiendi katika ukumbi wa Dar Safari uliopo eneo la Buza.

**Mjengoni Classic Band**
Bendi yenye maskani yake jijini Arusha, kila Ijumaa na Jumamosi huwa inafanya vitu vyake katika ukumbi wa Kokoriko Annex, siku ya Jumapili huwa ipo ndani ya ukumbi wake wa nyumbani wa Mjengoni Club Orasiti jijini humo

**Tukuyu Sound Band**
Bendi hii inayoongozwa na vijana machachari, Kalala Junior na Papii Kocha, kila Jumapili kama kawaida yao humalizia wikiendi katika ukumbi wao wa nyumbani wa Mawasiliano Park uliopo Ubungo.




# BINADAMU WABAYA WILL PAUL AJUTIA...

KWELI dunia ni kama uwanja wa fujo, ndivyo Staa wa muziki wa kizazi kipya kutoka Kenya, Willy Paul anavyojikuta akipambana kwa sasa na walimwengu.

Paul, hakujua kwamba hatua yake ya kujichangisha fedha na kununua gari, kama ingemtokea puani na kuanza kujutia kutokana na maneno ya watu.

Kama ilivyokuwa kwa wasanii wengine, Willy Paul aliamua kununua gari aina ya Mercedes Benz na kisha kulianika mitandaoni, lakini majibu yake yalikuwa tofauti, wengi walimdhihaki kwa kudai alidanganya kuwa amenunua gari jipya.

Gari hilo lenye rangi ya njano, linadaiwa kuwa sio jipya badala yake lilipakwa rangi ili lionekane jipya.

Katika ukurasa wake wa Instagram, alikana madai hayo huku akipakia video iliyoonyesha magari yake yote, kuanzia ya zamani na matatu aliyonunua hivi karibuni.

"Walisema nilipaka gari langu la kitambo rangi ya njano, hapana, magari yangu haya hapa yametulia. Maisha mazuri yasiyo na vikwazo maisha bila utata wowote," Willy Paul alijigamba.

Mwanamuziki huyo aliwashauri watu kuwatakia wengine mema na kutowaonea wivu wanapofanikiwa.

"Mjifunze kusherehekeana kwa sababu maisha ni mafupi na hayataki hasira, kwa hivyo mfurahie maisha ," aliongeza.

Amemshukuru Mungu kwa mafanikio yake mwaka huu na kwa kumjalia uwezo wa kujizawadi gari lingine.

Willy Paul aliwashukuru mashabiki wake kwa kumuunga mkono wakati wote na hata wale ambao walikuwa wanamkejeli.

"Na kwa mashabiki wangu ambao walinipa nafasi ya pili asanteni. Ni kwa sababu ya ukarimu wenu nimefika hapa," alisema.



# Burna Boy afaidi mastaa wa majuu

MWIMBAJI maarufu nchini Nigeria na mshindi wa tuzo ya Grammy, Burna Boy, ameendelea kukaa bega kwa bega na mastaa wakubwa wa kimataifa

Hivi karibuni Burna Boy ameonekana akiwa pamoja na msanii wa Marekani, DJ Khaled, huku akionyesha zawadi yaa boksi nne za viatu vipya alivyokabidhiwa.

Kupitia ukurasa wake rasmi wa Instagram, kupitia simulizi zake, Burna Boy alifichua kwamba alikuwa amepewa zawadi ya sneakers na staa huyo wa kimataifa.



## Wengi wahoji afya ya akili ya Kanye

RAPA na mbunifu wa mitindo nyota kutoka Marekani, Kanye West maarufu kama Ye, amejikuta akipoteza utajiri wake kutokana na kichwa chake kutotulia na kushabikia mambo yenye utata.

Kanye ambaye siku za nyuma aliwakasirisha Wamarekani weusi baada ya kuelezea utumwa ni kama watu walijitakia, na hivi karibuni kuibua mjadalaa kuhusu kauli yake kwamba Watu weupe wana haki ya kuishi, kauli zake zimewakera watu wengi na kila mara wanamuona kama aliyechanganyikiwa akili.

Tweet iliyomponza na kusababisha kampuni zilizokuwa akifanya nao kazi kujiengua ni ile aliyeandika kupitia Twitter kwamba “Ninapoamka, ninakaribia kwenda Death Con” kwa Wayahudi,”.

## Kumbe Meghan katoka Nigeria?

MKE wa mwanamfalme wa Uingereza, Prince Harry, Meghan Markle ametoboa siri kwamba ana uhakika kuwa asilimia 43 ya vinasaba asili yake nchini Nigeria.

Akizungumzia asili yake wiki hii, Meghan amesema amefanya vipimo vya vinasaba na kugundua kuwa chimbuko la ukoo wake una asili ya Nigeria na hivyo anaamini yeye ni mmoja wao.

“Nitaanza kuchimba zaidi katika haya yote kwa sababu mtu yeyote ambaye nimemwambia, hasa wanawake wa Nigeria, ni kama wameshtuka” Meghan anasema.





## Kunle amtaliki mkewe

NDOA ya muigizaji wa Nollywood Kunle Afod na mkewe Desola Afod imevunjika kutokana na sababu ambazo hazijawekwa wazi.

Hivi karibuni Desola alitumia akaunti yake ya Instagram kufichua kuwa ndoa yake na mwigizaji Kunle Afod imefikia mwisho.

“Habari njema unayotaka kusikia...niliondoka kwa Kunle Afod,” aameandikaa.

Ndoa nyingine ya watu mashuhuri iliyovunjika hivi karibuni nchini humo ni ya Gideon Okeke.

## Rihanna kuzindua ya Black Panther

MWIMBAJI nyota kutoka visiwa vya Barbados, Rihanna anaweka mambo sawa kurudi jukwaani baada ya wimbo wake uliopamba filamu ya Black panther, kutaka kuuzindua rasmi.

Rihana amekuwa nje ya muziki kwa zaidi ya miaka sita ataachia wimbo wake wa kwanza na hivyo kurejesha hamu ya mashabiki wanaotaka kumuona akiimba jukwaani.

Mashabiki wanatarajia wimbo huo ‘Lift Me Up’ kama kumkumbuka staa wa Filamu huyo ‘Wakanda Forever’ Chadwick Boseman ambaye alifariki kwa maradhi ya saratani.



AMOU HAJI MTU MCHAFU DUNIANI:

# Hajaoga miongo saba, ala nyama zilizooza

IDADI kubwa ya watu wanapata sifa kemkem kutokana na kufanya mambo mazuri, lakini kwa Amou Haji, mkazi wa Dejjah, nchini Iran amepata umaarufu baada ya kutajwa kuwa ndiye binadamu mchafu zaidi duniani.

Haji anadai usafi unasababisha maradhi na kwamba kukwepa kwake kuoga ndiyo sababu aliweza kuishi hadi miaka 94 bila kuugua.

Anajulikana sana kama mtu mchafu zaidi, lakini kwa Amou Haji hilo halijamsumbua na haoni kama jambo baya.

Kabla ya kufariki akiwa na umri wa miaka 94 mnamo Oktoba 2022, hakuwa ameoga kwa takriban miongo saba, kando na kunawa miezi michache tu.

Hatahivyo, ni ngumu kutaja sababu kamili, kulingana na Times Now News, baadhi ya wenyeji wanafikiri kwamba alikuwa na hofu ya maji.

Wengine wanasema aliamini tu kwamba usafi huleta magonjwa, na alibaki mchafu katika kutafuta maisha bora.

Karibu kila mtu alisisitiza kwamba Haji alivumilia aina fulani ya kiwewe cha ujana ambacho kilimfanya atafute maisha ya kujitenga.

Shirika la ZME Science liliripoti kwamba akiwa kijana, alimpenda mwanamke ambaye alimkataa.

Haijalishi ni sababu gani ya uchafu wake, ilionekana kama hali inayomfaa Haji, sambamba na maelfu ya mambo yake mengine ya ajabu ambayo wengi wetu tungeona yanachukiza.

Haji aliishi na kujiosha mara moja kati ya miaka ya 1950 na 2022, alifanikiwa kufikia umri wa miaka 94 licha ya hekima ya kawaida kusema kwamba usafi wa jadi ni sehemu muhimu ya kuishi maisha marefu na yenye afya.

**MLO WA AMOU HAJI**

Amou Haji aliripotiwa kujikimu kwa lishe na chakula chake alichopenda zaidi ni nyama ya nungunungu iliyooza.

Sio kwamba hakuweza kupata chakula kipya, lakini hakukipenda.

Inadaiwa Haji alikasirika wakati wanakijiji walipojaribu kumletea vyakula vilivyopikwa nyumbani na maji safi.

Ingawa alikataa maji safi, bado alibaki na maji, akinywa lita moja kila siku.

Alikusanya maji yake kutoka kwenye madimbwi na kuyanywa kutoka kwenye bati la mafuta lenye kutu. Alipokuwa akila au kunywa, Haji alifurahia burudani yake anayopenda zaidi kama vile kuvuta kinyesi cha wanyama kutoka kwenye bomba lake.



Wakati hakukuwa na kinyesi karibu, alikubali sigara za tumbaku, na alijulikana kuvuta sigara tano kati ya hizo kwa wakati mmoja.

**MAISHA YA AJABU**

Ingawa mara kwa mara Haji alipokea zawadi za chakula na sigara kutoka kwa wakazi wa eneo hilo, alipendelea kujizuia.

Aliishi nje kidogo ya kijiji kidogo cha Dejjah, na mahali alipopenda sana pa kulala palikuwa ndani ya shimo la ardhini.

Miaka kadhaa iliyopita, kikundi cha wananchi wenye urafiki walimjengea kibanda cha matofali ili alale kukiwa na mvua au baridi nje.

Mbali na kibanda hicho, alifanikiwa kupata joto wakati wa miezi ya baridi kwa kuvaa kofia kuukuu na kuweka matambara machache ya nguo alizomiliki.

Amou Haji anaweza kuwa hajaoga, lakini bado alijali jinsi alivyokuwa anaonekana.

Alipunguza nywele na ndevu zake kwa kuzichoma hadi urefu aliotaka na alitumia vioo vya gari kujitazama mara kwa mara.



Hata hivyo, inaonekana alifurahia kuishi peke yake, nyakati fulani alionekana kuwa mpweke.

Haji alikuwa na matatizo ya kueleweka linapokuja suala la kukutana na watu, lakini inasemekana alisema kwamba angependa kupata mke.

Kulingana na LADbible, mambo ya kufurahisha ya Haji ni pamoja na kuendelea na siasa na kujadili vita alivyokuwa akifahamu zaidi, ikiwamo Mapinduzi ya Ufaransa na Urusi.

Gavana wa eneo hilo hata alisema kwamba Haji alipendeza kuzungumza naye licha ya sura yake, na aliwashutumu wakorofi waliomdharau na kumrushia mawe na maneno.

Haji alionekana kuzoea unyanyasaji huo, hata hivyo, kwani aliushughulikia kwa karibu miaka 70.

Afya ya Amou Haji ilivyostawi

Kwa mtu ambaye hajaoga tangu miaka ya 1950, Amou Haji alikuwa na afya ya kushangaza katika maisha yake yote.

Madaktari wa eneo hilo ambao walimfanyia vipimo walishangaa kwamba mzee huyo wa miaka 94 aliweza kudumisha maisha yake machafu.

Kulingana na PopCrush, Profesa mshiriki wa parasitology kutoka shule ya afya ya umma huko Tehran aitwaye Dk. Gholamreza Mowlavi aliwahi kumfanyia vipimo Haji ili kubaini kama alikuwa na ugonjwa wowote unaohitaji tiba.

Baada ya kupima kila kitu kuanzia homa ya ini hadi UKIMWI, Mowlavi alihitimisha kuwa Amou Haji alikuwa na afya nzuri sana.

Ilibainika alikuwa na ugonjwa mmoja tu wa trichinosis, ambao unasababishwa na maambukizi ya vimelea vinavyotokana na kula nyama mbichi au isiyopikwa vizuri.

Kwa bahati nzuri, Haji hakuonekana kuonesha dalili zozote za kutishia maisha.

Dkt. Mowlavi pia alibaini kuwa huenda Haji alikuwa na mfumo thabiti wa kinga baada ya miongo saba bila kuoga.

Amou Haji alistawi katika mbinu yake isiyo ya kawaida hadi kifo chake kilichotokea mwaka huu.

Kulingana na Guardian, kifo chake kilikuja miezi michache baada ya wenyeji kumshawishi kuoga kwa mara ya kwanza katika takriban miaka 70.

# Maelfu walivyonufaika na utafutaji, ujasiriamali Dar

## • Wanawake wang'ara kusaka mafunzo, fursa kujikomboa

**Na Sabato Kasika**

KATIKA juhudi za kuwasaidia wanawake na vijana kuinuka kiuchumi kupitia ujasiriamali, wakazi takribani 5,000 wa Kipunguni jijini Dar es Salaam, sasa wanaweza kujisimamia wenyewe kutokana na kufunzwa mbinu za utafutaji na ujasiriamali unaolenga kuwainua kimaisha.

Kati ya 5,660 waliofunzwa vijana 3,650 wamenufaika na mafunzo stadi ya ujasiriamali katika mpango wa kusaidia jamii kuinuka kiuchumi jijini hapa.

Mafunzo waliyopata ni pamoja na ushonaji, ufumaji, kutengeneza mkaa mbadala na mambo ya ujasiriamali.

Katika mpango huo unaoratibiwa na Kituo cha Sauti Jamii Kipunguni jijini Dar es Salaam, ulioanza mwaka 2018.

Akizungumza na Nipashe, Mwenyekiti wa kituo hicho Fatma Talib, wakati ufunguzi wa ofisi zao uliofanywa na Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, amesema kundi hilo limefanikiwa kujitegemea kiuchumi kutokana na miradi mbalimbali waliyoanzisha. Anafafanua kuwa kati ya vijana 3,650 waliopata mafunzo, 2,500 wanawake na wanaume 1,150.

Anasema wanawake waliopata mafunzo ya ujasiriamali, wameongoeza kufikia 1,600 na wanaume 280, na kutoka makundi maalum wako 120.

"Hapa pia bado wanawake wameendelea kuwa wengi kwa kufikia 82, wakati wanaume ni 38, inatokana na kukumbana na ukatili, wanajibidisha kujikomboa kiuchumi," anasema.

Mkurugenzi wa kituo hicho, Seleman Bishagazi anasema kuanzia mwaka 2017 kituo hicho hadi Juni mwaka huu, wasaidizi wa kisheria wa Kituo cha Sauti ya Jamii Kipunguni wamefanikiwa kufutilia kesi mbalimbali 385.

Anasema mfano matunzo ya mtoto ni kesi 48, utelekezaji wa familia kesi 51, migogoro ya ndoa kesi 42, ukatili wa kisaikolojia kesi 64, mashauri ya madai kesi 30, unyanyasaji kingono kesi 31 na vipigo kwa wanawake kesi 28," anasema.

Bishagazi anataja kesi nyingine kuwa ni mirathi zipo 28, migogoro ya ardhi kesi 16, vitisho kwa wanandoa kesi 21, ubakaji kesi 11 na rushwa ya ngono kesi saba, ambapo anasema jumla yake ni kesi 385.

"Lakini pia tumetoa elimu kuhusu uelewa wa haki kwa vikundi 23 ambavyo vimekuwa vikiripoti kesi za ukatili moja kwa moja namba



Waziri Gwajima (katikati) akielekezwa jinsi mafunzo ya ufundi cherehani wanavyofanywa.

za msaada wa kisheria WILDAF 116," anasema Bishagazi.

Anafafanua kuwa wamefikia mafanikio hayo kwa msaada wa wadau mbalimbali wanaotetea haki za binadamu wakiwamo Shiriki la Wanawake la Sheria na MAendeleo Afrika (WILDAF), Dawati la Jinsia na Watoto la Polisi, Ustawi wa Jamii na vikundi vya kijamii.

Bishagazi anawataja wadau wengine kuwa ni viongozi wa dini, wazee wa kimila, mangariba na ulinzi shirikishi, ambao kwa pamoja wametoa mchango kukabili vitendo vya ukatili nchini.

**OFISI ILIVYOJENGWA**

Mkurugenzi Bishagazi anasema jengo hilo, limejengwa kwa gharama ya Sh. milioni 11.9, ambao ni ujenzi wa gharama nafuu, na kwamba kuna ofisi moja na chumba cha kutolea mafunzo ya ufundi ya ujasiriamali.

"Sauti ya Jamii Kipunguni ina wanachama 28 na tulijiwekea mikakati ya kuwa na ofisi yetu miaka mitatu iliyopita na tukakubaliana kuweka akiba kidogo tangu mwaka 2017 ambayo inatokana na kazi tunazofanya," anasema.

Anataja kazi hizo kuwa ni pamoja na kuhudhuria mafunzo mbalimbali na kiasi cha fedha walichowezeshwa walitumia kununua kiwanja na maandalizi ya ujenzi.

"Kimsingi, tunaheshimu faida tunayopata kwenye miradi yetu ikiwamo mauzo ya mkaa, kukodisha maturubai, viti na marejesho tuliokubaliana na kwa yeyote anayepata fursa ya kushiriki mafunzo yenye posho," anasema.

Anafafanua kuwa pesa nyingine zimetokana na malipo wanayolipwa kutoka katika mashirika ambayo yanawapa tenda za kutoa mafunzo kwenye vikundi mbalimbali vikiwamo vya ujasiriamali.

"Kwa njia hiyo, tumefanikiwa kununua kiwanja cha robo heka kwa Sh. milioni 5, tukajenga kwa gharama ya Sh. milioni 6. 9, ambapo jumla ya gharama zote ni Sh. milioni 11. 9, ofisi ina huduma ya choo, maji, huku mfumo wa umeme ukiwa tayari umefanyika tunasubiri kuunganishiwa nishati hiyo," anasema.

**WAZIRI GWAJIMA I**

Waziri Dk. Dorothy anapongeza juhudi za kituo hicho akisema kinafaa kuwa mfano wa kuigwa, huku akirejea takwimu zilizopo kuhusu ukatili nchini kwamba, mwaka watoto 11, 499 walifanyia ukatili.

"Lakini 5,899 kati yao walibakwa, asilimia 60, ambayo ni zaidi ya nusu, walibakwa majumbani kwao na ndugu zao na pia watoto 1,114 asilimia 60 wakiwa wamelawitiwa majumbani mwao, asilimia 40 njiani wakienda shule, katika magari ya shule, shuleni au maeneo mengine," anasema Dk.Dorothy.

"Hapa ukigawanya kwa mwezi ni kama wastani wa waliobakwa ni 491, waliolawitiwa ni 93, lakini unaambiwa kwamba hao wote, wengi hawakutoa taarifa sehemu yeyote, bali ni asilimia 12 pekee waliripoti," anasema.

Waziri anaongeza kuwa kuwapo na mashirika mengi yasiyo ya kiserikali yanayopambana na ukatili huo ni hatua nzuri, na kuyataka yafanye kikamilifu kazi ili jamii iondokane na ukatili huo unaoacha makovu mioyoni kwa manusura.

"Ninaambiwa watu wananishangaa kila siku nipo mitaani, ninapita kutafuta kamati na asasi za kupambana na ukatili na ndiyo maana nimefanikiwa kukutana na Kituo cha Sauti ya Jamii Kipunguni," anasema.

Katika ufafanuzi wake, anaeleza kuwa alipofika kituoni hapo kwa mara ya kwanza mwanzoni mwa mwaka huu, ailivutiwa na vitu fulani fulani alivyovikuta ambavyo ni nadra kuvikuta sehemu nyingine.

"Wizara hii imeundwa kupambana na ukatili wa aina yoyote kwa watu wote wakiwamo watoto, nimevutiwa jinsi Kipunguni inavyofanya kazi, nisisitize umuhimu wa mabaraza ya watoto, madawati ya ulinzi wao shuleni na nje ya shule, nitazunguka kila kona kuyakagua kama yanafanya kazi," anasema.

Anasema atafanya kazi hata katika majumba ya watu, na kwamba akikuta kuna mtu anafanya ukatili, atamkamata huko huko na kumfikisha kwenye vyombo vya sheria, ili kukomesha vitendo hivyo katika jamii.

Waziri huyo anasema vita hiyo inahusisha jinsi zote na siyo upande mmoja, na kwamba wanaume ambao kila mara wamekuwa wakituhumiwa kuhusika na ukatili watakapotoka na kusema ukweli, hatua hiyo itasaidia kuokoa mabinti.



Mabinti na wanawake wa Kata ya Majohe wakichuma mboga kwenye moja ya bustani wanazosimamia baada ya kupata mafunzo ya ujasiriamali.

MAKALA

# Licha ya vita Urusi 'baba lao' kuuza chakula duniani

## -Tanzania imo imenunua ngano dola milioni 101

Na Mwandishi Wetu

UPATIKANAJI wa chakula katika dunia ya leo ndiyo changamoto kubwa ambayo mataifa yote hayana budi kuishughulikia, kwa mujibu wa taarifa ya Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa(FAO), idadi ya watu wanaokabiliwa na njaa duniani imeongezeka hadi milioni 828.

Wanakaribia bilioni moja huu si mchezo ni tatizo kubwa. Kinachoshuhudiwa sasa ni ukweli kuwa kama balaa hilo halitatatuliwa ifikapo mwaka 2030 ila hali halisi inaelekea kuwa mbaya zaidi, dunia inaweza isiwe mahali salama pakuishi.

Changamoto hii ya uhaba wa chakula na ugawaji wa chakula usio sawa itatatuliwa kwa kupanua biashara ya kimataifa kwa ajili ya kuwashawishi wazalishaji muhimu wa chakula wafanye mchango mkubwa zaidi katika masoko ya kimataifa.

Ukweli ni kwamba watu wapende wasipende lakini katika muktadha huu wajibu wa Urusi katika kuhakikisha upatikanaji wa chakula duniani upo na utabakia kuwa wa muhimu tena, unaelezwa kwamba umeongezeka.

La kufurahisha ni kwamba kwa miaka kadhaa iliyopita Urusi imeongeza ugavi wa chakula na ndiye muuzaji mkubwa wa bidhaa za kilimo kuliko taifa jingine duniani. Mwaka hadi mwaka imeendelea kukuza uzalishaji na usafirishaji wa bidhaa muhimu za kilimo.

Kwa mfano, uchambuzi wa takwimu ya forodha za Urusi, tangu mwaka 2013 zinaonyesha kuwa nchi hiyo imeongeza uuzaji wa bidhaa za kilimo kuanzia dola bilioni 16,3 hadi kufikia dola bilioni 37,1 kiwango ambacho ni maradufu.

Miongoni mwa kilichoongezeka ni nafaka, maharagwe, mafuta ya kula na nyama za aina mbalimbali. Sasa hivi Urusi imeshika nafasi ya kwanza duniani katika kuuza ngano ughaibuni huku ikiwa kwenye nafasi ya pili ya kuiuzia nchi mbalimbali mafuta ya kula na nafasi ya tatu ya kuuza shayiri.

Aidha, nchi hiyo iko mstari wa mbele katika kusafirisha maharage na samaki kwa masoko ya nje.Ni ukweli usiofichika kwamba ni taifa linalochangia upatikanaji wa chakula katika nchi za Asia na Afrika ambako inasafirisha zaidi ya nusu ya bidhaa zake.

Katika kipindi cha miaka mitano tangu 2017 hadi 2021 Urusi imeongeza uuzaji wa chakula kwa bara la Asia kwa asilimia 55 kufikia dola bilioni 14,3 na kwa Afrika kwa asilimia 24 hadi kufikia dola bilioni 4,5.

Hata leo mwaka 2022 inaendelea kuyalisha mataifa yanayokabiliana na janga la njaa kama Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Afghanistan, Ethiopia, Sudan, Syria, Nigeria, Yemen, Sudan ya Kusini, Pakistan na Haiti. Hivyo basi biashara yote ya bidhaa za kilimo za Urusi na nchi maskini duniani imeshazidi tani milioni 1.2 zenye thamani ya dola milioni 533,6.

Aidha, mwaka huu, Urusi imepeleka bidhaa za kilimo kwa nchi za Afrika kama vile Misri iliyopta tani milioni 2.3 zenye thamani ya dola bilioni moja, Algeria tani 381,000 thamani ya dola milioni 262.6, Libya tani laki 755,000 zenye thamani ya dola milioni 254.2, Tunisia tani 77, 000 zenye thamani ya dola milioni 58.2, Kenya 96,000 zenye thamani ya dola milioni 36 wakati Tanzania pia inanunua ngano za Kirusi ambayo thamani yake ilikuwa dola milioni 101 mwaka jana.

Hata hivyo, hali halisi katika soko la nafaka duniani inaendelea kubakia kwenye wasiwasi, mathalani, katika msimu wa 2022/23 mavuno ya mazao makuu ya ngano, shayiri na mahindi yanatarajiwa kupungua kwa tani milioni 36 wakati msimu uliopita ulifikia tani milioni 2,106.

Kadhalika Urusi inategemea kupata mavuno makubwa ya nafaka hizo zote tatu za ngano, shayiri na mahindi, ni kwa mujibu wa makadirio ya awali na kwamba nchi hiyo itavuna takriban tani milioni 140 za mazao hayo.



Rais wa Urusi, Vladimir Putin , nchi yake ndiyo mzalishaji mkubwa wa nafaka duniani, kuwa vitani kumesababisha upungufu mkubwa wa chakula kwenye mataifa tajiri na maskini. **PICHA: MTANDAO**

### VIKWAZO VYA NINI?

Viongozi wa nchi hiyo wanasema kuwa, kama ilivyo sasa, siku zijazo Urusi iko tayari kuhakikisha usambazaji wa kudumu wa chakula kwa masoko ya nje, ambayo ni mchango mkubwa kabisa katika kutatua tatizo la uhaba wa chakula katika mazingira ya kuongezeka kwa mahitaji ya chakula duniani kwa ujumla, na hasa katika Asia na Afrika.

Ni dhahiri kwamba vikwazo vyovyote vinavyozuia kusafirisha nafaka kutoka Urusi si kwamba vitasababisha ongezeko zaidi la bei za chakula bali pia vitaleta matokeo ya maafa kwa nchi nyingi zinazoendelea, hasa kwa bara la Afrika ambalo kihistoria linaitegemea Urusi kama muuzaji muhimu zaidi wa chakula.

Vikwazo dhidi ya mfumo wa kifedha wa Urusi vinapunguza uwezo wa mataifa mengine wa kufanya malipo kwa kufuatana na mikataba ya kibiashara, ikiwa ni pamoja na malipo ya kununua chakula. Changamoto hii inaathiri mno biashara ya Afrika kwani nchi za bara hilo zinategemea sana benki za Magharibi.

Kwa upande mwingine dunia isisahau kuhusu marufuku na vizuizi katika sekta ya uchukuzi. Matatizo hayo yameileta hasara zaidi sekta ya biashara ya kimataifa ambayo tayari imeshatikiswa na usumbufu wa minyororo ya ugavi wa bidhaa za kimataifa na kikanda kutokana na janga la UVIKO-19. Katika mazingira haya ya vikwazo kampuni za Magharibi za uchukuzi na bima zilikataa kuendelea kutoa huduma zao za kusafirisha mizigo ya Kirusi, kuingia kwenye bandari za Urusi na kufanya miamala ya bima na kampuni za Urusi.

**Kwa mfano, uchambuzi wa takwimu ya forodha za Urusi, tangu mwaka 2013 zinaonyesha kuwa nchi hiyo imeongeza uuzaji wa bidhaa za kilimo kuanzia dola bilioni 16,3 hadi kufikia dola bilioni 37,1 kiwango ambacho ni maradufu.**

Hata hivyo, licha ya vikwazo na marufuku nchi hiyo ya Urusi mwaka huu imeongeza uuzaji nje wa bidhaa zake za kilimo ambao thamani yake ilifikia dola bilioni 29,5 kuanzia Januari hadi Oktoba, kwa maneno mengine, uuzaji uliongezeka kwa asilimi 15 ikilinganishwa na kipindi kama hicho cha mwaka jana.

Takwimu pia zinaonyesha kuwa usafirishaji wa nje katika nchi za Magharibi ulipungua kwa asilimia 14 kwa dola milioni 948 na kufikia dola bilioni sita, wakati usambazaji kwa mataifa mengine yasiyoiwekea Urusi vikwazo uliongezeka kwa asilimia 25 (kwa dola bilioni 3.4) na kufikia dola bilioni 23.5.

Hii ndiyo ishara ya kwamba Urusi inaendelea kushirikiana kikamilifu na nchi marafiki zake ili kuhakikisha usalama wa chakula na utulivu katika maeneo yenye uhitaji zaidi wa huduma hiyo duniani unafikiwa.

TULIKOTOKA, TULIPO & TUNAKOKWENDA...

# Unakumbuka? Tishio Wanyonya Damu na taharuki yake kila kona

## • Likionekana gari jekundu, 'hao wamefika!'

**Na Adam Fungamwango**



TANGU miaka ya 1960 hadi mwishoni mwa miaka ya 1980 nchini Tanzania kulikuwa na uvumi wa kuwepo watu wanaoitwa 'wanyonya damu.'

Watu hao ambao wanafahamika kwa jina lingine la Mumiani, wanadaiwa wanavamia watu usiku hasa wale waliopenda kutembea usiku wa manane au walevi na kunyonya damu zao kwa kutumia vifaa walivyonavyo.

Ikadaiwa watu wanaofanya kazi hii hutumwa na watu wengine kutoka nchi za nje ambao huuza kwa bei kubwa.

Zikawa taarifa za kukutwa kwa miili ya watu wakiwa wamekufa huku ikiwa imegongwa mihuri kuonyesha kuwa marehemu kanyonywa damu.

Na ikawa inasemekana kuwa hata askari polisi wakiikuta maiti imepigwa mhuri basi hapo tena hakuna kesi, wanajua kuwa mtu huyo amenyonywa damu, hivyo wanawapa tu ndugu wakazike na kesi inaishia hapo.

Na wengi wa watu ambao walikuwa akisemwa kuwa ni wanyonya damu walikuwa ni watu wenye kipato. Hivyo kipato chao kuhusishwa na unyonyaji wa damu.

Pia wakawa wanahusisha kuwa wana mahusiano ya serikali kwa sababu damu inayopatikana nyingine pamoja na kuuzwa, iliyobaki inapeleka hospitalini kwenye akiba ya damu.

Ukikaa na watu wa zamani wana historia na hadithi nyingi za aina hiyo, kila mmoja atakusimulia kivyake lakini huwezi kukuta hata mmoja mwenye uhakika na anachokisema.

Kwenye mikoa au majiji yote nchini zipo hadithi hizo, na Dar es Salaam sehemu ambazo zilikuwa maarufu na uvumi wa wanyonya damu.

Sehemu hizo ni kama Buguruni, na Mwananyamala ambapo hata jina lenyewe maana yake ni 'mtoto nyamaza' kwa lugha ya kizaramo, kwani wakati huo ilikuwa ni porini tu na wakazi walikuwa wachache.

Kulikuwa na uhalifu wa kukaba watu, lakini wengi walihusisha na watu hao wanaoitwa 'mumiani'.

Kulikuwa na watu maarufu pande mbalimbali za nchi wakati huo hasa waliokuwa na uwezo mkubwa kipesa walikuwa wakihusishwa na kazi hiyo, wakiogopwa na baadhi ya akinamama na watoto.

Wakati mwingine hata mitaani tu, sokoni na sehemu zingine likionekana gari ambalo wana wasiwasi nalo na hasa lenye rangi nyekundu, basi watu wataanza kutimua mbio bila kuuliza na wakifika majumbani huzusha stori kuwa wamewaona wanyonya damu.

Twende kwenye miaka ya 1970 hadi mwishoni mwa miaka ya 1980, stori za mumiani zilihamia mashuleni.

Nako huko ndiyo balaa kwani ikionekana gari yenye rangi nyekundu, wanafunzi wanatoka madirishani na kukimbilia majumbani.

Kinamama nao wakiona hivyo, khanga mkononi wanakwenda mashuleni kuwawashia moto walimu kuwa wanashirikiana na mumiani kutaka kuwanyonya damu wanafunzi.

Wale watoro wakiona hivyo ndiyo hawaendi shuleni hata mwezi kwa madai kuna wanyonya damu.

Je ni kweli kulikuwa na watu wa aina hiyo? Ukweli ni kwamba hadi leo haijathibitika na zimekuwa ni stori za kufikirika kwani hakuna uthibitisho kamili.

Kulikuwa na watu fulani kwa sababu zao wanazozijua walitengeneza vitu kama hivyo kwa kuwatia watu hofu.

Ni kama zile zile tu imani za ushirikina. Watu wanaweza kutengenezewa hofu kuwa fulani ni mchawi wakamhofia kijiji kizima na kumchukia.

Wakati ule tatizo kubwa lilikuwa ni elimu. Leo hii utakuta matamasha makubwa ya wanafunzi wa shule za msingi na sekondari huku kukiwa na magari ya msalaba mwekundu wamepaki pamoja na wafanyakazi wake tayari kwa kutoa huduma. Ni kwa sababu hivi sasa si wanafunzi tu, bali hata wazazi wanajua kazi za msalaba mwekundu.

Wakati huo ilikuwa si rahisi kwani linapoonekana gari la msalaba mwekundu tu, basi watoto wote wanatimua mbio.

Magari yote yaliyokuwa na msalaba mwekundu yalikuwa yanaogopewa na watoto na hata baadhi ya watu wazima yakinasibishwa na vitu kama hivyo.

Hii ni elimu kubwa imefanyika na serikali imefanya kazi kubwa kuelemisha raia wake hadi leo hii kuona hata mtoto mdogo aliona watu wa msalaba mwekundu ni marafiki na watoa huduma ya kwanza.

Hivi leo tunaweza kujiuliza swali moja tu. Hivi kama wale waliokuwa wakiendesha magari ya msalaba mwekundu wangekuwa wana mpango kweli wa kufanya shughuli hiyo walikuwa na ulazima gani wa kuwa na aina ya gari ambalo linawafahamisha na watu wanakimbia?

Si ingekuwa rahisi kwao kuwa na gari hata la rangi ya bluu wakafanya kazi yao vizuri kwa sababu hawatokimbiwa na mwindo wanayoyataka hivyo kuwapata kirahisi.

Kwa nini wanyonya damu watumie gari jekundu ambalo likionekana kwa watu wanakimbia na wanapata shinda kuwakamata? Kwa nini wasiwe na gari ambalo watu hawatokuwa na wasiwasi nalo ili kazi iwe rahisi kwao?

Hapa unaona kabisa kuwa ilikuwa ni uvumi uliokuwa unavumishwa na watu kwa sababu wao binafsi wanazozijua wao kwa ajili ya kuitia hofu jamii, lakini hakukuwa na uweli wowote.

Kama kawaida kuna meseji za wadau kutoka kwenye mtandao ya kijamii baada ya mada hii kutambulishwa.

"Mimi nadhani zilikuwa ni propaganda tu za watu, hivi kweli inakuwaje utoe uhai wa mtu kwa ajili ya kuokoa uhai wa mti?" Aliandika mdau mmoja.

Mwingine akakumbushia kuwa kuna watu hasa watoro walikuwa wana tabia ya kulianzisha ili kuzua taharuki na kusababisha wanafunzi kukimbilia majumbani.

"Hadi hatuendi shule kisa gari jekundu, jamani, halafu saa ingine mmekaa darasani mnashangaa tu ka mtu kanawashtua, 'gari jekundu hilo', hizo mbio zake sio za nchi hii."

Wachangiaji mada hii kwenye mtandao walizidi kufunguka.

"Zilikuwa imani za kijinga tu sisi Mbeya kuna dokta mmoja miaka ya 1990 alikuwa anamiliki hospitali yake, watoto wa miaka hiyo tukimuona tunatimua mbio, eti ananyonya damu ili atengenezee vidonge. Ulikuwa ni ushamba tu na kukosa elimu, si unajua tatizo letu kubwa ni elimu, hata sasa kuna vitu ambavyo bado havijakaa sawa, mawazo ya wengi wetu yamejaa ushirikina shirikina mtu akifanikiwa tunamwita mchawi, hatuamini katika uwezo na matumizi sahihi ya akili na utashi kuleta mabadiliko." Mchangiaji huyo aliandika kwa hisisa kali.

Mama mmoja akaandika, akikumbuka mbali kwani ameshawahi kutimua mbio kwa sababu ya mumiani

"Nimekumbuka mbali, walikuwa wanatudanganya jamani, acha kabisa wanyonya damu hahahaha, aliyeanzisha fikra hizi hakika alikuwa mtu mbaya sana. Ilifika wakati tukawa tunaambiwa kuwa Ubongo wa watu ulitumika kutengeneza dawa za kutuliza maumivu." Baada ya kuanduika haya, mwanamke mwenzake ambaye naye alikuwa mtoto kipindi hicho akamjibu.

"Lakini huwa napata hisia kuwa baadhi ilikuwa wanasumbuliwa na wivu hadi kuibua uzushi kuchafua wenzao, ila walikuwa wakiwatuhumu watu ambao baadhi utajiri wao ulikuwa ni ule unaoleta mashaka." Hapo kuna mwingine akaongeza.

"Nadhani kuna watu walikuwa wanapata utajiri kwa sababu ya kula rushwa, pembe za ndovu, na kwa njia zisizo halali, halafu ukaletwa mpango tu wa kutengeneza mazingira nyekundu wanekane mumiani ili waogopwe na jamii wasifuatiliwe mambo yao."

Kuna stori ya waumini kutokea dirishani na kutimua mbio baada ya mchungaji wao kuteremka kwenye gari lenye rangi jekundu.

"Kule Rukwa kuna Mchungaji mmoja miaka hiyo alipewa lifti na gari lenye rangi nyekundu baada ya gari lake kupata hitilafu njiani, alipofikishwa kwenye kanisa alikokuwa anakwenda kutoa mahubiri, waumini wote walitokea dirishani kutokana na yeye kuteremka toka gari waliloamini ni la mumiani."

Mada hii inamaliziwa na mmoja wa waliokuwa anapenda sana tukio hili litokee ili wasiende shule.

"Binafsi nilikuwa napenda hizi habari za za wanyonya damu, maana nilikuwaga napata sababu ya kutoroka shule kihalali."

**Tuma meseji 0716 350534**

HABARI KIMATAIFA

## Jeshi la Rwanda lazidi kushtumiwa

**WASHINGTON,** MAREKANI

MAREKANI imelitaka jeshi la Rwanda (RDF) kuacha kuwasaidia wapiganaji wa msituni wa M23 katika mapigano baina yao na vikosi vya serikali ya Jamuhuri ya Kidemokrasia ya Congo.

Jeshi la Rwanda RDF halijatoa kauli ya wazi kuhusiana na shutuma hizo kutoka kwa Marekani dhidi yake. Hatahivyo awali Rwanda ilipinga madai ya kuwa na uhusiano na M23.

Alhamisi mapigano mengine yaliibuka baina ya wanajeshi wa serikali ya DRC na wapiganaji wa M23 katika barabara inayounganisha mji wa Goma ambao ni makao makuu ya jimbo la Kivu Kaskazini na miji mingine ya mashariki mwa nchi hiyo.

Waziri wa Habari wa DRC, ambaye pia ni msemaji wa serikali Patrick Muyaya, alisema kuwa nchi yake inashukuru msimamo uliochukuliwa na Marekani wa kulaani usaidizi unaotolewa na Rwanda kwa M23.

M23 walikuwa wakikana kusaidiwa na Rwanda. Katika mazungumzo ya awali na BBC, msemaji wake alisema hawapewi hata sindano ya msaada na serikali ya Rwanda. **BBC**

## Rais wa China kufanya ziara Saudi Arabia

**RIADH,** SAUDI ARABIA

WAZIRI wa Mambo ya Nje wa Saudi Arabia, Mwanamfalme Faisal bin Farhan, amekiambia kituo cha televisheni cha Al-Arabia kuwa Rais wa China Xi Jinping anatarajiwa kufanya ziara katika taifa hilo la ghuba. Aliyasema hayo jana baada ya mazungumzo na mwenzake wa China Wang Yi, katika mkutano ambao bin Farhan amesema umefanyika katika wakati muhimu.

Aidha, ofisa huyo mwandamizi wa Saudi Arabia alisema nchi yake iko katika hatua za mwisho ya maandalizi ya mkutano wa kilele baina ya China na mataifa ya Kiarabu. Ziara hiyo ya Xi Jinping nchini humo imetangazwa wakati taifa hilo la kifalme likiwa katika mvutano mkubwa na Marekani ambayo ni mshirika wake wa siku nyingi, baada ya shirika la mataifa yanayouza nje mafuta kwa wingi, OPEC+ linaloongozwa na Saudi Arabia kuamua kupunguza viwango vya uzalishaji, licha ya onyo kutoka Marekani. **DW**



Mwandamanaji wa Kipalestina akitumia kombeo kurusha mawe kuvuka mpaka wa Israel mashariki mwa Jiji la Gaza wakati wa mapigano na wanajeshi wa Israel kufuatia maandamano mpakani. **PICHA: AFP**

# Marekani yapata hofu Ukraine, Russia kutumia 'bomu chafu'

**WASHINGTON,** MAREKANI

RAIS wa Marekani ameelezea mashaka yake kuhusu maneno ya Rais wa Russia, Vladimir Putin, kwamba hana nia ya kutumia silaha za nyuklia katika vita vya Ukraine.

Putin alisema katika hotuba yake juzi kwamba Russia haijatishia kutumia silaha za nyuklia na ilijibu tu kuhusu usaliti wa nyuklia wa viongozi wa Magharibi.

"Kama hana nia, kwanini anaendelea kuzungumza kuhusu jambo hilo? Kwanini hazungumzi kuhusu uwezo wa kutumia silaha za kimkakati za nyuklia?" alisema Biden katika mahojiano na televisheni ya NewsNation.

Katika mahojiano na CNN, mratibu wa mawasiliano ya baraza la usalama la Ikulu ya White House, John Kirby alisema kuwa Russia huenda isizingatie matumizi ya "bomu chafu" na inabuni sababu ya kuilaumu Ukraine kwa bomu hilo.

Wakati huo huo, Kirby alisema kuwa nchi yake bado haijaona ishara zozote kuhusiana matumizi ya bomu la maangamizi.

"Mara kwa mara huwalaumu wengine kwa kile wanachokifanya au wanachokaribia kukifanya," Kirby alisema.

Amesemna hadi jana hawajaona dalili kuwa Warussia wanapanga kutumia bomu la aina hiyo au hata kuandaa.

Wakati huo huo, Rais wa Russia, Vladimir Putin anaendelea kukataa wazo la uhuru wa Ukraine, ambalo kimsingi haliendani na uwezekano wa mazungumzo kamili ya amani, wataalam wa Taasisi ya Amerika ya Utafiti wa Vita (ISW) waliandika katika taarifa yao.

Wakati wa hotuba katika mkutano wa klabu cha majadiliano na Putin aliendelea kukataa wazo la uhuru wa Ukraine, akisema kwamba dhamana pekee ya kweli ya uhuru wake inaweza kuwa Russia iliyounda nchi hiyo.

Putin alirudia kusema kuwa ni jambo la ukweli wa kihistoria kwamba Waukraine na Warusi kimsingi ni taifa moja ambalo liligawanywa katika majimbo tofauti.

Taarifa za Putin zinakataa ukweli wa kisheria kwamba Ukraine ni nchi huru, Shirikisho la Russia pia limetambua mamlaka ya Ukraine, na watu wa Ukraine wako kama taifa tofauti, inabainisha ISW.

Marudio ya Putin ya wazo kwamba Ukraine na Russia ni watu wamoja, wamegawanywa katika majimbo tofauti kutokana na hali ya kihistoria, inaonyesha lengo lake la kuharibu hali ya Kiukreni na kufuta dhana ya watu wa nchi hiyo.

Katika hatua nyingine, Rais Volodymyr Zelensky, alisema Russia imeanzisha mashambulizi zaidi ya 30 ya ndege zisizo na rubani nchini mwake katika muda wa siku mbili pekee.

Aliongeza kuwa kwa jumla Russia imefanya mashambulizi 4,500 ya makombora na zaidi ya mashambulizi 8,000 ya anga.

Akizungumza kutoka mji mkuu wa Kyiv, akiwa amesimama kando ya ndege isiyo na rubani ya Shahed ya Iran iliyoanguka, Zelensky aliahidi kukata mbawa za nguvu za anga za Russia.

Maofisa wa nchi za Magharibi wanaamini kuwa Iran imetoa idadi kubwa ya ndege zisizo na rubani kwa Russia, lakini nchi hiyo na Iran zinakanusha madai hayo.

Haya yanajiri huku Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani Antony Blinken akitaja matumizi ya fujo ya Russia ya ndege zisizo na rubani kuwa ya kutisha.

Mwanadiplomasia huyo mkuu wa Marekani aliwashutumu makamanda wa Russia kwa kutumia vifaa hivyo kuua raia wa Ukraine na kuharibu miundombinu wanayoitegemea kwa ajili ya umeme, maji na joto.

"Canada na Marekani zitaendelea kufanya kazi na washirika wetu na washirika wetu kufichua, kuzuia, na kukabiliana na utoaji wa silaha hizi kwa Iran," alisema Blinken.

Katika wiki za hivi karibuni, mashambulio ya Urusi yalilenga miundombinu ya kiraia ya Ukraine, na kuharibu usambazaji wa umeme na maji nchini humo wakati joto linapoanza kushuka.

**BBC**

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTELEWA NA CHETI



**SHADIDER AWAMY MAGWIRA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S3881/0537** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **AHMES SEKONDARI** mwaka **2019**. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha Polisi.
**Taarifa ya Polisi: DAR/URA/RB/411305/2022.**

## KUPOTELEWA NA CHETI



**BAHATI MOHAMED MKENGA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S1450/0521** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **EFATHA SEMINARY SEKONDARY SCHOOL** mwaka 2019. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha Polisi. **Taarifa ya Polisi: DAR/URA/RB/411401/2022.**

## KUPOTELEWA NA VYETI



**TOUMA NKWABI NG'WANAKILALA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0342/0076** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **SHAABAN ROBERT** Sekondari mwaka **1995**. Cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S0347-0159** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **TAMBAZA HIGH SCHOOL** mwaka 1998. Cheti cha Chuo chenye namba **15243** cha chuo cha **IFM** mwaka **2004.** Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi.
**Taarifa ya polisi: DAR/CHU/RB/422069/2022.**

## KUPOTELEWA NA CHETI



**ZENA CHRISTOPHER BUGHALI** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA CHETI CHA KIDATO CHA NNE CHENYE INDEX NAMBA S1520-0048 KILICHOTOLEWA NA BARAZA LA MITIHANI TANZANIA[NECTA] MWAKA 2011 KUPITIA SHULE YA SEKONDARI KISONDELA.YEYOTE ATAKAYEKIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHO KARIBU.**TAARIFA YA POLISI MBE/MBE/RB/274174/2022.**

## KUPOTELEWA NA VYETI




**NEEMA ALBERT** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S0784-0096 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **AIRWING** Sekondari mwaka 2003. Cheti cha kidato cha sita chenye index namba S0347/0853 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **TAMBAZA SEKONDARI** mwaka 2006. Cheti cha Chuo chenye namba 04606 cha chuo cha IFM mwaka 2009. Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi.
**Taarifa ya polisi: DAR/CEN/RB/416413/2022.**

## KUPOTELEWA NA CHETI



**THOMAS JACKSON MHUFU** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA CHETI CHA KIDATO CHA NNE CHENYE INDEX NAMBA **S0692-0114** KILICHOTOLEWA NA BARAZA LA MITIHANI TANZANIA [NECTA] MWAKA **2019** KUPITIA SHULE YA SEKONDARI **ROSMINI**. YEYOTE ATAKAYEKIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHO KARIBU.**TAARIFA YA POLISI TAN/KIL/RB/405144/2022.**

## KUPOTEA KWA VYETI



**YASINTA E KALUNDE** Anatangaza kupotelewa kwa cheti cha kuzaliwa, cheti cha kidato cha nne kilichotolewa na baraza la mitihani tanzania [**necta**] kupitia shule ya sekondari **WAKALANDA** chenye Index **No. S5683-0090-2019** na Result sleep **(kidato cha sita Nsimbo secondary)** school Index **No. S1800-0583-2022.**
**Taarifa ya Polisi: MOR/MOR/RB/421662/2022**

**FOMU YA MIRATHI-2**
**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya MOROGORO**
**KITUO CHA MJINI MKOA MOROGORO**

**Usimamizi wa Mirathi Na. 73/2022**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHENU**
**ISSA ALLY NGAYAMA WA NGOTO "B" KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOTOLEWA NA MUSSA ISSA NGAYAMA**

**TANGAZO / GAZETI**
(Kanunu ya 5 (2) kanuni za usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)
Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 3 / Mwezi 11 Mwaka 2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Zingatia;
Endapo kuna yeyeto mwenye Wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
* Wosia wa Marehemu huyu upo Mahakamani na waweza kukaguliwa
* Marehemu hakuacha wosia
* Futa isiyohusika

**Imetolewa leo tarehe 24 mwezi 10 mwaka 2022**

HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO MJINI
MOROGORO

**FOMU YA MIRATHI-2**
**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya MOROGORO**
**KITUO CHA MJINI MKOA MOROGORO**

**Usimamizi wa Mirathi Na. 78/2022**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHENU**
**EUNICE SOORI AYO WA KICHANGANI KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOTOLEWA NA FELIX RUMISHA OBEID**

**TANGAZO**
(Kanunu ya 5 (2) kanuni za usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)
Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 7 / Mwezi 11 Mwaka 2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Zingatia;
Endapo kuna yeyeto mwenye Wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
* Wosia wa Marehemu huyu upo Mahakamani na waweza kukaguliwa
* Marehemu hakuacha wosia
* Futa isiyohusika

**Imetolewa leo tarehe 28 mwezi 10 mwaka 2022**

HAKIMU

**FORM NO. 58**
**IN THE COURT OF DISTRIC T DELEGATE OF MOROGORO**
**DISTRICT AT MOROGORO**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 116 OF 2022**

**In Matter of the Estate of the Late REVOCATUS SENI MASANJA**

**By 1. CHARLES SENI MASANJA**
**2. .................................**

All Persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or latter of administration) is made to the above - named petitioner.
Objection to the grand should be field on or before the **16** day of **November / 2022.**
Dated at **Morogoro**, this **25th** day of **OCTOBER 2022**

RESIDENT MAGISTRATE

## KUPOTEA KWA RESULT SLIP

**ASELA RAYMOND KALAGANO** anatangaza kupotea kwa Result Slip ya kidato cha sita yenye index namba **S4419/0704** iliyotolewa na **LUKOLE SEKONDARI** mwaka **2022.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. **Taarifa ya Polisi: DAR/KIG/RB/420761/2022.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA - MWANZA**
**SHAURI NA 12B YA 2022**
**JEREMIAH JOHN MAHALU.......MLETA MAOMBI**
**DHIDI YA**
- **AZANIA BANK LTD**
- **DAVID CHIGULU........WAJIBU MAOMBI**

**KWA: DAVID CHIGULU**
Unafahamishwa kwamba mleta maombi hapo juu amefungua Shauri / Ombi dhidi yako katika Baraza la Ardhi na Nyumba Mkoa wa Mwanza, Ombi hili limepangwa kutajwa tarehe 01/12/2022 katika chumba cha Baraza, Barabara ya Makongoro jengo liko mkabala na Mahakama ya Mwanzo Mwanza mjini Tanzania.
Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria katika Baraza siku hiyo wewe mwenyewe, wakili wako au mtu mwingine anayeruhusiwa kisheria.
KAA- ukijua kwamba kushindwa kufika, Baraza hili tasikiliza ombi hilo na kutoa uamuzi bila wewe kuwepo.
Imetolewa nami kwa Amri na Chapa ya Baraza leo tarehe 18/10/2022.

**MURIRYA N.** MURIRYA N.
**MWENYEKITI**
**18/10/2022.**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**PAULO STEVEN KOLE** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki aina ya **BOXER** yenye namba za usajili **MC 841 BJG.Engine No. PFZWGC20310. Chassis No. MD2AIBZ3GWC97415.**Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. **Taarifa ya polisi: DOD/DOD/RB/419211/2022.**

**Form No. 2B**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA KIGOMA**
**MAHALI.........KIGOMA......MAOMBI....69....MWAKA ..2019**

**THE REGISTERED TRUSTEES OF ROMAN CATHOLIC DIOCESE OF KIGOMA.........MWOMBAJI**
**DHIDI YA**
**OLAF KABOBOYE (MSIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHEMU LEORNAD M KABOBOYE)..............**
**MJIBU MAOMBI WITO/KUITWA SHAURINI**

**KWA: OLAF KABOBOYE(MSIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHEMU LEORNAD M. KABOBOYE**

**POPOTE ULIPO**
Fahamu kwamba shauri hili limepangwa kutajwa/Kusikilizwa tarehe. 07........Mwezi...11...Mwaka..........2022...Saa...2:30 Asubuhi mbele ya Mheshimiwa M. Mwinyi...Mwenyekiti wa baraza. Hivyo unaamriwa kuhudhuria mbelel ya Baraza siku hiyo bila kukosa.
AMRI hii imetolewa kwa mkono wangu na Lakiri/Muhuri wa Baraza hili leo tarehe 07....Mwezi ...09....Mwaka....2022

MWENYEKITI

**IN THE DISTRICT COURT OF KIGOMA**
**AT KIGOMA**
**CIVIC CASE No. 9 OF 2022**
**GIDION RUHAZA LUBUNDI t/a RUHAZA ENTERPRISES...PLAINTIFF**
**VERSUS**
**SAMWELI KIBINA LUTAMBI.......1ST DEFENDANT**
**M/S LGNA COMPANY LIMITED .......2ND DEFENDANT**

**TO: 1. SAMWELI KIBINA LUTAMBI**
**2. M/S LGNA COMPANY LIMITED**

**NOTICE OF DATE OF MENTION/HEARING**

**TAKE NOTICE** that the above case has been fixed for mention on 1st day of November, 2022 at 08:30 am before Hon. Eva Mushi, SRM
YOU ARE required to appear in this Court on the fixed date without fail.
**GIVEN UNDER MY HAND** and **SEAL** of the Court this......day of .....2022

EVA MUSHI
......................................
**EVA MUSHI**
**SENIOR RESIDENT MAGISTRATE**

## KUPOTEA KWA KADI ZA PIKIPIKI

**KINGLION INVESTMENT CO. LIMITED** INATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI ZA PIKIPIKI ZENYE NAMBA ZA **USAJILI MC 876 DKM; MC 664 DNJ; MC 776 DBL.** YEYOTE ATAKAYEZIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI. **TAARIFA ZA POLISI: IRI/IRI/RB/420129/2022; IRI/IRI/RB/420130/2022; na IRI/IRI/RB/420131/2022.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA (MAHAKAMA)**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO ENABOISHU WILAYA YA ARUMERU**
**SHAURI LA MADAI NA 85 YA 2022(BREAK MASS LUGENDO)**
**Ayazkao Microfinance TLD MDAI**
**Dhidi ya**
**Richard Birika MDAIWA/MSHTAKIWA**
**HATI YA KUITWA SHAURINI (SUMMOS GENERAL)**
**(MCA Na.2/1984)**

**Kwa Richard Birika wa Arusha**
**Kwa kuwa umelazimika uhudhurie mahakamani ili ujibu shtaka /madai kuwa shahidi kama ifuatavyo**
**Fika mahakamani bila kukosa.**

**UNAAMRULIWA NA JAMHURI** uhudhurie mbele ya mahakama hii siku ya Alhamisi tarehe 3/11/2022 saa 3:00 asubuhi au mara baada ya hapo ili shauri hili liweze kusikilizwa.

**USIKOSE KHUDHURIA**
Fahamu ya kwamba ukikataa kupokea hati hii na kuweka sahihi yako au ukipokea na kuacha kuhudhuria mahakamani ni kosa K/f Na.114 A Sura 16 K/A. Hivyo mahakama inaweza kukuchukulia hatua kali za kisheria.
HATI HII IMETOLEWA NA AMRI YANGU NA MUHURI WA MAHAKAMA HII LEO TAREHE 18/10/2022

HAKIMU

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM II**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**

Katika mahakama ya mwanzo: **PONGWE**
Ombi la **JUMAA ATHUMANI JUMAA** kuteuliwa Msimamizi wa Mirathi ya Marehemu **ATHUMANI JUMAA**
Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa Kuja kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 14.11.2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa.

**Tarehe 14. 11. 2022**

**Sahihi ya Hakimu**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**KANDA DODOMA**
**SHAURI LA MIRATHI NA.4/2022**
**MATALA MORICE MANYAMA............MWOMBAJI**
**MAREGESI BENJAMIN MANYAMA .... MAREHEMU**
**KWA: YEYOTE**

**POPOTE PALE ULIPO.**
**YAH: TAARIFA YA KUTAJWA KWA MAOMBI YA USIMAMIZI WA MIRATHI NA 4/2022 MAHAKAMA KUU YA TANZANIA DODOMA MAREHEMU MAREGESI BENJAMIN MANYAMA**
**UNAFAHAMISHWA KWAMBA;** shauri tajwa hapo juu litatajwa Mahakama kuu Tanzania, Kanda ya Dodoma, mbele ya Mhe. G. J Mdemu, Jaji wa Mahakama kuu ya Tanzania Dodoma,saa tatu (3:00) kamili asubuhi siku ya Alhamisi tarehe 24/11/2022.
**HIVYO BASI;** unatakiwa ufike wewe mwenyewe au Wakili wako siku hiyo iliyotajwa bila kukosa.
**NA ENDAPO**; hutofika wewe mwenyewe au wakili wako siku hiyo iliyotajwa inatosha kumaanisha kwamba shauri hili litashughulikiwa na Mahakama kama itakavyoamua pasipo wewe au wakili wako kuwepo
**IMETOLEWA;** kwa mkono wangu na Mhuri wa Mahakama hii leo tarehe 24 mwezi wa Oktoba,2022.

NAIBU MSAJILI
MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
DODOMA

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**TANGA**
**SHAURI LA KUKAZIA HUKUMU NA. 30 LA 2022**
**AZIZA NKUNGU & ANOTHER......... MDAI**
**DHIDI YA**
**BAYPORT FINANCIAL SERVICE (T) LTD......WADAIWA**
**MRUFAANIWA:BAYPORT FINANCIAL SERVICE (T) LTD**
**KUITWA SHAURINI**
Mwombaji amefungua shauri dhid yako mbele ya mahakama kuu ya Tanzania-Tanga. Shauri limepangwa kusikilizwa tarehe 2/11/2022 saa tatu asubuhi.
Hivyo basi unatakiwa kuhudhuria wewe mwenyewe au wakili wako kwa tarehe iliyopangwa. Endapo hautahudhuria sahuri hili litasikilizwa upande mmoja na kutolewa uamuzi.
Imetolewa na kutiwa Saini na muhuri wa mahakama kuu ya Tanzania – Tanga leo tarehe 21/10/222

KAIMU NAIBU MSAJILI
TANGA


**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# HADITHI

MAWENI ni moja kati ya vijiji nchini ambavyo vipo mbali na makao makuu ya mkoa. Kutokana na kuwa vipo kilometa nyingi, miundombinu yake na mawasiliano yamekuwa hafifu, kitu ambacho kimewapa baadhi ya viongozi wa kijiji kufanya wanavyotaka. Wameingia mkataba wa kitapeli na kinyonyaji na tajiri aliyejifanya mwekezaji, kuwanyang'anya mashamba wanakijiji na kumuuzia. Badala yake wanakijiji wanalima kwenye ardhi aliyouziwa mwekezaji huyo. Mazao yaliyopatikana anayachukua na kuwalipa wanakijiji hao pesa kidogo ambayo haiwatoshi kujikimu kwa msimu mzima. Tajiri, watoto wake na viongozi wa kijiji pia wamekuwa na tabia ya kunyanyasa kijinsia watoto wa kike. Mary, ni mmoja wa wasichana warembo kijijini hapo ni mmoja waliopata shida hiyo. Hawana pa kupeleka malalamiko, wala wa kumlilia, isipokuwa Mungu tu. Fuatana na mtiririko wa kisa hiki.

# MTAKE MSITAKE-3

**Na Adam Fungamwango : (0716 350534)**




Awali hakutaka kabisa kuifanya kazi ile. Lakini yeye ndiye alikuwa mkubwa, ndugu zake aliofuatana nao kuzaliwa walikuwa ni wanawake, hivyo mama yake alimwambia kama asipokwenda basi hakukuwa tena na mtu wa kwenda kumchukua bibi yake ambaye ni mgonjwa.

"Bibi yako ni mgonjwa sana, kwa hiyo mimi na baba yako tumekuchagua wewe uende nyumbani. Uende kijijini ukamchukue bibi yako. Tunaona kama kule inawezekana matibabu ni ya shida kuliko huku. Hapa anaweza kupata matibabu ya uhakika na kwa uwezo wa Mungu atapona," akamkumbuka mama yake jinsi alivyomuagiza.

Akamuonya pia kutojiingiza kwenye migogoro isiyomhusu.

"Kule ni kwetu sisi, mimi na baba yako tumetoka kule, lakini wewe na ndugu zako mmezaliwa Dar, kule hamjulikani sana, tangu mko wadogo mlikuwa mnakwenda wakati wa likizo tu, kwa hiyo ukifika huko ujiepushe sana na mambo yasiyokuhusu."

"Kwa nini mama unasema hivyo, kwani umeona mimi ndiyo mtu wa kufuatilia vitu visivyonihusu?"

"Hapana, mimi nakufahamu mwanangu kuliko wewe unavyojifahamu. Wewe una huruma sana hupendi kuona watu wananyanyasika au kuonewa, unaweza kukutana na kitu kama hicho huko, ukataka kufanya kama huku, lakini mazingira ya huko na ya huku siyo sawa, unaweza kupata matatizo makubwa kabla hujatatua tatizo la msingi la kumleta bibi yako." Mama akamuonya.

Hayo ni moja kati ya maneno machache anayoyakumbuka Adel kabla hajatinga kwenye kijiji kile.

Alifika nyumbani kwa bibi yake, lakini hali aliyoikuta haikuwa tena ya kumchukua na kumpeleka Dar es Salaam.

Akaamuru wajomba zake wampeleke kwenye zahanati ili afya ya bibi iimarike.

Ndiyo kipindi ambacho anakutana na mkutano wa wanakijiji. Kwa sababu ndugu zake wengi walikuwa wamempeleka bibi zahanati, yeye na ndugu mmoja wakaamua kwenda kwenye mkutano huo.

Na hata baada ya hapo hakujua kama watu walikuwa wanamfuatilia na baada ya kuona kuwa hana madhara wakamuacha aendelee na shughuli yake iliyomleta.

**"He, umejuaje jina langu wakati wewe mgeni?"**

Adel hakutilia maanani yote aliyoyasikia kwenye mkutano ule japo alikuwa anapiga makofi sana. Jicho lake lilikuwa kwa mtu mmoja tu. Kwanza alishangaa amefikaje kule kijijini? Hakuonekana kama ni mtu wa kule bali aliende tu kama yeye. Alikuwa anawaza kuwa hata kama angemchukua na kumpeleka Dar vile vile alivyo bila kumuongezea kitu chochote, angewazidi wasichana wengi ambao wangepelekwa saluni za gharama na kupambwa kwa nakshi mbalimbali hata kwa masaa 12.

"Hivi mjomba Fotu, kuna msichana mmoja kule kwenye mkutano alikuwa amevaa jinsi na fulana ya kijani ni nani?"

Kilifuatiwa kicheko cha mzaha kutoka kwa aliyekuwa anaulizwa.

"Nilijua tu, yaani labda kama ungekuwa hujamuona, lakini kama umemuona ni lazima ungeuliza tu. Mjomba yule anaitwa Mary, ndiye mrembo mwenyewe wa kijijini hapa, kila mwanaume, kila mvulana anamtaka, kapiga chini hadi mwekezaji Usonzo, analialia tu."

Adel akatabasamu. "Ni kweli ni mrembo wa hapa, hajaolewa?"

"Bado msichana mdogo yule, ila ana mchumba wake anaitwa Enock."

*****************************

Ulikuwa mchana wa jua kali. Adel Adam alikuwa anazunguka kijijini hapo peke yake kwa kile alichokiita kunyoosha miguu.

Akiwa kwenye barabara isiyo na lami kwa mbali kidogo aliona mtu akija. Kutokana na jua kali lililokuwa likimpiga usoni hakujua ni nani. Alibaki akitembea kwa hatua fupi fupi na taratibu. Lakini kila kiumbe yule alipokuwa akikaribia ndiyo hamu ya kutaka kumuona ilizidi kumshika.

Alipofika karibu alikumbuka kuwa ameshawahi kukutana na mtu huyo. Hakuwa mwingine ni yule msichana. "Anaitwa nani vile, Mary." Akakumbuka na kujijibu mwenyewe.

Ilibaki hatua sita ili wapishane. Macho yake walimuangalia mrembo yule kwa namna ambayo hakutaka ajulikane kama anamwangalia.

Lahaula, alipompiga jicho tu, macho yao wote yalikutana. Ni kwamba hata Mary naye alikuwa akimtazama Adel.

Hakukuwa na kizuizi tena. Ilibidi Adel amsalimie "Hujambo Mary?"

Sekunde kadhaa zilipita bila kujibiwa, kiasi kwamba alianza kuhisi kama msichana hakupendezwa na salamu ile.

"He, umejuaje jina langu wakati wewe mgeni?"

Kumbe badala yake kujibu, Mary alipatwa na mshtuko mdogo, ni kwa nini mgeni yule amelijua jina lake mapema kiasi hicho. Ni nani aliyemwambia, na kwa nini hajalisahau.

"Nilisikia wanakuita." Akadanganya.

"Nani walikuwa wananiita?"

"Rafiki zako." Akajibu Adel. Wakati huo wote wawili walikuwa wamesimama katikati ya jua kali.

Mary akatabasamu. Tabasamu lililoonyesha kuwa hakukubaliana na jibu lile. Ndipo Adel alipozidi kuuthaminisha uzuri wa msichana yule.

Wakati huo ulisikika muungurumo wa bodaboda ambayo ilikata kona ghafla. Kwa bahati mbaya, Adel na Mary aliposimama ilikuwa ni karibu na kona hiyo.

Mwendeshaji alikata kona kwa kasi na akili yake haikumtuma wala kudhani kama anaweza kukutana na watu au watoto kwenye kona.

Ilipokata tu ilielekea kwa Mary. Alikuwa ameshika kikapu. Adel tayari alihisi hatari. Tayari dereva wa bodaboda alianza kuhamanika baada ya kuona kuna watu na kwa spidi aliyonayo hawezi kusimama.

Ktendo bila kuchelewa, Adel ambaye alisimama kando kidogo na Mary, alisogea hatua moja kubwa, akamshika mkono Mary kwa nguvu na kumvuta kule alipo.

Ni kati hiyo, bodaboda ilipita pale aliposimama Mary, lakini dereva alikuwa ameshaanza kuyumba baada ya kukuta kuna watu kwenye kona. Dereva na bodaboda yake aliangukа kwenye kichaka karibu na mtu wa mkorosho.

Nguvu ya mkono wa Adel ilimvuta Mary hadi alikosa balansi na kutokana na tishio la kugongwa alipatwa na mshtuko, kiasi cha kuzuiwa kifuani.

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

# SIMBA YAINGIA MKATABA MNONO NA MO ASSURANCE

**Na Saada Akida**

KLABU ya Simba imeingia mkataba wa miaka minne na kampuni ya Mo Assurance, kwa ajili ya matibabu ya wachezaji, benchi la ufundi na waajiriwa wote wa klabu hiyo.

Akizungumza wakati wa kutia saini makubaliano hayo, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Simba, Barbara Gonzalez, alisema ukiacha mkataba huo, klabu itakuwa inapata sh. milioni 250 kila mwaka.

**Alisema, bima hiyo ita hudumia pia watu wanne wa nyongeza kutoka kwa familia za wafanyakazi hao wa Simba pamoja na kugharamia misiba na huduma ya uzazi.**

"Hii itawahusisha timu ya wakubwa ya Simba, timu ya vijana, Simba Queens ambapo muajiriwa atakuwa na nafasi ya mke au mume na watoto wanne," alisema.

Barbara alisema, mkataba huo umeokoa zaidi ya sh. milioni 300 kwa klabu ambazo zilikuwa zinatumika katika matibabu ya wachezaji kwa kila mwaka.

Mkurugenzi wa Masoko wa Mo Assurance, Fatma Dewji alisema walikuwa na mazungumzo ya muda mrefu na klabu ya Simba ili kuwapa urahisi wachezaji wanapokuwa katika majukumu yao.

Fatma aliongeza kuwa, kama kuna klabu nyingine ambayo itahitaji makubaliano hayo wapo tayari kukaa mezani na kulizungumza hilo.



Vijana wakiwania mpira wakati walipokuwa wakifanya mazoezi katika Uwanja wa Oysterbay Polisi mkoani Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## *Listening Part' ya Town Classic Gwambina leo*

**Na Sabato Kasika**

BENDI mpya ya muziki wa dansi ya Town Classic, inatarajia kutoka mafichoni leo na kufanya onyesho la kwanza, ambalo ni maalum kwa ajili ya kuwasikilizisha mashabiki wa muziki huo nyimbo zake leo

Meneja wa bendi hiyo, Andrew Sekidia, ambaye pia ni mpiga kinanda, amesema onyesho hilo litafanyika leo katika ukumbi wa Gwambina Lounge, ambao zamani ulijulikana kama TCC Club Chang'ombe Dar es Salaam.

"Tunafanya onyesho la 'Listening Part' ili mashabiki wa muziki wa dansi wapate nafasi kusikiliza nyimbo zetu, kushuhudia kikosi kizima cha Town Classic na pia kupata maoni yao," amesema Sekidia.

Sekidia ametaja baadhi ya nyimbo za bendi hiyo ambazo zitapigwa kwenye onyesho hilo kuwa ni 'No Stress, Shem Darling' na nyingine zilizoandaliwa kwa muda wa mwezi mmoja wakati bendi ikiwa kambini Dar es Salaam.

"Baada ya listening part, bendi yetu itajipanga kwa ajili ya onyesho katika Uwanja wa Jamhuri mjini Morogoro wakati wa pambano la ngumi kati ya Twaha Kiduku na bondia kutoka Argentina," amesema.

Amefafanua kuwa bendi yao inamilikiwa na kampuni ya MO Green International Sports Promotion na kwamba katika onyesho la Morogoro itashirikiana na bendi ya Waluguru Original ya mjini humo.

"Listening part tutakayofanya, ndio itaonyesha mwelekeo wa bendi yetu na ninaamini italeta upinzani mkali kwa bendi nyingine, kwani kampueni ya MO Green International ilijipanga kabla ya kuanzisha," amesema.

Meneja huyo amesema uongozi wa kampuni yao umeanzisha bendi hiyo, ili kupiga muziki wa ushindani, kwa lengo la kuinua na kurejesha hadhi na heshima ya dansi kama ilivyokuwa miaka ya nyuma.

## Polisi, Dodoma mechi ya kisasi

**Na Hadija Mngwai**

MECHI ya Polisi Tanzania dhidi ya Dodoma Jiji inatarajiwa kuwa ya kisasi, jasho na damu baada ya timu hizo mbili kuwa katika mstari wa hatari kwenye msimamo wa Ligi Kuu Bara ambapo kila upande unahitaji kujikwamua kutoka katika nafasi iliyokuwepo.

Polisi itaikaribisha Dodoma katika mchezo wa Ligi Kuu Bara utakaochezwa Uwanja wa Ushirika Moshi, Novemba Mosi mwaka huku zikipambana kujinasua kutoka mkiani.

Polisi inashika nafasi ya 15 huku Dodoma ikiwa nafasi ya 16 na zote zinapambania kujikwamua kutoka nafasi hizo, huku zikiwa zimetimua makocha wao wa awali.

Timu ya Polisi ilimtimua kocha wake Mrundi, Joslin Sharrifu na Dodoma imemtimua, Masoud Djuma.

Akizungumza na Nipashe, Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiriano ya Polisi Tanzania, Frenk Rukwalo amesema kuwa, mchezo wao huo utakuwa na upinzani mkubwa kutokana na timu zote kutokuwa katika nafasi nzuri.

"Tumejipanga vyema kuhakikisha tunafanikiwa kushinda mchezo wetu dhidi ya Dodoma kwani tunajua wapinzani wetu watakuwa na upinzani kwa kuwa na wao hawako katika nafasi nzuri.

"Tunahitaji kujikwamua kutoka katika nafasi tuliyopo ili tuweze kuwa juu na kumaliza mzunguko wa kwanza katika nafasi nzuri kwa kuutumia vyema uwanja wa nyumbani.

"Kwa sasa timu ipo chini ya kocha wa viungo, John Tamba huku tukiwa tunaendelea na mchakato wa kusaka kocha mwingine, tunatumia muda huu kujiimalisha ili kutwaa pointi tatu katika michezo yetu ijayo," alisema Rukwalo.

## Yondani hana hofu na Yanga

**Na Shufaa Lyimo**

MCHEZAJI wa Klabu ya Geita Gold, Kelvin Yondani amesema yupo fiti kuvaana na matajiri wake wa zamani Yanga katika mchezo wa leo.

Akizungumza na gazeti hili alisema Yanga ni timu ya kawaida kama zilivyo timu nyingine hivyo hana hofu kukutana nayo.

"Nimejipanga vizuri kukutana na timu ya Yanga nitafuata maelekezo niliyopewa na benchi langu la ufundi nikishirikiana na wachezaji wenzangu," alisema Yondani.

Alisema mchezo huo utakuwa mgumu na wa ushindani kutokana na aina ya wachezaji wa timu zote mbili.

Mchezaji huyo alisema Ligi msimu huu ina ushindani kwani kila moja imejipanga kupata pointi tatu kwenye kila mchezo.

Alisema mchezo uliopita dhidi yao na timu Ruvu Shooting ulikuwa mgumu licha ya kufanikiwa kutoka na pointi tatu.

Alisema mazoezi waliyoyafanya yatawasaidia kupata matokeo mazuri katika mchezo huo ambao unasubiriwa kwa hamu kubwa.

## ZISIKUPITE

### MUDRYK AWINDWA
MKURUGENZI wa michezo wa Shakhtar Donetsk, Carlo Nicolini amesema Arsenal na Manchester City ni miongoni mwa Klabu kadhaa zilizotaka kumnunua mshambuliaji wa Ukraine, Mykhaylo Mudryk mwenye umri wa miaka 21, ambaye anaweza kugharimu zaidi ya euro 100 ambayo Manchester United ililipa Ajax kumnasa mshambuliaji wa Brazil, Antony. (***Calciomercato.it, via Mirror***)

### ALMIRON MKATABA MPYA
KLABU ya Newcastle United inatarajiwa kumpa mchezaji wa kimataifa wa Paraguay, Miguel Almiron mwenye umri wa miaka 28 mkataba mpya baada ya kuimarika kwake chini ya kocha, Eddie Howe. (***Telegraph***)

### HOJBJERG KUONGEZEWA
KIUNGO wa kati wa Denmark, Pierre-Emile Hojbjerg pia yuko mbioni kuongezewa mkataba mpya, huku Tottenham Hotspur ikionesha kuwa wanataka kuanza mazungumzo juu ya masharti mapya ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27. (***Times***)

### EDWARDS ATAKA KURUDI ENGLAND
KIUNGO wa mshambuliaji wa Sporting Lisbon, Marcus Edwards mwenye umri wa miaka 23 amesema uhamisho wa kwenda Ureno umekuwa mzuri kwake, lakini angependa kurejea kucheza katika nchi yake ya England. ***(Evening Standard)***

### FULHAM YAKOMAA NA MAIA
KLABU ya Fulham imewasilisha ombi la pili kwa kiungo wa kati wa Brazil, Pablo Maia mwenye umri wa miaka 20 na pia wanawafuatilia viungo wa Sao Paulo, Rodrigo Nestor mwenye umri wa miaka 22 na Igor Gomes mwenye miaka 23, pamoja na beki wa kati Luizao mwenye miaka 20. (HITC)

### FOREST PIA INAMTAKA
KLABU ya Nottingham Forest pia wanavutiwa na Pablo Maia na wako tayari kulipa bei ya pauni milioni 9 kwa kinda huyo wa Brazil. (***Nottinghamshire Live)***

### MAN YAWINDA MAKIPA
KLABU ya Manchester United inamfuatilia mlinda mlango wa Porto na Ureno, Diogo Costa mwenye umri wa mika 23, na mlinda mlango wa Athletic Bilbao na Hispania, Unai Simon mwenye miaka 25, wakati ikisubiri kuamua iwapo wataongeza mkataba wa mchezaji wa kimataifa wa Hispania, David de Gea mwenye miaka 31. ***(Athletic***)

### ABOUKHLAL ANYATIWA
KLABU za Southampton na Leicester City zinamfuatilia kwa karibu nyota wa Toulouse na mchezaji wa kimataifa wa Morocco, Zakaria Aboukhlal mwenye umri wa miaka 22. Winga huyo anatarajiwa kushiriki michuano ya Kombe la Dunia nchini Qatar. (***Echo***)

### EMERY KUIMARISHA KIKOSI
KOCHA mpya wa Aston Villa, Unai Emery atapewa fedha nyingi kuimarisha kikosi chake wakati wa dirisha la usajili la Januari. (***Football Insider)***

### NUNEZ ALIMUULIZA SUAREZ
MSHAMBULIAJI wa Liverpool, Darwin Nunez mwenye umri wa miaka 23 amesema mchezaji mwenzake wa Uruguay, Luis Suarez mwenye miaka 35, ambaye pia aliichezea Liverpool aliwasiliana naye ili kumpa ushauri wa jinsi ya kukabiliana na presha ya kucheza Ligi kuu England. ***(ESPN***)

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# TEN HAG: RONALDO ATAFUNGA ZAIDI

## Asema kiwango chake kinaimarika na anaweza kufunga mengi zaidi...

**MANCHESTER,** England

CRISTIANO Ronaldo atafunga zaidi mabao baada ya kufunga akirejea kwenye kikosi cha Manchester United kilichoibuka na ushindi wa 3-0 dhidi ya Sheriff kwenye Ligi ya Europa juzi, kwa mujibu kocha, Erik Ten Hag.

Ronaldo alitolewa nje kwenye sare ya Chelsea mara ya mwisho baada ya kukataa kuonekana kama mchezaji wa akiba wakati wa mchezo uliopita dhidi ya Tottenham, lakini alifunga kwenye ushindi huo na kuwafanya Mashetani Wekundu hao washike nafasi ya pili katika Kundi E.

Lilikuwa bao la kwanza la nyota huyo wa Ureno msimu huu kwenye uwanja wa Old Trafford na Ten Hag, ambaye alishuhudia Diego Dalot na Marcus Rashford pia wakifunga, na sasa anatarajia mabao mengi zaidi yatakuja.

**"Kuona Ronaldo akipata bao lake ilikuwa nzuri," alisema Ten Hag wakati wa mahojiano yake baada ya mechi na BT Sport.**

"Alitengeneza, timu ilimtengenezea, na tunajua ana uwezo wa kumalizia. Alihitaji bao na sasa nina imani kutakuwa na mabao mengi kutoka kwake.

"(Uchezaji wa timu) ulikuwa sawa. Bila shaka, unatumaini atafunga katika kipindi cha nusu saa, kwa hiyo ilichukua muda mrefu, lakini tulistahili bao hilo.

"Kipindi cha pili, tulifunga mabao mengine mawili mazuri kutokana na mchezo wa wazi na nimefurahishwa na bao safi kwa sababu hatukutoa chochote. Ulikuwa ushindi wa umakini."

Kocha huyo pia alitetea uamuzi wake wa kumtoa Antony wakati wa mchezo ukiwa bado hakuna bao lolote kabla ya mapumziko.

Alipoulizwa sababu ya kumtoa winga huyo wa zamani wa Ajax, Ten Hag alijibu: "Nilitaka kuona Marcus na Cristiano wakiwa karibu pamoja, na wenye nguvu upande wa kulia."

United sasa inahitaji ushindi wa angalau mabao mawili dhidi ya vinara wa kundi lao la E, Real Sociedad wiki ijayo ili kutinga hatua ya 16 bora.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,044,3

MECHI KALI
LIVERPOOL
VERSUS
LEEDS
1 | 1.27
X | 5.78
2 | 8.17

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa
vodacom m-pesa
airtel money
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
18+
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# DESCHAMPS AWAONYA POGBA, VARANE



**PARIS, Ufaransa**

DIDIER Deschamps amewataka Raphael Varane na Paul Pogba kuthibitisha kuwa wanaweza kutoa mchango kwenye kombe la Dunia Qatar 2022 baada ya kutangaza kuwa hatapeleka wachezaji ambao ni majeruhi.

Bosi huyo wa Ufaransa alisema kila mmoja atakayesafiri kwenda kwenye michuano hiyo ambayo Les Bleus watakuwa wakitetea taji walilotwaa nchini Urusi lazima atoe mchango wake.

Beki wa kati wa Manchester United, Varane hatarajiwi kucheza soka la klabu yoyote hadi fainali za Qatar 2022 zianze, baada ya kupata jeraha la mguu, huku Pogba akirejea kwenye mazoezi na Juventus baada ya kufanyiwa upasuaji wa goti lakini hataharakishwa kurudi uwanjani.

"Ni wazi kabisa," alisema Deschamps katika mahojiano na tovuti ya Ufaransa ya Brut.

"Sijawahi kuanza mashindano makubwa na mchezaji majeruhi, hata kama kuna baadhi ya watu ambao wanaweza kutoa mifano kutoka 2018 na mabeki wetu wa pembeni ambao walikuwa Benjamin Mendy na Djibril Sidibe.

"Walipona. Baada ya hapo, ni kuhusu hali ya kimchezo. Na kati ya wakati nilipotengeneza orodha na kile ambacho kilipaswa kutokea.

"Lakini kwenda kwenye mashindano makubwa na wachezaji ambao hawako tayari, tunajiweka kwenye wakati mgumu."

Pogba bado anasubiri kufanya vyema uwanjani katika kipindi chake cha pili akiwa Juventus, baada ya kujiunga tena na wababe hao wa Serie A kutoka Manchester United.

# Henry: Barcelona bila Xavi mambo yangekuwa magumu

**LONDON, England**

THIERRY Henry amepuuzilia mbali mapendekezo kwamba Xavi si kocha sahihi wa Barcelona, au kwamba kibarua kimekuja mapema sana tofauti na uzoefu wake kwenye ukocha, akidai mambo kwa sasa yangekuwa mabaya zaidi bila gwiji huyo.

Baada ya kunoa meno yake kama kocha katika klabu ya Al-Sadd ya Qatar, Xavi aliteuliwa na Barca chini ya mwaka mmoja uliopita.

Tayari aliiongoza timu hiyo kumaliza nafasi ya pili kwenye msimamo wa Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga, baada ya mwanzo mbaya chini ya Ronald Koeman na kuepusha kukosa nafasi ya kushiriki Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Barcelona wamekuwa katika kiwango kizuri cha nyumbani hadi sasa msimu huu 2022/23, wakishinda michezo yote isipokuwa miwili kati ya 11 na wamekuwa kileleni mwa msimamo hadi walipofungwa na Real Madrid kwenye Clasico mwezi huu.

Lakini Ligi ya Mabingwa Ulaya imekuwa na habari tofauti, kwani wameshindwa kushinda mechi yoyote kati ya nne zilizopita na wameshuka hadi kwenye Ligi ya Europa kwa mwaka wa pili mfululizo.

Xavi amekuwa akikabiliana na hali ya msukosuko wa kifedha katika kipindi chote alichokuwa madarakani na amelazimika kutafuta njia za kuunda kikosi kipya kufuatia shughuli nyingi za uhamisho wa majira ya joto.

Licha ya hali ya kifedha ya klabu hiyo kuimarika kwa muda mfupi, bado kuna uwezekano wa Barca kuendelea kuwa kwenye wakati mbaya siku zijazo baada ya onyo la hivi majuzi kutoka kwa rais wa LaLiga, Javier Tebas.

Henry, ambaye alicheza na Xavi kwa misimu mitatu katika kilele cha mafanikio ya klabu chini ya Pep Guardiola, amemuunga mkono mchezaji mwenzake wa zamani kuendelea kuongoza meli hiyo.

"Mwisho wa siku, matokeo huwa yanahesabiwa na ndivyo tulivyoona hivi majuzi nchini England kwa kutimuliwa kwa Steven Gerrard," alisema Mfaransa huyo akinukuliwa na CBS Sports.

"Lakini kama kwa wakati huu Barcelona wangekuwa na kocha mwingine anayesimamia basi volcano ingelipuka. Ingekuwa mbaya zaidi kuliko sasa."

## HABARI MICHEZO

303,118/-

# AZAM YAANZA KUOTA UBINGWA

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kuifunga Simba bao 1-0 kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa juzi, klabu ya Azam imesema msimu huu malengo yao ni ubingwa na kama walishindwa kabisa basi kukamata nafasi ya pili itakayowawezesha kucheza Ligi ya Mabingwa msimu ujao, huku ikitamba kuwa wataiengua timu moja kati ya Simba au Yanga kwenda kwenye nafasi ya tatu.

Kaimu Afisa Habari wa klabu hiyo, Hasheem Ibwe amesema ushindi dhidi ya Simba umewaonyesha kuwa wana uwezo mkubwa wa kutwaa ubingwa au kushika nafasi ya pili na kama wakifanikiwa hivyo, ina maana moja kati ya timu hizo itashuka hadi nafasi ya tatu msimu huu.

Kuhusu mechi juzi alisema amefurahi timu yake kuibuka na ushindi dhidi ya timu ngumu na nzuri ya Simba

"Simba ni timu nzuri sana na ngumu kukabiliana nayo, hivyo ni lazima nifurahi.

Kuifunga timu kubwa nzuri na bora kama ya Simba wakati tukiwa tumedharauliwa, wapo waliovuka mipaka wakisema hili ni tawi la Simba, wapo walitutusi kuwa tumeitoa mechi Chamazi kuipeleka Uwanja wa Benjamin Mkapa ili tuipoteze, lakini sasa kimya, wakibisha turudiane tena, hata tukirudiana nao tutawafunga," alitamba.

Ibwe amewasifu mashabiki wa Azam waliokuwa wamedharauliwa na kubezwa kuelekea kwenye mechi hiyo na hata wakati wanawasili uwanjani.

"Kikubwa kilichonitoa machozi ni mashabiki wachache wa Azam ambao waliungwa mkono na Yanga, walidharauliwa, lakini wakatoka uwanjani mashujaa.

Kituo kinachofuata ni Ihefu, tutajitahidi kufanya vema, tutakutana nao Azam Complex, tunaamini tutaiweza baada ya kushinda mechi yetu dhidi ya Simba.

Tunataka kabla ya mechi saba tuwe tumefuzu kucheza Ligi ya Mabingwa Afrika huku tukiutafuta ubingwa na kuengua mmoja hadi nafasi ya tatu," alisema.

Ilikuwa ni mechi ya kwanza Simba kupoteza msimu huu baada ya mechi sita, na ya nne kushinda kwa upande wa Azam ikikwea hadi kwenye nafasi ya pili tatu ya msimamo kwa pointi 14, ikizidiwa na Wekundu hao wa msimbazi kwa mabao ya kufunga.




Mshambuliaji wa Simba, Kibu Denis (kushoto), akiwania mpira na Winga wa Azam FC, Bruce Kangwa, wakiwania mpira wakati wa mchezo wa ligi Kuu uliopigwa Uwanaja wa Benjamin Mkapa mkoani Dar es Salaamm juzi, Azam imeibuka na ushindi wa bao 1-0. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Yanga yapania rekodi leo

INATOKA UK. 32

kukwea hadi kwenye nafasi ya pili ya msimamo.

Kocha Msaidizi wa Yanga Cedric Kaze amesema kuwa timu ya Geita Gold imeimarika kwa siku za karibuni na tangu msimu uliopita mechi yetu dhidi ya timu hiyo haikuwahi kuwa rahisi.

Itakuwa ngumu ya kutumia nguvu, lakini tumejiandaa kisaikolojia kuingia kwenye mchezo huo ili kusaka pointi tatu.

Ni rekodi nzuri, lakini siyo namba ya michezo, unaweza usifungwe lakini usifikishe malengo, malengo ni kutwaa ubingwa na siyo kumaliza bila kufungwa.

Amesema kuwa mbali na Mwamnyeto, pia Khalid Aucho hawatokuwepo.

Kocha wa Geita Gold Mathias Wandiba amesema wamejiandaa kikamilifu, wanaheshimu ubora wa Yanga, lakini timu yao pia ina wachezaji bora, tunajua tunakwenda kucheza mechi muhimu, tutahakikisha tunashinda, tupo nyumbani, hatuhitaji kupoteza, kikubwa tumejiandaa kwa mchezo huo.

# Mgunda: Uchovu Uliimaliza Simba

INATOKA UK. 32

vu na kuwataka kutumia fursa hiyo kuonesha uwezo wao nashukuru waliyafanyia kazi maelezo yangu," alisema Kally.

Alisema ushindi huo hautowavimbisha kichwa bali wataendelea kupambana kupata matokeo mazuri sababu kwa ubora na maandalizi waliyofanya hawastaili kuwa kwenye nafasi waliyopo hivi sasa.

Kwa ushindi wa juzi Azam FC sasa imepanda hadi nafasi ya nne kwenye msimamo wa ligi ikiwa na pointi 14 sawa na Simba iliyopo nafasi ya tatu huku mabingwa watetezi Yanga wakiwa kileleni mwa ligi hiyo kwa kukusanya pointi 17.


SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 29/10/22 | 17:00 | Hull City vs Blackburn | 2.59 | 3.19 | 2.74 |
| 02. 29/10/22 | 17:00 | Wigan vs Watford | 2.93 | 3.28 | 2.39 |
| 03. 29/10/22 | 17:00 | Preston vs Middlesbrough | 2.68 | 3.13 | 2.68 |
| 04. 29/10/22 | 17:00 | Huddersfield vs Millwall | 2.99 | 3.24 | 2.37 |
| 05. 29/10/22 | 17:00 | Brighton vs Chelsea | 2.94 | 3.29 | 2.38 |
| 06. 29/10/22 | 19:30 | Fulham vs Everton | 2.29 | 3.42 | 2.97 |
| 07. 29/10/22 | 19:30 | Eintracht Frankfurt vs Borussia Dortmund | 2.93 | 3.52 | 2.25 |
| 08. 29/10/22 | 21:30 | St. Pauli vs SV Darmstadt | 2.53 | 3.53 | 2.58 |
| 09. 30/10/22 | 15:00 | AJ Auxerre vs AC Ajaccio | 2.45 | 3.07 | 2.97 |
| 10. 30/10/22 | 15:30 | Hannover vs Karlsruher SC | 2.41 | 3.43 | 2.79 |
| 11. 30/10/22 | 15:30 | Sandhausen vs Eintracht Braunschweig | 2.63 | 3.22 | 2.68 |
| 12. 30/10/22 | 15:30 | Paderborn vs Hamburger SV | 2.28 | 3.73 | 2.79 |
| 13. 30/10/22 | 16:15 | FC Sion vs FC Zurich | 2.39 | 3.48 | 2.79 |
| 14. 30/10/22 | 17:00 | Brest vs Reims | 2.40 | 3.33 | 2.83 |
| 15. 30/10/22 | 18:30 | Boavista vs Vizela | 2.50 | 3.25 | 2.80 |
| 16. 30/10/22 | 19:00 | Sandefjord vs Ham-Kam | 2.58 | 3.37 | 2.63 |
| 17. 30/10/22 | 19:05 | Lorient vs Nice | 2.57 | 3.26 | 2.67 |

MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAMOSI - 29/10/2022

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:00 | 4332 | Tanzania Prisons vs Namungo | 2.34 | 2.58 | 3.50 |
| 14:00 | 5037 | Bristol City vs Swansea | 2.24 | 3.36 | 2.97 |
| 14:30 | 2523 | Leicester vs Manchester City | 8.01 | 5.27 | 1.31 |
| 14:30 | 2857 | Konyaspor vs Kasimpasa | 1.69 | 3.79 | 4.59 |
| 15:00 | 4337 | Cagliari vs Reggina | 2.18 | 3.17 | 3.27 |
| 16:00 | 1194 | Napoli vs Sassuolo | 1.26 | 5.73 | 8.70 |
| 16:00 | 4614 | Geita Gold FC vs Young Africans | 4.38 | 3.02 | 1.85 |
| 16:30 | 1062 | VfL Wolfsburg vs VfL Bochum | 1.64 | 3.96 | 4.56 |
| 16:30 | 2411 | RB Leipzig vs Bayer Leverkusen | 1.77 | 3.91 | 3.86 |
| 16:30 | 2995 | Stuttgart vs Augsburg | 1.77 | 3.71 | 4.06 |
| 16:30 | 4319 | Bayern Munchen vs Mainz | 1.22 | 6.36 | 9.54 |
| 17:00 | 1305 | Crystal Palace vs Southampton | 1.90 | 3.42 | 3.82 |
| 17:00 | 1819 | Brentford vs Wolverhampton | 2.14 | 3.36 | 3.16 |
| 17:00 | 2165 | Brighton vs Chelsea | 2.82 | 3.22 | 2.41 |
| 17:00 | 2952 | Norwich City vs Stoke City | 1.79 | 3.47 | 4.26 |
| 17:00 | 3186 | Rangers vs Aberdeen | 1.33 | 5.16 | 7.74 |
| 17:00 | 3435 | Randers vs Copenhagen | 3.08 | 3.43 | 2.18 |
| 17:00 | 3441 | Bournemouth vs Tottenham | 4.77 | 3.78 | 1.65 |
| 17:00 | 3791 | Shakhtar Donetsk vs Oleksandria | 1.35 | 4.67 | 6.81 |
| 17:00 | 4098 | Newcastle vs Aston Villa | 1.78 | 3.61 | 4.15 |
| 17:00 | 4211 | Burnley vs Reading | 1.57 | 3.98 | 5.18 |
| 17:00 | 4767 | Cardiff vs Rotherham | 1.98 | 3.32 | 3.66 |
| 17:00 | 4802 | St Johnstone vs Kilmarnock | 2.49 | 2.94 | 2.99 |
| 17:00 | 4895 | Zulte Waregem vs Standard Liege | 2.94 | 3.59 | 2.19 |
| 17:00 | 5252 | Dundee Utd vs Motherwell | 2.59 | 3.14 | 2.69 |
| 17:15 | 4596 | Cadiz CF vs Atletico Madrid | 6.00 | 3.70 | 1.58 |
| 17:15 | 5448 | Genoa vs Brescia | 1.49 | 4.05 | 6.13 |
| 17:30 | 3508 | Santa Clara vs Porto | 7.38 | 4.49 | 1.40 |
| 18:00 | 1799 | Paris St Germain vs Troyes | 1.12 | 8.15 | 17.46 |
| 18:00 | 4236 | RB Salzburg vs TSV Hartberg | 1.16 | 6.62 | 11.68 |
| 19:00 | 2403 | Lecce vs Juventus | 4.55 | 3.36 | 1.78 |
| 19:00 | 4397 | Grasshoppers vs FC Luzern | 2.83 | 3.53 | 2.28 |
| 19:15 | 2756 | Kortrijk vs Cercle Brugge | 3.53 | 3.58 | 1.95 |
| 19:15 | 5224 | KVC Westerlo vs St Truiden | 2.15 | 3.28 | 3.28 |
| 19:30 | 2827 | Eintracht Frankfurt vs Borussia Dortmund | 2.78 | 3.52 | 2.29 |
| 19:30 | 2972 | Sevilla FC vs Rayo Vallecano | 1.96 | 3.30 | 3.90 |
| 19:30 | 3761 | Fulham vs Everton | 2.29 | 3.32 | 2.92 |
| 19:45 | 1291 | Sparta Rotterdam vs Fortuna Sittard | 1.99 | 3.51 | 3.41 |
| 20:00 | 3939 | Benfica vs GD Chaves | 1.16 | 6.96 | 13.92 |
| 20:00 | 5862 | Nimes vs Bastia Borgo | 1.67 | 3.64 | 4.99 |
| 20:15 | 5217 | Beitar Jerusalem vs Hapoel Haifa | 2.63 | 3.26 | 2.42 |
| 21:30 | 4610 | Servette Geneva vs FC Lugano | 1.98 | 3.49 | 3.54 |
| 21:45 | 1638 | Inter vs Sampdoria | 1.22 | 5.91 | 10.84 |
| 21:45 | 3985 | Liverpool vs Leeds | 1.27 | 5.78 | 8.17 |
| 21:45 | 4123 | Brugge vs Oostende | 1.27 | 5.78 | 8.97 |
| 22:00 | 2201 | GO Ahead Eagles vs SBV Excelsior | 1.72 | 3.86 | 4.16 |
| 22:00 | 4048 | Strasbourg vs Marseille | 2.84 | 3.33 | 2.37 |
| 22:00 | 4700 | Valencia vs Barcelona | 4.66 | 4.10 | 1.64 |
| 22:30 | 5491 | FC Arouca vs Sporting Lisbon | 6.56 | 4.28 | 1.45 |
| 23:30 | 4116 | Academia Cantolao vs Ayacucho | 2.07 | 3.17 | 3.31 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

Michezo

Jumamosi Oktoba 29, 2022

Nipashe



UKURASA 29

## Ten Hag: Ronaldo atafunga zaidi




Mkurugenzi wa Bodi ya Wakurugenzi ya Mo Assuarance, Fatma Dewji (kulia) akikabidhi mfano wa hundi ya Sh Milioni 250 kwa Afisa Mtendaji Mkuu Mkuu wa Simba, Barbara Gonzalez kwa ajili ya bima ya matibabu ya wachezaji, benchi la ufundi na waajiriwa wote wa klabu hiyo. Wanaoshuhudia kutoka kulia ni Gregory Fortes , Afisa Mtendaji Mkuu Mo Assuarance. **PICHA: SAADA AKIDA**

# MGUNDA: UCHOVU ULIIMALIZA SIMBA

## ●●●Asema asilaumiwe yeyote, Ongala asema sasa wameanza kazi rasmi...

**Na Saada Akida**

KAIMU Kocha Mkuu wa Simba, Juma Mgunda amesema sababu ya kupoteza mchezo wa Ligi Kuu dhidi ya Azam FC ni uchovu waliokuwa nao wachezaji wake baada ya kucheza mechi mfululizo bila kupata muda wa kutosha wa kupumzika.

Huo ni mchezo wa kwanza kwa Simba kupoteza msimu huu na kocha huyo ameeleza kuwa kipigo hicho hapaswi kumlaumu mchezaji wala kiongozi yeyote sababu hayo ni matokeo ya mpira.

Akizungumza baada ya mchezo huo, Mgunda alikiri mchezo ulikuwa mgumu na walijitahidi kupambana lakini wakajikuta wanapoteza pointi tatu ambazo waliingia uwanjani wakiwa na lengo la kuzichukua ili kurudi kileleni.

"Nawapongeze Azam kwa ushindi walicheza vizuri na walistaili kushinda, lakini kwa upande wetu tulijitahidi kwa kila namna tulitengeneza nafasi nyingi tukashindwa kuzitumia ndio mchezo wa mpira unavyokuwa tumekubali matokeo na tunarudi kujipanga kwa ajili ya mechi zijazo," alisema Mgunda.

Kocha huyo alisema uchovu waliokuwa nao wachezaji wake pamoja na ratiba ngumu vinaweza kuwa sababu ya kushindwa kupata matokeo mazuri lakini hataki hicho kiwe kisingizio cha kupoteza mchezo huo.

Kwa upande wa Kocha Mkuu wa Azam FC, Kally Ongala aliwapongeza wachezaji wake kwa kucheza kwa kujitoa na kufanikiwa kupata ushindi huo ambao utawaongezea ari katika mechi zinazo kuja.

Kally alisema pamoja na ushindi lakini haukuwa mchezo rahisi kutokana na ubora waliokuwa nao Simba, ingawa anafurahi kuona vijana wake wamezitumia vyema mbinu alizowapa na kufanikiwa kupata matokeo hayo.

"Wakati napewa timu ari ya kupambana kwa wachezaji ilikuwa chini sana lakini baada ya uongozi kunikabidhi timu nilijaribu kuongea nao kwa utuli-

INAENDELEA UK. 31

Nabi

## Yanga yapania rekodi leo

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI Yanga ikipania kuendeleza rekodi ya kutopoteza mechi ya 45 mfululizo ya Ligi Kuu Tanzania Bara leo itakapovaana na Geita Gold kwenye Uwanja wa CCM Kirumba, Mwanza, wenyeji wa mchezo huo wameapa kumaliza mfululizo wa timu hiyo kucheza mechi bila kupoteza.

Ofisa Habari wa Klabu ya Yanga, Ali Kamwe amesema baada ya mechi dhidi ya KMC, wanarejea wakiwa na baadhi ya wachezaji ambao hawakuwepo kwenye mechi iliyopita.

"Tunajua ugumu wa mechi, haitokuwa rahisi kwa sababu Geita Gold ni timu ngumu, lakini sisi tuna wachezaji wazuri na maandalizi bora zaidi. Kuna waliosema kuwa tunataka kuendeleza rekodi yetu ya kucheza mechi mfululizo bila kupoteza, ni kweli hatujapoteza, lakini hatujiandai kwa ajili ya kulinda rekodi, ila tumefanya maandalizi ya mchezo husika," alisema Kamwe.

Wachezaji ambao walikosekana kwenye mechi dhidi ya KMC Jumatano iliyopita ni Fiston Mayele, Khalid Aucho, Kibwana Shomari ambao walipumzishwa, na Bernard Morrison ambaye alikuwa anatumikia kifungo cha mechi tatu.

"Kwenye mechi hii hatujaja na Mwamnyeto kwa sababu ya plan tu ya mwalimu, tuna mechi nyingi mfululizo hivyo kwa plani yake na ushahuri wa wataalam wa afya, wameshauri tuwe makini kuhakikisha tunalinda afya zao kwa kuwapumzisha ili tupate ufanisi wao kwa asilimia mia moja," alisema Kamwe.

Kwa upande wa Geita Gold, Kaimu Katibu Mkuu Liberatus Pastory alisema maandalizi ya mechi hiyo yamekamilika chini ya Kocha Mkuu, Fred Felix Minziro.

"Mechi yetu itachezwa CCM Kirumba saa 10:00 jioni, ninachoweza kusema Geita Gold tumeandaa timu kwa ajili ya kuleta ushindani, hata kama huko nyuma tulipoteza dhidi ya Simba au Yanga, lakini hatukupoteza kirahisi, tulileta ushindani mkubwa, tunaamini tutapata matokeo na tutakuwa timu ya kwanza kuifunga Yanga na kuzima ile rekodi yao ya kuwa timu isiyofungwa," alisema Liberatus.

Yanga ipo kileleni ikiongoza ligi kwa pointi 17, na ikishinda mechi hiyo itafikisha pointi 20 na kuzidi kukwea kileleni, wakati Geita Gold kama itafanikiwa kushinda, mbali ya kuzima rekodi ya Yanga kucheza mechi ya 45 bila kupoteza, itakuwa imefikisha jumla ya pointi 16 na

INAENDELEA UK. 31

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >